**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Saba – Tarehe 5 Aprili, 2006**

(*Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi*)

**D U A**

*Spika (Mhe. Samwel John Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Taarifa ya Mwaka wa Hesabu zilizokaguliwa na Hifadhi za Taifa Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 [*The Annual Report and Audited Accounts of the Tanzania National Parks for the year ended 30th June, 2005*]

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:-**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Sukari Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005 (*The Annual Report and Accounts of the Sugar Board of Tanzania for the year ended 30th June, 2005)*

Taarifa ya Ishirini ya Utendaji na Hesabu za Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa Mwaka ulioishia tarehe 31 Machi, 2005 (*The 20th Annual Performance Report and Audited Accounts of the Tanzania Tobacco Board for the year ended 31st March, 2005)*

**MASWALI NA MAJIBU**

**Na. 90**

**Chakula cha Njaa Wilaya Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Mpwapwa ina Tarafa tatu (3) Kata Kumi na nane (18) na Vijiji Themanini na nne (84) na wakazi wapatao 254,000 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, na kwa kuwa katika tathmini ya tatizo la njaa iliyofanyika Januari, 2006 imeonekana kuwa watu wengi wana tatizo kubwa la njaa kwa mwezi Februari, 2006 Wilaya hiyo ilipata tani 449 tu na mahitaji halisi ni zaidi ya tani 2000 kwa mwezi.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mgao wa chakula cha njaa ili kupunguza tatizo la njaa Wilaya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, naomba kutoa maeleo mafupi kama ifuatavyo:-

Serikali kwa kutumia Timu ya Usalama wa Chakula nchini yaani *Food Security Information Team (FSIT)* na wadau wengine ilifanya tathmini ya kina ya kuainisha maeneo na watu ambao wangeathirika na upungufu wa chakula nchini. Kazi ya kutathmini ilifanywa kwa kushirikisha wataalam kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mamlaka ya Hali ya Hewa na Taasisi ya Chakula na Lishe. Wengine ni kutoka Shirika la Chakula na Kilimo Duniani yaani *Food and Agriculture Organisation (FAO*), Mpango wa Chakula Duniani yaani *World Food Program (WFP)*, Mashirika yasiyo ya Kiserikali wakiwemo *Famine Early Warning System Network (FEWSNET*) na Mashirika yanayojihusisha na Huduma za Kibinadamu katika ngazi za Mikoa na Wilaya. Wengine ni wataalam kutoka katika Mikoa, Wilaya, Kata, Vijiji na Mashirika kadhaa yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa mapendekezo na ushauri wa Wataalam hao ndio ulikuwa Msingi wa kufanya maamuzi ya kugawa chakula cha njaa.

Tathmini ilibainisha kwamba jumla ya watu 3,764,843 wangekuwa na upungufu wa chakula na wangehitaji tani 99,676 za nafaka kwa miezi miwili kati ya February na Aprili, 2006.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa George M. Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa na watu 254,000. Kulingana na kiwango cha ongezeko la watu, idadi ya watu katika Wilaya hii kwa takwimu za mwaka huu ni watu 297,013. Tathmini ya mwezi Januari, 2006, ilibanisha kuwa, wananchi wapatao 32,985 kati ya wakazi hao 297,013 wana upungufu wa chakula na wanahitaji tani 792, kati ya mahitaji hayo tani 673 ni chakula cha bei nafuu na tani 119 chakula chakula cha bure.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha mahindi yaliyotolewa ya tani 499 kilizingatia uwezo wa Serikal ikilinganishwa na mahitaji makubwa kitaifa (99,679) na kiasi halisi cha mahindi yaliyokuwepo maghala ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula (56,744).

Ili kukidhi mahitaji ya chakula kwa watu wenye upungufu wa chakula ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa, Serikali imeagiza gani 42,000 za mahindi kutoka nje. Pamoja na hatua hii, Serikali kupitia Viongozi wa Wilaya ya Mpwapwa wanafuatilia kwa karibu hali ya upatikanaji chakula katika maeneo hayo, na Serikali haitasita kutoa chakula kulingana na hali halisi itakayojitokeza.

Napenda nimshukuru Mheshimiwa Lubeleje, kwani ni yeye binafsi ambaye alikuja ofisini kwetu akatoa *report* juu ya upungufu wa chakula katika Wilaya yake ya Mpwapwa. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo la nyongeza.

Kwanza, napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya kupata taarifa kwamba Wilaya ya Mpwapwa ina tatizo kubwa sana la njaa kwa busara zake alitembelea Wilaya ya Mpwapwa na kuona tatizo hilo na pia niishukuru Serikali kwa hizo tani 449 ambazo nathibitisha kwamba zimefika.

Sasa je, kwa maeneo ambayo yamebaki kama Naibu Waziri alivyojibu ni lini wananchi hao watapata chakula kwa sababu tatizo la njaa bado linaendelea katika Wilaya ya Mpwapwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyokwisha jibu katika swali la Msingi mahitaji ya chakula kwa Wilaya ya Mpwapwa ilikuwa ni tani 792 lakini katika mgao tulioupeleka kwa ajili ya matumizi kati ya Februari na Aprili tulipeleka tani 449. Kwa hiyo, hizo tani za ziada ni mategemeo yetu kwamba katika kipindi hiki cha pili ambacho tutakuwa tunategemea kwamba tutakuwa tumefanya tena tathmini tutawapelekea tani zilizobaki na kwa hiyo maeneo yaliyobaki yatapata chakula.

**Na. 91**

**Kuwezesha Kamati za UKIMWI**

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa wa UKIMWI umekuwa ukishambulia kwa kasi sana maeneo ya Vijijini, na kwa kuwa, Serikali iliunda Kamati za Kudhibiti UKIMWI Wilayani, katika Kata na Vijiji na kwa kuwa Kamati za Kata na Vijiji zimekuwa zikishindwa kukutana na kufanya kazi yake kwa sababu ya ukosefu wa fedha.

Je, Serikali inachukua hatua zipi ili kuwezesha Kamati hizo ziweze kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mbunge Viti Maalum, kutanguliza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inetoa agizo na mwongozi wa kuundwa Kamati za Kudhibiti UKIMWI katika kila Halmashauri ya Wilaya. Aidha, zipo Kamati za Kata na Vijiji kwa madhumuni hayohayo. Agizo hilo lilitolewa Februari, 2003 na Kamati ziliundwa kisheria, Kamati za UKIMWI zinafanya kazi kama zilivyo Kamati nyingine za Halmashauri na vikao vyao vinagharamiwa na Halmashauri zenyewe. Hata hivyo, pale ambapo fedha zaidi inahitajika kutekeleza mpango au afua waliyobuni Halmashauri yenyewe, Serikali Kuu inaweza kusaidia kwa hali na mali. Ni kwa Msingi huu, Halmashauri zinatakiwa kuingiza katika Makadirio ya Bajeti zao gharama za udhibiti wa janga la UKIMWI ili zipatiwe fedha kutoka Hazina, wafadhili au asasi mbalimbali. Baada ya utangulizi huo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Kamati za Udhibiti wa UKIMWI zinatakiwa kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu kupata fedha kutoka Halmashauri husika, kama Kamati nyingine zinavyofanya. Halmashauri zinatakiwa kugharamia Kamati zao zote bila ubaguzi. Napenda kutoa wito kwamba Kamati za kudhibiti UKIMWI zisionekane kuwa ni yatima kwa sababu tu zilichelewa kuundwa. Aidha, katika mwaka wa fedha ujao ni mategemea Halmashauri zote zitakuwa zimetenga fedha kwa shughuli za kudhibiti UKIMWI na hivyo kuwezesha Kamati zake zote kufanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa zaidi.

**MHE. MERYCE MUSSA EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika pamoja na majibu mazuri ya Waziri napenda kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, amesema kuwa Kamati hizi ziko chini ya Halmashauri na Halmashauri inatakiwa izigharamie.

Lakini pia kwa kuwa, janga hili ni la ulimwengu mzima mimi ningependa kumuuliza Waziri kuwa je, sasa hivi hawaoni kwamba kuna umuhimu wa Wizara hii kuzisukuma Halmashauri ziweze kufuatilia Kamati hizi kwa karibu ili ziweze kufanya kazi ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI (MHE. DR. LUKA J. SIYAME):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Meryce Emmanuel kama ifuatavyo:-

Katika jibu langu la Msingi nilitamka kwamba kwa sababu Kamati za UKIMWI ziliundwa na ziko kihalali kama Kamati nyingine zozote na inabidi katika bajeti ya msimu ujao wa mwaka ujao zitengewe fedha kwa ajili ya matumizi yake ya shughuli zake zote basi labda hilo ilikuwa ni jibu la kiungwana kwamba kwa kweli tunasisitiza kwamba kila Halmashauri ni lazima itenge pesa kwa ajili ya shughuli za Kamati za UKIMWI.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza na aidha namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika kwa kuwa tumepokea fedha nyingi na kwa taarifa mbalimbali zilizoko ni zaidi ya bilioni 50 kutoka *Global Fund* pamoja na mfuko wa Rais Bush na kwa kuwa, waathirika na hata yatima wengi wanaotokana na UKIMWI wapo vijijini na kwa kuwa Kamati hizi ndizo zinazowajua na ndizo zinazokuwa karibu nao. Ni lini fedha hizo sasa zitaelekezwa huko kuliko kwenye semina nyingi zinazofanyika katika ngazi za juu ambazo haziwahusishi wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, MAAFA NA KAMPENI DHIDI YA UKIMWI:-** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Dr. Slaa Mbunge wa Karatu kama ifuatavyo:-

Nakubali fedha nyingi zimepokelewa kutoka kwa wafadhili mbalimbali kama *Global Funds* na kwa taratibu ya fedha hizo nyingi kupitia ama *TACAIDS* ama *National Program for AIDS control* zinapelekwa kwenye mikoa ama zile *agencies* ambazo zimeteuliwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za UKIMWI.

Pamoja na mambo hayo, semini ni sehemu tu ya matumizi ya pesa hiyo kwa ajili ya advocacy na sensitisation za hao watu ambao watatumika kuhudumia hao wananchi lakini kimsingi shughuli zote zinalenga kuhudumia hao waathirika ambao wako vijijini na kwenye vitongoji ama kwenye kaya.

Serikali imebuni mipango mbalimbali ya kuweza kuwahudumia hao watu kupitia ama kwa huduma zitolewazo mahospitali ama kwa huduma za kinga na ama kwa wale watoa huduma kwenye majumba yaani *home based care system*. Kwa hiyo ni kwa taratibu hizo fedha hizo zinatumika.

**Na. 92**

**Kuchelewesha Mishahara ya Walimu**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Walimu wa shule za Msingi na Sekondari wanapoanza kazi bado wanakabiliwa na tatizo la kuchelewa kuanza kupata mishahara yao.

(a) Je, Serikali inaifahamu kero hiyo?

(b) Kama inalifahamu tatizo hilo je inasemaje?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo (Viti Maalum) lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kero za walimu wa shule za Msingi ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupata mishahara yao wanapoanza kazi mara baada ya kutoka vyuoni. Ucheleweshaji wa mishahara kwa walimu wapya huwasababishia kero na usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kero na usumbufu unaojitokeza katika suala zima la mishahara kwa walimu wapya hutokana na urasimu uliopo katika kukamilisha taratibu za ajira zao. Mwalimu anapoajiriwan na kupangiwa kituo cha kazi anatakiwa kujaza *form EB1* ambayo inasaini wa na Mkuu wa Shule na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya kwa wale walimu ambao ni wa shule za Msingi, kwa walimu wa shule za Sekondari *form* hiyo huwasilishwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Mafunzo ya Ufundi kwa shule za Sekondari baada ya hapo *form* ya walimu huwasilishwa ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na hatimaye Wizara ya Fedha.

Hii inatokana na kuwa ajira za walimu wapya zinahusisha Wizara zifuatazo:-

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua mlolongo huu, Ofisi yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu inaliangalia suala hili na namna ya kuboresha utaratibu wa ajira kwa walimu wapya. Nafurahi kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeunda Kamati Maalum ya kushughulikia tatizo hilo. Kamati hiii inajumuisha Makatibu Wakuu kutoka Wizara hizo nne. Nampongeza Mheshimiwa Diana Chilolo, kwa kuwajali walimu wenzake. (*Makofi*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na pongezi alizonipa nina swali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa, mpaka sasa bado kuna malimbikizo ya mishahara ya walimu ambao walichelewa kuingia kwenye *Payroll.* Je, Serikali inasema nini kuhusu malimbikizo hayo ili walimu waweze kukidhi haja ya mahitaji yao kwani wako wengi ambao hata vitanda vya kulalia hawana?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo.

Kama nilivyosema kwenye jibu langu la Msingi kwamba suala hili sasa hivi linashughulikiwa kwa karibu na Wizara zote nne kwa hiyo, hiyo Kamati ya Makatibu Wakuu itakapokutana itaangalia pamoja mambo mengine ni pamoja na hayo malimbikizo ya walimu. Suala hili linashughulikiwa kikamilifu. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nina swali la nyongeza.

Pamoja na Serikali kukiri kujua tatizo la mishahara ya walimu na malimbikizo ya madeni ya walimu, Mheshimiwa Naibu Waziri ulipata kutamka ndani ya Bunge hili kiasi ambacho kimekuwa ni madeni ya malimbikizo ya walimu na siku iliyofuatia Chama cha Walimu Tanzania Mkoa wa Dar es Salaam ulikanusha taarifa yako.

Mheshimiwa Spika, ni nini usahihi wa deni halisi la walimu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imekubali kwamba tatizo la ucheleweshaji wa mishahara ya walimu lipo. Pili lile suala ambalo walimu wamekanusha ni sahihi kama nilivyosema awali.

Katika jibu langu nilisema kwamba malimbikizo yaliyohakikiwa ni shilingi bilioni 12.8. Malimbikizo yaliyolipwa ni shilingi bilioni 2.5. Wakati malipo yaliyobakia ni shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Spika, zile milioni 200 nilisema kwamba zipo Hazina na kwa sababu yale malimbikizo yalikuwa ni ya muda mrefu kuanzia mwaka 1999 mpaka 2004 chochote kinaweza kikatokea.

Mheshimiwa Spika, zile shilingi milioni 200 ni za walimu waliofariki ambao watu wao au wale warithi wao hawajafuatilia kule Hazina na hizo ni shilingi milioni 121. Shilingi milioni 70 zilirudishwa Hazina kwa vile hundi zilizochacha. Kwa hiyo, huo ni msimamo halisi wa Serikali na taarifa hiyo ni sahihi kabisa. (*Makofi*)

**Na. 93**

**Barabara Kuwekwa Lami**

**MHE. JOYCE M. MASUNGA** aliuliza:-

Kwa kuwa, sasa Manispaa ya Shinyanga inaunganishwa na Miji mingine nchini kwa ujenzi wa barabara ya lami ya Mwanza – Dodoma – Dar es Salaam ili kutimiza ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais Mkoani Shinyanga wakti wa kampeni mwezi Oktoba, 2005:-

(a) Je, ni lini barabara za Mji wa Shinyanga zitawekwa lami, ili barabara kuu ya lami inayojengwa isiishie kupita kwenye mji wenye barabara za vumbi tupu?

(b) Je, ni lini Serikali itaunganisha kwa barabara ya lami Mji mdogo wa *Old Shinyanga* kutoka barabara Kuu inayojengwa kupitia Mji wa Shinyanga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joyce Masunga, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango madhubuti wa kuziwekea lami barabara za Manispaa ya Shinyanga kwa awamu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara (*Road Funds*) kwa awamu mbalimbali. Katika mwaka huu wa fedha, Serikali kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imetenga kiasi cha shilingi 432,000,000/= kwa ajili ya kuweka lami kilomita mbili tu za Mji wa Shinyanga. Fedha hii tayari imepelekwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa na mchakato wa kumpata Mkandarasi wa kufanya kazi hii umeanza kufanyika.

Pia Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga imetenga kiasi cha shilingi milioni kwa ajili ya kuzifanyia matengenezo barabara zilizoko chini yake. Barabara hizi zina urefu wa jumla ya kilomita 60, kilomita 2.2 ni za lami, kilomita 14 ni za changarawe na kilomita 30 ni za udongo.

(b) Mheshimiwa Spika,Mji wa *Old Shinyanga* upo kwenye barabara ya mkato inayoanzia Shinyanga Mjini kuelekea Mwanza kupitia kijiji cha Bubiki katika barabara hii ni ya Mkoa. Kwa sasa hivi ni azma ya Serikali kuziwekea lami barabara zote kuu zote nchini. Zoezi hili bado linaendelea na linatekelezwa kwa awamu kulingana na fedha itakavyopatikana.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Naibu Waziri na kumshukuru kwa kilomita mbili mbili za kutuwekea lami *inshallah Mungu* atatujalia lakini naomba niulize maswali miwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Shinyanga Mjini kwenda *Old Shinyanga* wananchi wengi wanatumia barabara hiyo wakiwemo wananchi wa kawaida, wakulima wanaoleta vyakula kutoka *Old* Shinyanga na vijiji ambavyo vipo pale pamoja na wauza

maziwa ambao nao wanatumia baiskeli na baiskeli hizo wanazozitumia mara nyingi huwa zinaharibika na vilevile barabara ni mbaya sana.

**WABUNGE FULANI:** Uliza swali.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** Naombeni tafadhali mimi ndiye nimeruhusiwa. Mheshimiwa Spika, naomba unilinde.

**SPIKA:** Naam! Endelea lakini liweke swali vizuri.

**MHE. JOYCE M. MASUNGA:** *Old Shinyanga* kuna hospitali ambazo zinaleta wagonjwa kwenda mjini Shinyanga kwa maana ya Hospitali ya Mkoa.

Kuhusu barabara hiyo, Je Mheshimiwa waziri haoni kwamba ni muhimu sana kutengenezwa kwa haraka kwa kuzingatia kwamb kuna vikosi vitatu vya jeshi ambavyo wanaishi mjini na kwenda *Old Shinyanga* na kawaida wanajeshi wanatakiwa wakati wa amani wapumzike na wakati wa vita wafanye kazi na kwamba sasa wakati wa amani barabara ni mbaya viuno vinakatika na wakati wa vita itakapokuwa tutakuwa sisi ndiyo tumewasababisha kutokufanya kazi yao vizuri? Tunaomba barabara hiyo iweze kutengenezwa kwa haraka iwezekanavyo. Swali la pili,….

**SPIKA:** Mheshimiwa nadhani linatosha sasa kwa sababu swali la kwanza limekuwa refu na lina vipengele virefu hata hivyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri endelea kujibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joyce Masunga, kama ifuatavyo:-

Ni kweli barabara hii imepita sehemu ambazo ni za kiulinzi wa kitaifa, lakini utengenezaji wake inatakiwa ushirikiano wa Wizara zinazohusika yaani Wizara ya Miundombinu pamoja na Wizara ya Ulinzi kwa pamoja wataliangalia suala hili kwa sababu hawawezi wakatengeneza bila Wizara hizi kushirikiana kwa pamoja.

**Na. 94**

***Artificial Grass* Kwenye Viwanja vya Michezo**

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD** aliuliza:-

Kwa kuwa, viwanja vingi hapa nchini vina *pitch* za mifumo ya zamani ya kuotesha majani tofauti na nchi nyingine:-

(a) Je, Serikali itafikiria kuweka *artificial grass* kwenye viwanja vyetu vya michezo ili kuwanusuru wachezaji wa mpira wa miguu wasichubuke pale wanapoanguka?

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kwa kufanya hivyo kutawalinda wachezaji wetu na afya zao?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL. N. BENDERA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rajab Soud, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haikuwa na wala haina mpango wa kupanda Majani Bandia yaani *artificial grasses* kwenye viwanja vyake vya michezo kwa sababu inatilia maanani utunzaji na uboreshaji wa mazingira ya nchi yetu hata kwenye viwanja vya michezo. "Majani Bandia" hayawezi kuwekwa kwenye kiwanja bila kubadilisha uoto wa ardhi, hali ambayo inaharibu mazingira ya viwanja.

(b) "Majani Asilia" kama yalivyo "Majani Bandia" hayawachubui wachezaji wetu, ila viwanja visivyokuwa na majani kabisa ndivyo vinavyoumiza na kuwachubua wachezaji.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri hasa yakiwa yamefika mahali ndipo akiwa ni mwanamichezo lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia zaidi afya za wachezaji na viwanja vyetu vilivyo hasa mambo ya *tetanus* na mambo mengine. Mheshimiwa Naibu Waziri anasema nini kuhusu hilo hivyo viwanja ambavyo havina majani atatusaidia vipi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO (MHE. JOEL. N. BENDERA)** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, mchezaji wangu wa timu ya Taifa kama ifuatavyo.

Ni kweli baadhi ya viwanja katika nchi kwa kweli havina majani na hili ni tatizo la wanaomiliki viwanja kwa kutokuvitunza vizuri, mimi nadhani nitoe wito kwa wananchi na wanaomiliki viwanja nchini tuwe na tabia ya kuvitunza viwanja vyetu kwa kupanda majani na kumwagilia maji ili viweze kuwa vizuri tuondokane na tatizo hilo. (*Makofi*)

**Na. 95**

**Ujenzi na Ukarabati wa Malambo**

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati au kupanua malambo ya Kabila, Mipa, Busangwa, Lagana, Mwamashimba na Busongo katika Wilaya ya Kishapu yaliyojengwa 2003/2004 ambayo ni madogo sana na hukauka mapema sana hivyo kutokuwa na msaada kwa wafugaji?

(b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, upo umuhimu wa dharura wa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kuwasaidia wananchi kukarabati majosho manane (8) Wilayani Kishapu kupitia mpango wake wa Kuendeleza Kilimo Wilayani (*District Agricultural Development Plan (DADP)* ili kudhibiti magonjwa ya mifugo katika Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mpendazoe, Mbunge wa Kishapu, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Ujenzi wa malambo nchini huzingatia mahitaji, aina ya matumizi na nia ya kutoa huduma ya upatikanaji wa maji mwanzo hadi mwisho wa mwaka. Hata hivyo, mara nyingi kumekuwepo na uhamishaji wa mifugo ya ziada kwenye maeneo yenye malambo au uanzishwaji wa kilimo cha umwagiliaji katika baadhi ya maeneo na kusababisha ongezeko la mahitaji ya maji ambayo hayakuwepo wakati wa usanifu. Aidha, ukame wa muda mrefu uliojitokeza miaka mitatu mfululizo hadi mwanzoni mwa mwaka 2006, ulisababisha malambo mengi kukauka.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara yangu kupitia utaratibu wake wa kuchimba malambo ya maji kwa ajili ya mifugo ilitoa jumla ya shilingi milioni 18 kwa ajili ya ujenzi wa malambo ya Mipa, Kabila, Ikonokelo, Sululu, Mwamadulu na Miyuguyu katika Wilaya ya Kishapu. Fedha hizo zilitolewa kwa mategemeo kuwa, Halmashauri ya Wilaya na wananchi wa Vijiji husika wangechangia kiasi kama hicho ili kufanikisha uchimbaji wa malambo. Katika utaratibu uliopo vijiji huchangia asilimia 20, Halmashauri asilimia 30 na Wizara yangu asilimia 50.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji, fedha zilizotolewa na Wizara yaani shilingi milioni 18 nilizozitaja zilitumika kujenga malambo matatu ya Ikonokelo, Miyuguyu na Mwamadulu. Mgodi wa Almasi wa Mwadui *(Mwadui Diamonds Mining Company)* nao ulichangia kujenga malambo ya Kabila na Mipa. Kutokana na upungufu wa fedha lambo la Sululu halikujengwa. Kazi hii haikuweza kukamilika kama ilivyopangwa kutokana na iliyokuwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini na wananchi wa Vijiji husika kushindwa kutoa michango yao. Tunatarajia ukarabati na upanuzi wa malambo haya pamoja na yale ya Busangwa, Lagana, Mwamashimba

na Busongo utakamilika punde michango ya wananchi wa Halmashauri itakapokuwa imetolewa kulingana na utaratibu niliouelezea.

(b)Mheshimiwa Spika, ni kweli pia upo umuhimu wa dharura wa kushirikiana na Halmashauri zote nchini na wadau wengine ili kukarabati majosho mabovu kupitia Mpango wa Kuendeleza Kilimo Wilayani ambamo Sekta ya Mifugo ipo kwa Kiingereza inajulikana *District Agricultural Development Plans (DADP)*. Ukarabati wa majosho umekuwa ukifanywa kwa njia ambayo ni shirikishi ambapo wananchi huibua miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukarabati wa majosho mabovu na mipango yao kuiwasilisha kwenye Halmashauri ya Wilaya husika kwa ajili ya kuombea fedha kupitia *DADP*.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiana na Halmashauri ya Wilaya yake katika kuwahamasisha wananchi kuibua miradi ya ukarabati wa majosho na hivyo kuchangia katika udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Serikali ipo tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kupitia Mpango wa *DADPs* kukarabati majosho manane aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge na mengine mengi yatakayopendekezwa na wananchi.

**MHE. FRED MPENDAZOE TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali ya Awamu ya Nne lengo lake kubwa katika Sekta ya Mifugo ni kuiendeleza ili iweze kuchangia kikamilifu katika uchumi wa Taifa na mapato ya wafugaji; na kwa kuwa, vilevile Serikali ya Awamu ya Nne inasisitiza zaidi ubora wa mifugo kwa wafugaji.

Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba upo umuhimu wa kidharura wa kuweza sasa kutoa ruzuku kwa madawa ya mifugo yakiwemo madawa yanayotumika kwa majosho ili kuinua tija katika Sekta hii ya Mifugo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa pembejeo nyingine Wizara yangu itaomba fedha kwenye bajeti yake ya mwaka huu 2006/2007 kwa ajili ya ruzuku ya madawa ya kuogeshea mifugo na kwa dalili zilivyo fedha hii inaweza ikapatikana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa vile nchi hii hatukuwa na utamaduni wa kutathmini athari za mazingira za malambo na mabwawa na ndiyo maana malambo mengi yamekuwa yanakauka. Je, Mheshimiwa Waziri atalithibitishia Bunge hili kwamba sasa malambo yote na mabwawa yote yanayochimbwa kwa ajili ya mifugo na kwa shughuli nyingine yatafanyiwa uchunguzi huo kuhakikisha kwamba haya yanakuwa *sustainable* au yanakuwa endelevu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika mkakati huu wa sasa wa Serikali ya Awamu ya Nne wa kuboresha mazingira nchini Tanzania tumepanga Mpango Maalum wa kuhakikisha kwamba wafugaji

wanapata maji na malisho katika sehemu zao ili kupunguza shida ya kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine katika nyakati tofauti. Chini ya Mpango wa Mazingira Serikali ina mpango wa kutenga fungu la fedha nzuri kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa, si mabwawa ambayo tutaweza kuyamaliza kwa nchi nzima kwa mwaka huu peke yake, lakini kwa kipindi cha mwaka 2006/2007 tunatarajia kutengeneza mabwawa makubwa katika sehemu nyingi hasa katika Mikoa ya Kaskazini. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Na. 96**

**Mikopo kwa Wavuvi – Mtwara**

**MHE. MOHAMED S. SINANI** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi waishio Pwani ya Bahari ya Hindi Mkoani Mtwara wanategemea uvuvi kujipatia mahitaji yao, lakini wanafanya shughuli hiyo kwa matatizo makubwa kwa kukosa nyenzo bora za uvuvi kama vile boti na nyavu za kuvulia.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mikopo ya masharti nafuu ili wajinunulie nyenzo bora za uvuvi waweze kuinua kipato chao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Sekta ya Uvuvi, imeandaa mpango wa kupiga vita umaskini miongoni mwa jamii ya wavuvi. Mpango huu uliandaliwa na kuanza kutekelezwa tangu mwaka 2000 kwa kutumia fedha za Serikali.

Wizara kwa kuzingatia umuhimu wa elimu katika mwaka 2002/2003 jumla ya wavuvi 25 kutoka Mkoa wa Mtwara walipewa mafunzo ya muda mfupi kuhusu mbinu za kupambana na umaskini. Washiriki walifundishwa masomo yafuatayo:-

- Kutambua umaskini uliopo miongoni mwao na namna ya kujikwamua kwenye umaskini huo kutokana na kutumia vyema rasilimali za uvuvi.

- Faida za kujiunga kwenye vikundi vya Ushirika na Vyama vya Kuweka na Kukopa na namna ya kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi.

- Uwezo na wajibu wa jamii waliopewa kufuatana na sheria ya uvuvi katika kulinda na kupanga matumizi ya rasilimali zilizopo kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu imetumia msaada wa fedha uliopatikana kutoka Serikali ya Ufaransa kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja

wa Mataifa na *Global Environmental Facility* kusaidia jamii ya wavuvi inayoishi ndani ya eneo la Hifadhi ya Bahari ya *Mnazi Bay.* Katika mwaka wa fedha 2005/2006 jamii hiyo imewezeshwa na kujengewa uwezo kama ifuatavyo:-

- Chini ya Programu ya kubadilishana Nyavu Haramu na Nyavu Endelevu, nyavu 721 zenye thamani ya shilingi milioni 10 zimetolewa kwa wavuvi wa vijiji 9 vilivyoko katika hifadhi.

- Katika kijiji cha Mgoji bwawa la kufugia samakki limechimbwa na kupandikizwa samaki.

- Wavuvi kutoka kijiji cha Msimbati wamepewa zana za uvuvi bora zenye thamani ya shilingi milioni 5 kwa ajili ya uvuvi wa maji ya kina kirefu.

Vikundi 5 vyenye jumla ya akina mama 40 kutoka vijiji vilivyoko ndani ya hifadhi wamepewa nyavu za kisasa zenye thamani ya shilingi milioni 21 kwa ajili ya uvuvi wa dagaa;

Aidha, Wizara yangu kwa kutambua upana na tatizo la kukosekana kwa vitendea kazi na umaskini miongoni mwa jamii ya wavuvi katika mwambao wa Bahari, kwa kushirikiana na Benki Dunia, mwaka huu wa fedha imeanza kutekeleza mradi wa kusimamia na kuendeleza Rasilimali za Bahari ujulikanao kama: "*Marine and Coastal Environmental Management Project. (MACEMP).*" Mradi huu utatekelezwa katika pande zote za Muungano kwa maana Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unakusudia kuboresha usimamizi wa rasilimali za Bahari pamoja na kuboresha maisha ya jamii ya wavuvi katika mwambao wa Pwani kama maeneo yafuatayo:-

(i) Kutoa fedha zitakazosaidia kutekeleza miradi ya wavuvi kupitia vikundi vya uzalishaji mali;
(ii) Kusaidia wavuvi kuanzisha Ushirika wa Akiba na Mikopo na uzalishaji mali;
(iii) Kutoa elimu ya ujasiliamali kwa jamii ya wavuvi;na
(iv) Kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi kwa utaratibu wa ushirikishwaji.

**MHE. MOHAMED S. SINANI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika Manispaa ya Mtwara Mikindani kuna kiwanda cha kutengenezea boti za kuvulia samaki ambacho sasa hivi kinakaribia kufa. Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua kiwanda hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kukishughulikia kiwanda hicho ama kukifufua kiwanda hicho kinachotengeneza boti.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali ina mpango mzuri kama maelezo yalivyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Jimbo la Kigamboni nalo lipo katika mwambao mwa Bahari ya Hindi na wavuvi wapo wengi. Serikali italisaidiaje Jimbo hilo kwa sababu mpaka sasa wananchi wamekuwa wakija katika Ofisi ya Mbunge kuomba misaada mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha vikundi na kupata misaada ya uvuvi. Je, maelekezo na misaada ya aina hiyo italisaidiaje Jimbo la Kigamboni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi ni kwamba katika Mradi *MACEMP* utahudumia Wilaya zote ambazo ziko kando kando ya Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, Jimbo la Kigamboni nalo litakuwa katika mpango huo. *(Makofi)*

**Na. 97**

**Vivutio vya Utalii**

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Rufiji inayo vivutio vingi kama vile Mbuga kubwa kuliko zote Afrika ya *Selous,* Chemichemi ya maji moto (*hot springs*) iliyoko Utete Rufiji ambayo maji yake ni dawa ya kutibu maradhi ya ngozi ya aina mbalimbali; na kwa kuwa, hata Wajerumani wakati wa ukoloni walikuwa wanakuja kuoga katika chemichemi hiyo ili kujitibu maradhi ya ngozi kila mwaka, na hata siku hizi maji hayo yanatibu magonjwa ya ngozi:-

(a) Je, Serikali inaufahamu ukweli huo na kama inautambua itatangaza rasmi kuwa chemchem ya maji moto ya Utete ni kivutio cha utalii?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuiendeleza chemchem hiyo na kuitangaza Tanzania nzima na nje ya nchi ili kuvutia utalii nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafahamu kuwepo kwa chemchem hiyo ya maji moto iliyoko Utete Rufiji kufuatia ziara iliyofanywa na wataalamu. Uwezekano wa maji hayo kuwa yanatibu maradhi ya ngozi unaweza kuwa upo kwa kuwa kuna madai kama hayo katika sehemu nyingine hapa nchini mfano kwenye maji moto ya Amboni, kule Tanga. Sifa hiyo ya maji kutibu maradhi ya ngozi inategemea sana kemikali zilizomo katika maji hayo. Ili kuweza kupata uhakika itabidi timu ya wataalamu wakahakiki ni kemikali zipi zipo na kuwahusisha wataalamu wa maradhi ya ngozi ili wathibitishe kama kemikali hizo zinatibu maradhi hayo ya ngozi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, kwa kuzingatia uasili wa eneo la Rufiji, Wizara yangu imeainisha Rufiji kama eneo la kuendeleza utalii wa ikolojia na inajitahidi kuvutia wawekezaji wa aina hiyo ya utalii. Kwa eneo la chemchem ya maji moto, linaweza kuendelezwa na mwananchi au kikundi cha wananchi au kampuni binafsi bila kuhitaji mtaji mkubwa. Wizara yangu imepewa dhamana ya kutangaza Tanzania kama kivutio cha utalii. Hata hivyo, maeneo haya hutangazwa yakiwa tayari kwa kukamilisha mambo yafuatayo:-

- Barabara inayofika kwenye chemichemi (Utete) inahitaji kuimarishwa ili ipitike wakati wote.

- Kuwe na uongozi wenye ubunifu kuendesha shughuli hiyo hususan "*guides*" ambao wanaweza wakatoa maelezo na historia ya chemchem hiyo.

- Vilevile pawe na malazi na umeme/aina mbadala ya nishati iwepo pia na huduma ya vyakula.

- Pawe na kibanda cha taarifa yaani *Information Centre.*

Mheshimiwa Spika, vigezo hivyo vikikamilika Wizara yangu itaitangaza chemichemi ya Utete kama moja ya kivutio cha utalii. Tunachofanya hivi sasa ni kuvutia wawekezaji katika eneo hilo. Ninachukua fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge Prof. Idris Mtulia tusaidiane katika kuhamasisha uwekezaji eneo la Rufiji kwa kuwa eneo hili lina fursa nyingi. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri yanatia moyo. Lakini inaonekana hajafika kule wala hayajui hayo maji yanatibu vipi. Hii inawezekana kabisa kuwa mfano wa Wasukuma waliokuwa wanachezea Almasi kama kete za bao mpaka akaja Williamson na akawambia jamani hii siyo kete za bao hii ni mali. Sasa inawezekana kabisa tukaacha maji yale yangefanya biashara kubwa kutoka katika nchi yetu eti kwa sababu tu wataalamu, wataalam. Mimi namkaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri aje na ninaomba anihakikishie katika Bunge hili kwamba atakuja, namhakikishia nitampa malazi na chakula? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu mwaliko wa kwenda Rufiji. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme kwamba nimekubali kufika katika chemchem hiyo ya maji moto iliyoko Utete. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kujitolea kunipa malazi pamoja na chakula. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kipindi hiki naomba nikutane na Mheshimiwa Mbunge tuweze kupanga ni lini tuongozane pamoja kwenda huko kwenye chemchem. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge baada ya majibu hayo, napenda tu kusema kwamba Mheshimiwa Spika hawezi kuruhusu Mawaziri Wanawake wawe wanafadhiliwa. Kwa sababu chini ya utaratibu wa Serikali Mawaziri wanapokwenda popote bila kujali jinsia wanalipwa posho zao. *(Kicheko)*

**Na. 98**

**Upatikanaji wa Askari katika Jeshi la Wananchi**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na kwa kuwa Maafisa wa Jeshi hilo vilevile wanatakiwa wapatikane kutoka katika pande zote mbili zinazounda Muungano lakini upande mmoja wa Muungano yaani Zanzibar inaonekana kwamba, idadi ya Askari wa vyeo vya Afisa wanaotoka Zanzibar kuingia katika Jeshi hilo ni ndogo sana ikilinganishwa na wale wanaotoka Tanzania Bara:-

(a) Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha Maafisa kutoka zaidi upande mmoja wa Muungano na upande mwingine kuwa na nafasi chache?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, ni vizuri kufanya mgawanyo maalum wa kiasilimia ili kuondoa utata unaojitokeza sasa?

(c) Je, ni kigezo gani kinachotumika katika kuwapata maafisa katika Jeshi hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu a, b, na c napenda kutoa maelezo yafuatayo:

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Wananchi wa Tanzania limeundwa kwa mujibu wa sheria ya ulinzi namba 24 ya mwaka 1966. Aidha, utendaji wa kazi zake pia umewekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni. Kwa kuzingatia sheria na kanuni hizo, hakuna mtu anayeandikishwa Jeshi kama Afisa mwenye kamisheni isipokuwa maafisa hupatikana kutokana na Askari wenyewe. Utaratibu mzima wa kuandikisha Askari wanaojiunga na Jeshi umewekwa na Serikali, nao huanzia katika Serikali za Mitaa na baadaye Wilaya. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya huwachambua waombaji wote na baadaye kuwapeleka kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kwa uchambuzi zaidi. Baada ya hapo waliochaguliwa hukabidhiwa kwa Kamati ya uandikishaji toka Makao Makuu ya Jeshi kwa kumaliza taratibu za kuandikishwa Askari.Kwa Maelezo hayo ni wazi kwamba mchakato mzima wa kumpata Askari ambaye anatarajiwa kuwa Afisa wa Jeshi unaanzia kwenye Serikali za Mitaa hadi Mkoa. Zaidi ni kwamba vijana wanaokubaliwa kujiunga na mafunzo ya uafisa ni wale ambao kwanza wametimiza masharti ya uaskari na pia kumaliza elimu ya kidato cha sita au zaidi na kufaulu kwa kiwango cha divisheni ya tatu (3) au zaidi. Baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Sababu kubwa na ya msingi inayofanya Maafisa toka zaidi upande mmoja wa Muungano ni idadi ya Askari wanaojiunga na Jeshi kwa mujibu wa sifa zao. Sehemu kama Zanzibar kutokana na udogo wake, watakaojiunga na Jeshi pia watakuwa kidogo na hatimaye Maafisa nao watakuwa kidogo. Kiuwiano (*ratio*), Bara ina watu wengi zaidi kuliko Zanzibar. Si rahisi idadi ya Maafisa Bara kuwa sawa na Zanzibar. Hata hivyo, historia inaonyesha kuwa vijana wengi wa Zanzibar waliomaliza kidato cha sita *(Form VI),* hawakuwa wakipendelea kujiunga na Jeshi. Kwa mfano, mwaka 2002 kati ya Askari 450 walioandikishwa kutoka Zanzibar ni 13 tu waliokuwa na sifa za kuwa Maafisa, mwaka 2003 kati ya Askari 345 ni 5 tu waliokuwa na sifa za kuwa Maafisa. Mwaka huu (2005/2006), Zanzibar imepewa nafasi 40 kati ya 200 ambazo wanahitajika kujiunga na mafunzo ya Uafisa. *(Makofi)*

(b)Kwa kuwa Askari ni Afisa wa Jeshi wanapomaliza mafunzo yao hutakiwa kufanya kazi katika sehemu yoyote ile ya Muungano, si busara kuanza kuweka asilimia ya Maafisa kwa pande mbili za Muungano, jambo la msingi ni kuwa vijana wenye sifa za kuwa Maafisa, toka Tanzania Visiwani kuendelea kujitokeza kwa wingi kujiunga na Jeshi ili baadaye waweze kusailiwa na kuandaliwa kwa mafunzo ya Uafisa. *(Makofi)*

(c) Maafisa wanapatikana baada ya kupitia mafunzo ya Uafisa ya mwaka mmoja. Hata hivyo, ili Askari aweze kuteuliwa kuingia katika mafunzo ya Uafisa lazima awe na sifa zifuatazo:-

(i) Nidhamu ya hali ya juu.
(ii) Uwezo wa kuongoza.

(iii) Elimu ya *Form VI* kwa kiwango cha *Division III* au kiwango cha juu zaidi.

(iv) Umri usiozidi miaka 23 kwa wale waliomaliza kidato cha sita, wataalamu wasizidi miaka 33 na madaktari umri wao usizidi miaka 35. *(Makofi)*

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a)Kwa kuwa hivi sasa Maafisa wengi wanatoka Tanzania Bara; na kwa kuwa wakati wa uandikishaji imebainika kwamba uongozi ulioko Zanzibar ambao unaongoza wanatoa jamaa zao kutoka Tanzania Bara na kuwaleta Zanzibar ili kujiunga na Jeshi hilo. Je, Serikali haioni kwamba kitendo hiki si halali na kinazorotesha Muungano? *(Makofi)*

(b)Kwa kuwa tunaelewa kwamba Tanzania Bara ni kubwa na hailingani na Tanzania Zanzibar. Je, Serikali itaisaidiaje Zanzibar kuhakikisha kwamba kuna uwiano wa uongozi ili tuweze kwenda sambamba katika Jeshi letu la Ulinzi?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, swali lake kwamba kuna watu wanatoka Bara kwenda kujiandikisha uaskari Zanzibar. Tunachofuata sisi ni Watanzania. Kwa sababu kama alivyosema yeye kwamba kuna watu wanatoka Bara kwenda Zanzibar vile vile asisahau kuwa wako wanaotoka Zanzibar kuja Bara kujiandikisha uaskari.

Mheshimiwa Spika, ningependa hii dhana ya kuigawa nchi katika Jeshi kwa misingi ya Uzanzibari na Ubara inakotupeleka si kuzuri. Hili ni Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Wananchi wa Tanzania. Sisi kama Wabunge kazi yetu ni kupalilia Utaifa wa Taifa moja la Tanzania. Hata hivi sasa ninapata tatizo kutoka kwa baadhi ya rafiki zangu wanaomba Wazanzibari ambao wako katika Jeshi warejeshwe Zanzibar wakafanye kazi Zanzibar. Hatuwezi kuendesha Jeshi kwa misingi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili la uwiano limeshajibiwa katika jibu la msingi. Ahsante. *(Makofi)*

**Na. 99**

**Tatizo la Maji – Nyuki Brigedi**

**MHE. ISSA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Nyuki Brigedi wameshirikiana kwa umoja wao kuchimba kisima ili kuondokana na tatizo sugu la Maji linalowakabili pamoja na familia zao, na wote wanaoishi kwenye kota za Jeshi; na kwa kuwa, hivi sasa wanahitaji mabomba, nyumba/kibanda, pampu ya maji na umeme ambavyo vyote vinagharimu kiasi cha

shilingi milioni ishirini na mbili laki nne na hamsini elfu (Tshs. 22,450,000/=) ili kukamilisha shughuli zote za kupata Maji safi na salama:-

(a) Je, ni lini Serikali itawakamilishia upatikanaji wa vifaa vilivyoainishwa katika swali hili ili waweze kupata Maji safi na salama?

(b) Je Serikali haioni kuwa ni hatari na sio jambo la busara sehemu muhimu kama hizo kukosa maji?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Jimbo la Mpendae, lenye sehemu (a) na (b) napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ilifanya ukarabati wa mfumo wa maji na usambazaji wake katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba. Katika kutekeleza kazi hiyo, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) lilitoa mchango mkubwa wa nguvukazi na utaalamu. Mchango wa Jeshi la Wananchi ulikuwa katika kuchimba mitaro, kufunga mabomba, ufungaji wa matanki mapya ya usambazaji maji safi pamoja na kukarabati yale ya zamani.

Mheshimiwa Spika, ni kutokana na juhudi hizo za Jeshi la Ulinzi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliamua kuwachimbia Wanajeshi kisima kimoja katika eneo la Brigedi ya Nyuki ili kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji yanayotoka kwenye mfumo wa Mamlaka ya Maji katika eneo hilo la Kambi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mbunge wa Mpendae, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli zinahitajika shilingi 22,450,000/= kwa ajili ya kukamilisha kazi ya kuongeza upatikanaji wa maji katika eneo hilo. Suala la kuwapatia vifaa kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji katika Kambi hiyo Wizara yangu inalifahamu na inalishughulikia.

(b) Kama nilivyoeleza katika maelezo yangu ya awali, hadi sasa eneo lote la Kambi ya Brigedi ya Nyuki linapata maji safi na salama kutoka katika mfumo uliopo wa maji ya bomba ya Mamlaka ya Maji. Aidha, Serikali inatambua umuhimu wa maeneo hayo na ndio maana imechukua hatua za makusudi za kuiruhusu Idara ya Maji ya Zanzibar kuwachimbia kisima Wanajeshi wetu kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji katika eneo hilo pamoja na kusaidia wakati wa dharura.

**MHE. HAFIDH ALLY TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sanaMheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Lakini wakati alipokuwa

anazungumzia makazi mazuri na hali salama ya Wanajeshi wetu katika Kambi hiyo ya Nyuki. Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka kwamba nyumba za Kambi hii ya Nyuki zilijengwa bila ya vyoo na hivi sasa Wanajeshi wanakaa mle bila ya vyoo, je Serikali iko tayari kujenga vyoo vya Kambi ile?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafuatilia Kambi zote za Jeshi la Ulinzi zilizopo nchini Tanzania na zile ambazo zina matatizo ya vyoo, zina matatizo ya maji, matatizo ya karo tunazifanyia kazi na tutaendelea kuzifanyia kazi katika bajeti ijayo? *(Makofi)*

**Na. 100**

**Uboreshaji wa *TAZARA***

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa, *TAZARA* haileti ufanisi katika utoaji wa huduma kutokana na ukosefu wa baadhi ya vipuri kama vichwavya treni, pamoja na ubovu wa reli yenyewe:-

(a) Je, Serikali za Tanzania na Zambia zina mpango gani wa kuiboresha *TAZARA?*

(b) Je, kuna mpango wowote wa kuibinafsisha *TAZARA,* na lini wamiliki wataufanikisha mpango huo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI)** alijibu:

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbnge wa Viti Maalum, naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TAZARA* ina takriban miaka 30 tokea ianze kutoa huduma mwaka 1976. Katika kipindi hicho, ufanisi wake umekuwa ukipanda na kushuka kutokana na hali halisi ya kibiashara na matukio mbalimbali. Sababu nyingine zilizochangia kushuka kwa ufanisi wa utendaji ni pamoja na:-

- Mabadiliko ya mfumo wa biashara katika ukanda wa Kusini mwa Afrika kufuatia kumalizika kwa siasa za ubaguzi za nchini Afrika Kusini.

- Kushuka kwa viwango vya biashara ya mizigo na abiria kulikochangiwa kutokana na upungufu wa vichwa, mabehewa na uharibifu wa mtandao wa mawasiliano uliosababishwa na wizi wa nyaya za simu.

- Kufunguliwa kwa njia mbadala za reli na aina nyingine za usafiri kama barabara kwa kiasi kikubwa na kumeongeza kwa ushindani wa soko la usafirishaji katika ukanda huu wa Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Zambia kupitia *TAZARA* zimekuwa zikichukua hatua za muda mfupi na wa kati, kuboresha uendeshaji wa reli hususan ununuzi wa vipuri vya injini za gari moshi, mabehewa na ukarabati wa miundo mbinu. Aidha, Serikali zimeweka bayana maamuzi ya kuingiza *TAZARA* katika mipango ya bajeti za Serikali za nchi. Katika bajeti ya mwaka 2005/2006 kwa Serikali ya Tanzania ilitenda shilingi milioni 1000.0 kwa ajili ya *TAZARA.* Fedha zimewasilishwa *TAZARA* kwa ajili ya ukarabati wa njia ya reli katika eneo la mmomonyoko wa ardhi la Kitete sehemu ya Mlimba hadi Makambako (km. 79).

Serikali ya Zambia, nayo ina mpango wa kuipatia *TAZARA* fedha kupitia bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2006. Pamoja na jitihada hizo Serikali zote mbili zimeendelea kutafuta na kupata misaada kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia mpango wa Ushirikiano wa Kiufundi (*Protocols).* Hadi sasa jumla ya (*Protocol*) Itifaki 12 zinazohusu *TAZARA* zimekwisha kamilishwa na kutekelezwa tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Reli ya *TAZARA.* Misaada inayotokana na Itifaki hizi inalenga kwenye ugavi wa vipuri vya injini, mabehewa, vifaa vya mitambo ya uokoaji, ukarabati wa miundombinu, mafunzo kwa wataalam wa reli na fedha taslimu kwa ajili ya ununuzi wa vipuri vya injini ambazo zimenunuliwa kutoka nje ya China.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali za Tanzania na Zambia zina mpango wa kubinafsisha *TAZARA* kwa kushirikisha sekta binafsi katika kuiendesha na kuiongoza *TAZARA.* Tayari nafasi imetolewa kwa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kuona uwezekano wa kushiriki katika suala hili. Na pia Kampuni ya Ushauri ya *Price Water House Coopers* iliteuliwa na Benki ya Dunia ifanye upembuzi yakinifu wa kupatikana mfumo bora wa kuishirikisha sekta binafsi katika *TAZARA.* Kampuni hiyo imekwisha kabidhi taarifa ya upembuzi huo kwa Serikali zetu mbili (Tanzania na Zambia). Taarifa hii inapitiwa kwa kushirikisha Tume zetu mbili za Ubinafsishaji.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza maswali mawili ya nyongeza kuhusiana na *TAZARA.*

Katika jibu la msingi Mheshimiwa Waziri amesema kwamba biashara imeshuka kutokana na kukuza barabara na njia nyingine upande wa Kusini mwa Afrika. Je, kutokana na uchambuzi uliofanyika kwamba hatua hizo zinadhuru reli ya *TAZARA* kati ya Tunduma na Dar es Salaam. Je, isingekuwa vizuri sisi Watanzania tuchangie mawazo kwamba tujenge reli kati ya Tunduma na Kasanga katika Ziwa Tanganyika ili kuchota bidhaa za *Congo* na ili reli hii ibaki na uhai licha ya hatua zinazochukuliwa zingine?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MAUA A. DAFTARI):** Mheshimiwa Spika, kimsingi mfumo huo anaouzungumzia Mheshimiwa Makwetta ni mzuri sana katika ku-*tap economics* za upande wa nchi za jirani. Lakini kinachogomba hivi sasa ni uwezo wetu wa Tanzania kufanya hivyo. Lakini namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba nia ipo ya kuona tunaunganisha reli zetu hizi ili zilete faida za kiuchumi kwa nchi yetu ili tupate biashara kutoka nchi za jirani kama tulivyofanya katika *corridor* ya Mtwara ambayo nia ni kujenga reli na huko kwingine tunaelekea huko huko.

**Na. 101**

**Kujenga Nyumba za Watumishi Makete**

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Makete ina miaka 27 toka ilipoanzishwa; na kwa kuwa muda mrefu sasa hakuna Shirika au Serikali iliyoweza kujenga nyumba kwa ajili ya kuishi watumishi, hali inayopelekea shida kubwa ya makazi na baadhi ya watumishi kukataa kufanya kazi Makete:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za watumishi ili kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wafanyakazi kwenda Makete?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kwa kupitia Wakala wa Majengo ni kuendelea kujenga nyumba kwa viongozi na watumishi wa ngazi za juu katika Mikoa yote na pia katika Wilaya zake kwa idadi na viwango tofauti kulingana na mahitaji.

Kulingana na majukumu ya viongozi sita walioko katika kila Wilaya, Serikali imeamua kujenga nyumba sita kila Wilaya ikiwa ni makazi rasmi ya *DC, DAS, OCD, DSO, DMO* na Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa tumeanza kujenga kwenye Wilaya mpya nne za Chato, Siha, Nanyumbu na Mkinga kwa kuzingatia kuwa hizi ni Wilaya mpya zilizokuwa na mahitaji ya haraka na ya lazima. Wilaya nyingine zitaendelea kujengwa nyumba hizo kutegemeana na pesa zitakavyokuwa zinapatikana. (*Makofi)*

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo yanaleta imani. Naomba kuuliza maswali ya nyongeza mawili kama ifuatavyo:-

Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba ili kupunguza tatizo la makazi katika Wilaya hizi mpango wa kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji ambayo yangepelekea watu binafsi kujenga nyumba za kupanga na kwamba mpango huu unakwamishwa na miundombinu ambayo haipitiki. Je, anaweza akalihakikishia Bunge hili kwamba anakubaliana na hilo? Na kama anakubaliana, ana mikakati gani ya kuona kwamba mbinu zinafanywa za kufanya zile barabara zipitike majira yote ya mwaka na hivyo kuwavutia wawekezaji kujenga nyumba kwa ajili ya kupanga watumishi?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba miundombinu au ubaya wa miundombinu unasababisha wawekezaji kushindwa kujenga au kuwekeza katika baadhi ya maeneo. Ni nia ya Serikali kwa kweli kuendelea kuboresha miundombinu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo limekuwepo ni ukosefu au uhaba wa fedha. Lakini juhudi ambazo Serikali imekuwa ikichukua katika kuboresha miundombinu ni dhahiri na nina hakika kwamba ikifika kipindi cha Bajeti mwaka huu ningeomba Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wengine waunge mkono juhudi au mikakati itakayoletwa na Wizara yangu ya Miundombinu katika kuendelea kuboresha miundombinu nchi nzima. Nina hakika Wizara hii ikishirikiana na Wizara zingine tutaweza kuboresha miundombinu na kuvutia wawekezaji katika maeneo yetu ya nchi yetu. *(Makofi)*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kumwuliza Naibu Waziri swali moja tu la nyongeza.

Sijui anatambua kwamba Kilindi pia ni miongoni mwa Wilaya mpya ambazo zimeanzishwa hivi karibuni, kwa sababu baada ya kutaja zile Wilaya nne nikashtushwa kidogo na naomba na mimi kwa niaba ya wananchi wa Kilindi na sisi tuorodheshwe katika hizo Wilaya mpya ambazo zinahitaji kupewa majengo hayo ya watumishi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ombi lake limefika. *(Makofi)*

**Na. 102**

**Kupanda Kwa Bei ya Ndizi**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya Ndizi katika masoko ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa na Bukoba imepanda kwa miaka miwili ya nyuma; na kwa kuwa, hali hiyo imechangiwa kwa kiasi kikubwa na wafanyabiashara toka Nchi jirani kununua ndizi moja kwa moja kwa wakulima:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia jambo hilo linaloendelea katika Wilaya ya Karagwe ili bei ya zao hilo katika masoko ya Mikoa iliyotajwa iwe nafuu?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwafanya wakulima wa Ndizi kunufaika na kilimo chao kama wenzetu wa Mataifa jirani?

(c) Je, ni kiasi gani cha fedha Serikali imepata kutokana na biashara hiyo ya Ndizi kwenda Nchi jirani?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza Sera na Mikakati ya kuhakikisha kuwa wakulima wanapata masoko ya uhakika kwa mazao yao. Lengo kuu ni kuona kuwa pato la wakulima linaongezeka na hivyo kuchangia katika juhudi za kupunguza umaskini vijijini.

Kuongezeka kwa bei ya ndizi katika mikoa ya Ziwa na Bukoba ni habari njema kwa wazalishaji wa ndizi katika eneo hilo. Hata hivyo, kuongezeka huko kwa bei kutaleta manufaa tu endapo wakulima wataongeza tija na kiwango cha uzalishaji wa zao hili.

Mheshimiwa Spika, bei ya ndizi katika Wilaya ya Karagwe itakuwa nafuu ikiwa uzalishaji wa zao hili utaongezeka sambamba na mahitaji. Ili kufanikisha lengo hili, Serikali itaendelea kutekeleza mikakati inayolenga kuongeza uzalishaji wa mazao ikiwa ni pamoja na zao la ndizi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kama njia mojawapo ya kuwawezesha wananchi wa mikoa hiyo.

Mikakati hiyo ya Serikali ni pamoja na kutoa mafunzo kuhusu uzalishaji kwa kuzingatia ubora wa mahitaji ya soko, kuimarisha miundombinu ya masoko, kuboresha upatikanaji wa taarifa za masoko na kuwaunganisha wazalishaji na masoko maalum.

Pamoja na hatua hizo, Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa Biashara wa zao la ndizi na nchi jirani. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa wafanyabiashara kutoka nchi jirani wananunua ndizi kutoka katika masoko na sio kununua moja kwa moja kutoka kwa wakulima.

Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe pamoja na Wilaya zingine zinazozalisha ndizi kwa wingi wanashauriwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya Biashara hiyo, pia kusimamia utaratibu huo ili wafanyabiashara waweze kwenda kununua mazao hayo katika sehemu ambazo zinakubalika na hivyo kuongeza ushindani na uwazi.

Mheshimiwa Spika, mwisho sehemu kubwa ya biashara ya zao la ndizi kati ya Tanzania na nchi jirani kwa hivi sasa si rasmi na hivyo mapato yanayotokana na biashara hiyo hayaingii kwenye kumbukumbu za mapato ya Serikali.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kuniridhisha. Lakini nina swali moja la nyongeza.

Katika Serikali ya Awamu ya Nne ina mikakati gani ili Mkoa wa Kagera wawe na soko lao maalum la kuuza ndizi ili wakulima wafaidike na kilimo chao na kwa mazao mengine?

**SPIKA:** Naona kama limekwishajibiwa. Lakini Naibu Waziri labda unapenda kutoa ufafanuzi zaidi.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika limejibiwa.

**SPIKA:** Limejibiwa. Ahsante sana. Sasa Karagwe naona?

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ninaomba nimwuliza swali lingine la nyongeza.

Kwa kuwa tunatamka kwamba zao la ndizi linatumika kutengeneza pombe ya kienyeji inayoitwa rubisi na pombe hiyo ya rubisi vile vile hutumika kutengeneza kinywaji kizuri sana kinachokubalika Karagwe pombe kali, maarufu kama *White Staff.*

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi kuwajengea kiwanda pale Karagwe au kuwatafutia mwekezaji ili hiyo pombe ya rubisi iweze kutengenezwa katika mazingira ya kisasa na viwango vinavyokubalika Kimataifa ili kuongeza kipato cha wananchi wa Karagwe?

**SPIKA:** Hii *White Staff* sio gongo hii au ni pombe gani hii? (*Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, majukumu ya Serikali ni kuandaa mazingira mazuri ya wawekezaji.

Kwa hiyo, Serikali itashirikiana pamoja na Mheshimiwa Mbunge katika kuweka mazingira mazuri. Lakini vile vile kutafuta wawekezaji ambao wanaweza kujenga viwanda hivyo vya hiyo *White Staff* ambayo unaizungumzia. *(Makofi)*

**Na. 103**

**Shirika la Haki Elimu**

**MHE. LAZARO S. NYALANDU (k.n.y. MHE. MGANA I MSINDAI)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la HAKIELIMU lililoanzishwa kwa Sheria ya Bunge lilianza kufanya kazi nzuri hapa Nchini kwa kuonyesha kukosoa, kusahihisha mema na maovu mbalimbali yanayotokea katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji kuhusu unyanyaswaji wa wanafunzi, uzembe kwa Walimu na kadhalika; na kwa kuwa Wananchi walinufaika na kufaidika na Shirika hilo na pia watenda maovu na watu wanaofanya manunuzi yasiyo halali walianza kujirudi na wengine kuchukuliwa hatua:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zilisababisha HAKIELIMU isimamishwe kutekeleza majukumu yake?

(b) Je, Serikali haioni kwamba, wakati huu wa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya inafaa kabisa HAKIELIMU kuruhusiwa kuendelea na shughuli zake?

(c) Je, Serikali haioni kwamba, haipendezi kwa chombo kilichoanzishwa kisheria kuchukuliwa hatua za kusimamishwa na mtu mmoja?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Shirika la HAKIELIMU lilifanya mazuri mengi, yaliyosaidia kubaini hila na matumizi mabaya ya fedha za MMEM kwa baadhi ya maeneo, jambo ambalo Serikali liliipokea. Serikali haikatai kukosolewa ili mradi kukosolewa kuoneshe hali halisi. Hata hivyo Serikali yeyote haiwezi kuvumilia na kukaa kimya pale ambapo uhuru wa kutoa maoni utatumika vibaya kuonesha hisia za kubeza, kudharau na kudhihaki mafanikio ya Serikali yaliyopatikana kwa kushirikiana na wananchi nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Serikali itakuwa tayari kuruhusu Shirika la HAKIELIMU kuendelea na shughuli zake iwapo tu litakuwa tayari kuacha kuendelea kubeza mafanikio ya Serikali na juhudi za wananchi za kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyoainisha kuwa Shirika la HAKIELIMU ni chombo kilichoanzishwa na Sheria ya Bunge na kinatambuliwa na Serikali, uamuzi wa kusitisha shughuli zake haukufanywa na mtu mmoja, bali ulikuwa ni uamuzi wa Serikali kwa mujibu wa sheria.

**MHE. LAZARO S. NYALANDU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza Serikali sasa itakiri mbele ya Bunge lako kwamba kama hawa HAKIELIMU wako tayari kujirekebisha watapewa nafasi ya kuendelea na kazi zao walizokuwa wanazifanya ambazo zilikuwa na maslahi kwa wananchi?

Swali langu la pili, kwa kuwa walichokuwa wana-*advocate* HAKIELIMU ukiacha mambo mengine yaliyopita walifanya wakapitiliza na mimi kuna mambo mengine nilikuwa sikubaliani nayo. Lakini walikuwa wana *advocate* suala la elimu. Kwa kuwa mpaka sasa nchi nzima tumefungua shule nyingi za sekondari za Kata, hizi Shule za Kata hazina Walimu, maji, miundombinu ni tatizo kubwa sana ambalo tunaweza tukaliita ni *crisis.*

Sasa Waziri anaweza akakiri katika Bunge hili kwamba hilo ni tatizo ambalo linatakiwa lipate kipaumbele cha kwanza cha Taifa na kwamba ni nini kitafanyika katika bajeti inayofuata kuwakomboa wanafunzi wengi wanaoteseka sasa kwa kukosa walimu nchi nzima?

**SPIKA:** Sehemu ya pili ni swali ni jipya kwa sababu linaulizia upatikanaji wa Walimu ambapo swali la msingi linahusu Taasisi ya HakiElimu. Kwa hiyo, Naibu Waziri ungejibu ile sehemu ya kwanza tu inayohusu swali la msingi..

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeshatoa maelekezo kwamba HAKIELIMU wakiri na waombe radhi ili waweze kupewa ruhusa ya kuendelea na shughuli zao. Wakiweza kutambua yale waliyoyafanya kwamba yalikuwa yanawakera Watanzania na kuandika barua kwa Waziri anayehusika wataruhusiwa na wataendelea na shughuli zao bila ya matatizo. (*Makofi)*

**SPIKA:** Naona Dr. Zainab Amir Gama, umesimama mara kadhaa hebu uliza swali lako la nyongeza.

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuuliza swali la nyongeza. Nina swali moja la tu la nyongeza.

Kwa kuwa Bunge hatujaambiwa kitu gani HAKIELIMU *specific* imekosa au walichokifanya. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, anaweza kulieleza Bunge hili lako Tukufu, anakataa kwamba hakuna rushwa au ubabaishaji katika manunuzi ya vifaa katika masuala ya shule na huduma zingine? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kuongeza kama ifuatavyo. Kwenye jibu la msingi tumekubali kwamba Serikali iko tayari kukosolewa ili mradi kinachokosolewa kitokane na hali halisi, hatukukataa kukosolewa.

Tumeeleza wazi kabisa kwamba jambo la msingi lililosababisha mpaka hatua zikachukuliwa zilizosababisha kuzuia ilikuwa ni kutokana na hisia za kubeza, kudharau mafanikio makubwa na mazuri yaliyopatikana ya Serikali kupitia nguvu za wananchi nchi nzima. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama alivyoongea Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ni kwamba anaweza kuruhusiwa ili mradi asirudie tabia ya kubeza maendeleo ya kujivunia yaliyoshirikisha wananchi nchi nzima. *(Makofi)*

**Na. 104**

**Mafanikio ya Mpango wa *MMEM***

**MHE. KHADIJA SALUM ALLY (k.n.y. MHE. FATMA ABDULHABIB FEREJI)** aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa mwaka 2002 Serikali iliandaa programu ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi *(MMEM)* kwa madhumuni ya kuboresha Elimu ya Msingi kwa watoto wote nchini. Chini ya mpango huo kwa miaka mitano (2002 - 2006) tayari mafanikiko makubwa yamekwishapatikana katika idadi ya watoto walioandikishwa kuanza masomo na kwa kuwa tupo katika awamu ya mwisho ya programu hiyo na ili kukabiliana na ongezeko la uandikishaji mashuleni.

(a) Ni madarasa mapya mangapi pamoja na vyoo ambavyo tayari yameshajengwa kati ya matarajio ya madarasa 54,000?

(b) Ni Walimu wangapi wameajiriwa kati ya matarajio ya kuajiri Walimu 46,000?

(c) Ni kiasi gani *MMEM* imefanikiwa kuinua kiwango cha ubora wa Elimu ya Msingi hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUM B. MAHIZA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdulhabib Fereji, Mbunge kupitia Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa *MMEM* jumla ya madarasa 38,144 yamejengwa kati ya madarasa 54,093 yaliyokusudiwa. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 70.5. Aidha, jumla ya vyoo 28,305 vimejengwa katika kipindi hiki cha utekelezaji wa *MMEM* mwaka 2002 hadi 2006.

(b) Mheshimiwa Spika, jumla ya Walimu 50,546 wameajiriwa ambao ni sawa na asilimia 110 ya lengo la kuajiri Walimu 45,796.

(c) Mheshimiwa Spika, mafanikio ya *MMEM* kuanzia mwaka 2002 hadi 2006 katika kuinua ubora wa elimu yanajitokeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuimarika kwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kutoka uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi 20 mwaka 2000 hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi watatu mwaka 2006.

(ii) Kuendesha mafunzo kazini kwa Walimu wa shule za msingi, elimu kwa masafa yaani *distance learning* inayotolewa kwa Walimu 5,400. Mafunzo kuhusu njia za kufundisha na kujifunza zinawashirikisha wanafunzi yaani *participatory learning* yalitolewa kwa Walimu 44,535 na kutoa msaada wa kitaalamu kwa Walimu 8,700.

(iii) Kuwapatia Walimu 50,000 wa Daraja la *B* na *C* mafunzo ya kuinua kiwango chao cha taaluma kufikia Daraja *A*.

(iv) Kuimraisha mfumo wa ukaguzi wa shule kwa kuwapatia wakaguzi mafunzo na vitendea kazi ambapo jumala ya kompyuta 80 na magari 33 yalitolewa kwa Wakaguzi wa shule wa Wilaya, hatua hizo kwa kushirikiana na wadau wa elimu zimewezesha kupanda kwa kiwango cha kufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi kutoka asilimia 22 mwaka 2000 hadi asilimia 62 mwaka 2005. *(Makofi)*

**SPIKA:** Maswali yamekwisha na hata muda wa maswali umekwisha.Ninayo matangazo. Tangazo la kwanza ningeomba kwanza kwa hali ya kipekee tumtambue Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga, ambaye amerejea kutoka Afrika Kusini yuko nyuma pale.

*(Hapa Mheshimiwa Siraji Juma Kaboyonga alisimama ili aonekane na kukaa sehemu yake Bungeni)*

**SPIKA:** waheshimiwa Wabunge, ni baada ya matibabu ya muda mrefu. Namsimamisha yeye kwa sababu wengi wanatibiwa na kurejea lakini Mheshimiwa Kaboyonga alivumishwa kule Tabora Mjini kwenye Jimbo lake kwamba amefariki dunia. Kwa hiyo, niliona ni muhimu sana wale wabaya wake waelewe kwamba Mheshimiwa Kaboyonga yupo, amerejea na ana afya njema kama mnavyomwona na anatabasamu. Aliondoka hapa akitembelea magongo amerejea katika hali nzuri. Karibu sana Mheshimiwa na pole sana. *(Makofi)*

Matanagazo mengine, taarifa ya vikao, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, inaombwa ikutane leo saa tano asubuhi chumba namba 219 ghorofa ya pili jengo la utawala. Kamati ya Ulinzi na Usalama inaarifiwa kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati leo mara baada ya kipindi cha Maswali na Majibu. Kikao kitafanyika katika ukumbi namba 37 uliopo ghorofa ya pili ndani ya ukumbi mkubwa wa Bunge. Kikao cha Kamati ya Maliasili na Mazingira ni leo saa tano asubuhi chumba namba 432 ghorofa ya nne jengo la utawala. Pia kutakuwepo na kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii saa tano asubuhi ukumbi namba 231 ghorofa ya pili *Wing C*.

Kamati ya Uwekezaji na Biashara itakutana leo saa tano asubuhi katika ukumbi namba 227.

Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote, wanaombwa kukutana ukumbi namba 231 *Wing C,* Wabunge Wanawake wote saa saba mchana mara baada ya shughuli za asubuhi.

Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Utendaji ya *Amani Forum, Tanzania* wanaomba kukutana leo saa tano asubuhi ukumbi namba 133. Pia kutakuwa na ziara ya Kamati ya Katiba na Sheria na Utawala kutembelea Ofisi ya Waziri Mkuu. Ziara hiyo inaanza mara baada ya kipindi cha Maswali na Majibu, Kamati walipanga ziara ya kutembelea Ofisi ya Waziri Mkuu nadhani ni ofisi ya hapa Dodoma.

Natangaza kwamba Kaimu Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa CCM Zanzibar kwamba kile kikao cha Waheshimiwa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar kimeahirishwa hadi hapo itakapotangazwa tena.

Tangazo lingine ni kuhusu Waheshimiwa Wabunge wa kutoka Mikoa ya Kigoma, Tabora na Majimbo mawili ya Manyoni wanaombwa wakutane pale kwenye *Board Room* ya Spika baada ya kusitisha shughuli za Bunge hapo mchana saa saba.

Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa matangazo. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ni tofauti na Kamati ya Huduma za Jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa unaombwa utaje kifungu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimwa Spika, ni kuhusu ufafanuzi samahani.

**SPIKA:** Kanuni namba ngapi? Ufafanuzi endelea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ni tofauti na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Hivyo vikao vyote viwili vinatakiwa kukutana katika tangazo lako ambalo Wenyeviti wa Kamati hizo mbili wamewasilisha katika meza yako.

**SPIKA:** Nimelikubali hilo, ahsante kwa ufafanuzi.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kushukuru kwa kupewa nafasi hii ya mwanzo kuchangia Muswada huu wa *Banking and Financial Institutions* siku ya leo Jumanne tarehe 5 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Benki Kuu kwanza kwa kupendekeza kuwepo kwa Muswada huu ambao utafuta Sheria ile iliyokuwepo sura namba 342 na kutunga Sheria hii mpya ya mwaka 2006. Kimsingi kwa maoni yangu nadhani Muswada huu ni mzuri tena unakidhi mfumo bora na salama na ambao utaendana na mahusiano ya kimataifa na hali hii tuliyokuwa nayo ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema nimefurahishwa sana na Muswada huu kuruhusu uwezekano wa kufanya kazi za kibenki na taasisi za fedha nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika nchi yetu tunaona kuna mabenki mengi sana ya nje. Kuna *Backlays Bank, Stan* **MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii, ni tofauti na Kamati ya Huduma za Jamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa unaombwa utaje kifungu.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimwa Spika, ni kuhusu ufafanuzi samahani.

**SPIKA:** Kanuni namba ngapi? Ufafanuzi endelea.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, Kamati ya Huduma za Jamii ni tofauti na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Hivyo vikao vyote viwili vinatakiwa kukutana katika tangazo lako ambalo Wenyeviti wa Kamati hizo mbili wamewasilisha katika meza yako.

**SPIKA:** Nimelikubali hilo, ahsante kwa ufafanuzi.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)***

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. HAZARA P. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kushukuru kwa kupewa nafasi hii ya mwanzo kuchangia Muswada huu wa *Banking and Financial Institutions* siku ya leo Jumanne tarehe 5 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali na Benki Kuu kwanza kwa kupendekeza kuwepo kwa Muswada huu ambao utafuta Sheria ile iliyokuwepo sura namba 342 na kutunga Sheria hii mpya ya mwaka 2006. Kimsingi kwa maoni yangu nadhani Muswada huu ni mzuri tena unakidhi mfumo bora na salama na ambao utaendana na mahusiano ya kimataifa na hali hii tuliyokuwa nayo ya utandawazi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kusema nimefurahishwa sana na Muswada huu kuruhusu uwezekano wa kufanya kazi za kibenki na taasisi za fedha nje ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika nchi yetu tunaona kuna mabenki mengi sana ya nje. Kuna *Backlays Bank, Standard Chartered,* sasa sio mbaya ifike wakati basi na sisi tunapoenda nje, nchi nyingine kama Uingereza, Afrika Kusini basi tuzikute benki zetu za *CRDB, NBC* na taasisi nyingine za fedha. Vile vile ni imani yangu kwamba mabenki yameelewa na nichukue nafasi kuipongeza Benki ya *CRDB* ambayo sasa hivi kwa kweli imeanza kutoa huduma ya Kadi ya *Visa* ambapo inatoa uwezekano wa mtu kuchukua hela hata unapokuwa nje ya nchi. Hili na nadhani benki hii kwa kweli ilikuwa inasubiri Muswada huu uwepo ili waweze kufungua *branch* nyingine huko nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa leseni kifungu namba 10 sehemu ya kwanza inasema kwamba; "Benki itakuwa na uwezo wa kutoa leseni katika kipindi cha siku 90. Hili jambo ni jema sana kwa hiyo, hapo naomba nitoe msisitizo kwamba tunaposema siku 90 benki itakuwa na uwezo wa kutoa leseni au kutoa maamuzi ya kukataa maamuzi ya kutoa leseni, jambo hilo lizingatiwe sana. Sasa isiwe siku 90 halafu watu wanapokuja kutaka huduma hiyo wanaambiwa njoo kesho.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba ya Mheshimiwa Rais akiwa Mkoani Kilimanjaro ametuambia kwamba tujitahidi tunapomwambia mtu njoo baada ya wiki mbili, akija baada ya hizo wiki usimwambie aje tena baada ya nusu saa. Kwa hiyo, ninaafiki, lakini ninaomba sana iwepo haja ya kuzingatia kipindi hicho cha siku 90.

Kwa hiyo, ipo haja ya benki kuweka nguvukazi ya kutosha ili waweze kupitia nyaraka ambazo zinatakiwa ili ndani ya siku 90 tuweze kuwapa moyo wawekezaji katika sekta hii katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika Muswada huu baadhi ya vipengele vimetumia maneno ambayo ni yakiujumla sana. Kwa mfano, kipengele cha 8 (e), kinasema nyaraka zingine. Pale wamesema *other document.* Sasa tunaposema nyaraka zingine mimi kwa maoni yangu Benki imefanya kazi muda mrefu sana na imekuwa ikitoa huduma hii muda mrefu. Bila shaka hizi nyaraka nyingine benki inazijua. Isingekuwa vibaya hizo nyaraka nyingine zikatamkwa.

Vile vile ukienda kifungu namba 9 sehemu 2(c) inasema na mambo mengine kadri Benki itakavyoona inafaa. Kwa hiyo, iko lugha ambayo imetumika ambayo ni ya jumla jumla sana. Inasema: *"Such other matters as the bank may deemed necessary."* Sasa haya mambo mengine, nyaraka zingine ni mambo gani? Ikiwa kama Muswada wa Sheria ambayo tunakwenda kuipitisha ni vizuri haya mambo ungepatikana utafiti waweze kuyatamka bayana.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana pia na suala la kusimamisha na kufutwa kwa leseni kipengele cha 11. Zipo sababu nzuri sana ambazo zimewekwa katika Muswada ambapo zitapelekea leseni kufutwa au kusimamishwa na mimi kimsingi ninaziafiki. Lakini nitumie nafasi hii kuomba basi Benki Kuu ichukue nafasi pamoja na haki na mamlaka hayo watakayokuwa nayo ya kufuta na kusimamisha lesini kabla ya kufuta au kusimamisha kuwepo na hatua ya kuielekeza benki kwamba msipofanya jambo moja, la pili na la tatu mtapelekea kufutwa au kusimamishwa kwa leseni. Isiwe moja kwa moja wamekiuka kipengele tunafuta, Benki ifanje kazi ya ku-*promote rather than* ku-*control.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilidhani hayo ni mambo ya msingi kwanza watoe labda kusudio la kufutwa kwa leseni au nia na labda wanatoa siku kadhaa kwamba msipojirekebisha, mtapelekea leseni zenu kufutwa au kusimamishwa. Nadhani itakuwa ni jambo jema kwa sababu tupo kwenye ushindani mkali sana wa mahusiano ya Kitaifa na Kimataifa, sasa watu wetu katika sekta hii ya masuala ya fedha ndiyo kwanza wameanza. Sasa ipo haja ya kuwapa nafasi ya kujifunza na kuelekezwa pole pole itafika wakati mambo haya tukishakuwa tumeyafahamu vizuri basi benki inaweza kusema sasa moja kwa moja tunafuta au kusimamishwa. Kwa hiyo, nashauri kuwepo na hatua ambazo zinapelekea katika kufutwa au kusimamishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nimefurahishwa sana na Muswada huu kubadili viwango vya mtaji. Viwango vya mtaji wa kuanzisha maswala ya Benki na taasisi za kifedha mmetoka kuanzia bilioni moja kwenda bilioni tano. Hiyo ninaafiki lakini nimependezwa sana na suala zima ambapo wamesema kwamba Benki itakuwa na uwezo wa kutafakari na kutathmini eneo ambalo benki hiyo au taasisi hiyo itahitaji kuanzishwa. Kwa hiyo, upo uwezekano kwa kweli wa kuzingatia mtaji wa chini ya kiwango cha hiyo bilioni tano.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu watu wetu ambao sasa hivi wapo vijijini na katika ngazi ya kata bado mtaji huu ni mkubwa, wanaweza wakaanzisha huduma hii kwa mtaji mdogo na ukafanya kazi inayopaswa bila matatizo hasa watu wangu wa kule Makete na Ludewa kwa kweli jambo hili inabidi lizingatiwe sana ili kiwango hiki kiweze kutafakaliwa.

Lakini si hilo tu kwamba hicho kiwango kitaweza kuangaliwa pia kama kuna uwezekano wa Benki Kuu kutoa *privilege* ya kuweza kuhusisha benki hizo zikaanzishwa katika maeneo ambayo yapo mbali na *centers,* kwa sababu huduma hizi nyingi ziko katika Makao Mkuu ya Wilaya au Makao Makuu ya Mkoa, maeneo ya pembezoni bado tunahitaji kuwezesha huduma hii kuwepo.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchangia juu ya baadhi ya maneno mazuri ambayo yametumika, yako maneno mazuri sana yametumika ya kitaalamu ninaafiki lakini nilidhani basi ifike wakati yatumike maneno kuwepo na tafsiri ili hata yule mtu wa kawaida anapousoma Muswada huu au Sheria hii apate kuelewa. Inafika wakati ili mtu aelewe lazima awe amefanya kazi za huduma hizi za fedha au za kibenki kwa sababu maneno yametumika ya kitaalam sana na pengine yanakuwa hayaonekani katika kipengele cha tafsiri ambayo mara nyingi huonekana mwanzo wa Sheria.

Sasa ni vizuri maneno hayo yakaangaliwa, siwezi kuyataja yote ili Muswada huu ueleweke na wale ndugu zangu wa Ludewa na Makete waweze kuelewa nini maana ya maneno haya. Kwa mfano wa haraka haraka watu wenye uhusiano wa karibu na benki husika hasa hawa watu wenye uhusiano wa karibu *connected landing* ni watu gani, kwa kweli mtu wa kawaida kule Makete, Ludewa, Njombe watu wenye uhusiano wa karibu sio rahisi kueleweka na vile vile kuna maneno kama *abandoned property* mali iliyotelekezwa. Vitu kama hivyo ni ningeomba viangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kingine ni kuhusu uanzishwaji wa mfuko wa bima ya amana, pale kuna vigezo vizuri sana ambavyo kimsingi naviafiki ambavyo vinahitaji wajumbe wale ambao watakuwa kwenye mfuko wa bima na amana wawe navyo na vile vile kipengele Na. 37 sehemu ya tano viko vipengele ambavyo vinakataa ni watu gani ambao hawawezi kuwa katika huo mfuko wa bima na amana. Lakini nilipokuwa nazidi kutafakari wale watu ambao wanakataliwa kuwa ni pamoja na Wakurugenzi wa Bunge au watu ambao wanafanya kazi za kisiasa. Sasa nikasema tukishawatoa watu hawa na katika watu ambao wanahitajika kuwa wajumbe katika mfuko huo ni watu wenye uzoefu, ni watu wenye uzoefu na masuala haya, sasa watu wenye uzoefu lazima atakuwa au ni Mbunge au ni Mkurugenzi au ni mwanasiasa au ni mtu ambaye ana shares, na imesema mtu mwenye shares asiwe mjumbe.

Sasa hapa kwa kweli nadhani kidogo lingeangaliwa vizuri kwa sababu naona huku inatoa kibali wanasema lazima awe na *experience.* Sasa ili mtu awe na *experience* ni kweli kwamba atadondokea katika makundi hayo. Lakini kwa kuwa wamesema pia kuna wajumbe ambao watachaguliwa na Mheshimiwa Waziri kutokana na sifa hizo hapo sitataja suala la jinsia kwa sababu ni imani yangu kwamba sifa hizo zinawadondokea akinamama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni suala la kipengele Na.43, kipengele hicho kimezungumzia kuhusu *default fine* kwamba kutakuwa na *default fine* lakini hiyo *default fine* haijafafanuliwa ni kiasi gani na itakuwaje na vifungu vingine *fine* zake zimeelezwa moja kwa moja.

Sasa kwa mtu wa kawaida ambaye hajasomea au sio mtaalam wa masuala ya sheria kama madaktari na ma-*engineer* inakuwa ngumu kuelewa hiyo *default fine* ni kiasi gani lazima arejee kwenye sheria nyingine au kifungu kingine au kwenye tafsiri ili apate kujua nilidhani ipo haja ya hiyo *default fine,* kifungu Na. 43 itaelezwa pale pale sambamba na hiyo sehemu.

Mheshimiwa Spika, mara nyingine nashukuru kwa kunipa nafasi na bila kuathiri vifungu vilivyokuwepo ninaomba kuunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu nami nichangie hoja iliyo mbele yetu, nakushuru sana, namshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutupa uhai mpaka leo tunaendelea kuzungumza na tuko pamoja. Naanza kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kazi nzuri anayoifanya

pamoja na Waziri Mkuu. Nilikuwa sijasema neno la kupongeza, nilikuwa naangalia kwanza maana wengine huwa wanaharakisha harakisha lakini naangalia ni kitu gani kinaendelea.

Mheshimiwa Spiak, kwa kweli kazi wanayoifanya ni nzuri sana na wameingia kipindi ambacho wamekumbana na matatizo makubwa lakini wameyakabili vilivyo, nawapongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Waziri Mkuu, Makamu na uongozi mzima pamoja na Mawaziri na nimpongeze vile vile Mheshimiwa Waziri kuleta hizi kwanza hoja ya kwanza ilikuwa ni ile ngumu kabisa Benki Kuu kwa kweli ilikuwa ni ngumu na ilitutia utata kidogo lakini ameikabili, imeenda vizuri na hii ameileta hii. Pamoja na pongezi hizo mimi bado na utata kidogo na matatizo kidogo sina wasiwasi upande wa Mawaziri na viongozi katika ngazi hiyo, nadhani wasiwasi wangu umeondoka kwa sababu walikwenda wakaa jando, wakafanyiana mambo ya unyago kule Arusha wakapatana wakaenda pamoja.

Sasa wasiwasi wangu hapa katikati hapa na sijui kama baadhi ya watendaji wanawaelewa, napenda niende hivyo katika suala hili lililo mbele yetu baadaye tulifikia tu. Kwa sababu kuna mambo ambayo nikiyaona utekelezaji wake, wenzetu ile kasi mpya ari na nguvu mpya baadhi ya watendaji hawaelewi, nimeangalia katika tatizo la masuala ya njaa, maagizo mazuri yalitoka sana Serikalini wakatoa maelekezo baada ya tatizo la njaa kwamba leteni takwimu sahihi na kila kitu kifanyiwe kazi na Serikali, Rais alieleza, Waziri Mkuu alieleza lakini matokeo yaliyotokea wengine baadaye wakachukulia nafasi hiyo kwamba sasa tujinufaishe, hata juzi wakati Rais anahutubia watu walikuwa wanazungumza pale. Wengine katikati hawakuweza kuleta hata taarifa sahihi.

Mfano mzuri ni mfano wa Wilaya ya Geita, Wilaya ya Geita ilikuwa na mtatizo sana ya njaa, lakini kwenye taarifa tulizopewa ni kwamba Geita haikuwemo, lakini tulipofuatilia Waziri aliagiza, tukafuatilia takwimu Wilayani zilikwenda, Mkoani sijui hazikuchujwa. Sasa unakuta hawa watu inaonekana *they are not serious* zinakwenda hivi hivi mpaka Mkuu wetu wa Mkoa ameingilia kati pamoja na upya wake alikuja angalau ana hali nzuri ya afya lakini ameanza kuona, kwa sababu ya matatizo ya chakula Geita, wengine wamekula, wengine wamefukuzwa. Sasa unaona watu wanafukuzwa kila leo, kwa sababu watu hawajaelewa.

Mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu inabidi hawa watu nao muwaweke jando, vinginevyo mtafukuza wote, kwa mfano juzi kuna tukio ambalo Mheshimiwa Rais amezungumza litatangazwa, uamuzi mgumu. Makamu wa Rais ametangaza vizuri sana na kwa nia njema, inataka kubadilishwa kuwa nia mbaya kwa sababu ya watendaji ambao hawaelewi, ameeleza wafugaji na baadhi ya wakulima wahame maeneo ambayo yanatuletea tatizo na kasema vizuri kabisa mpaka mwezi wa sita watu watoke. Wapeni muda waondoke, lakini mwezi wa sita kila mtu asionekane, sisi wote tukashangilia, lakini utekelezaji wake sasa unatutisha, unakuta sasa watu wanakuja kulalamika Bungeni, kwa sababu watendaji sijui mimi sielewe sijui wanamwelewa Kikwete sijui hawamwelewi, sijui hawaelewi maelekezo sijui wanaogopa, wanakurupuka.

Sasa hivi ng'ombe wanakusanywa Karagwe wamewekwa sijui mia tano, wameshaweka na kiwango cha faini. Nani amewatuma watu sasa hivi wanahangaika, wanakusanya Wajaluo, Wasukuma wamesema watu wa nje waende, warudi kwao mwezi wa sita wawe wamerudisha mifugo yao. Sasa badala ya kutekelezwa sasa wanawakusanya, wanawapiga faini wanafanya nini, wanaanza kutuletea uhasama ambao sio wa lazima, *after all* hiyo mipaka yenyewe imeletwa na wazungu.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri ililetwa na wazungu, mtu ambaye zoezi zuri wanaanza kuliharibu watendaji. Mtu ambaye kwa mfano Blandes akienda Uganda anakuwa Mnyankole ni wale wale. Lakini zoezi zuri analiharibu kwa nini hali hii? Mimi nafikiri tujaribu kusikiliza sana maelekezo. *(Makofi)*

Sasa nakuja kwa hawa watu wa Benki. Ndugu zangu wa Benki sijui mnaifahamu ari mpya na nguvu mpya? Mnajielekezaje au mnaenda kinyumenyume, mnajielekezaje kule kwa wananchi kwa mkulima? Nimekuwa nasoma, sawa mmeweka Sheria zenu zinavyoenda na nini, lakini kuangalia sasa mikakati yenu kuhusu kusaidia huyu mkulima huyu mwananchi aweze hata kuweka programu za kuleta vijembe au za matrekta ya kuweza kuwasaidia. Tusikae na lile neno la *high risk,* nilisema hata *last time* kwamba neno hilo la *high lisk* halitakwisha kama hatutamsaidia mkulima kwa sababu ana uwezo, ana ardhi, mvua inaweza ikanyesha, akafanya vitu vizuri kama atapewa vifaa badala ya kufikilia fedha.

Vile vile kwa upande wa wachimbaji, najua wachimbaji hiyo ndiyo sijui ni *the highest risk,* wataalam wanasema kwa sababu wakiwakopesha hawana kitu. Lakini fanyeni *study* mna maeneo ya *study* ya kuweza kuchunguza kule kwa wachimbaji kwa mfano wachimbaji wa Rwamgasi ukienda, Wanyarugusu, wako *well organised* na hawatarajii kuondoka pale. Wanyakagwe, wapo pale wako *well organised* hata mitambo yao ni ya gharama. Lakini ukiangalia kwamba hawa tunaweza kuwasaidia, kwa sababu ukiwasaidia hao wanaweza kuajiri watu zaidi ya 1000 wakafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ninawaomba ndugu zangu watu wa Benki mimi ninawaomba sana, pamoja na Miswada hii hebu ajaribu Mheshimiwa Waziri kuangalia hawa tuwasaidieje wakulima wetu. Vinginevyo watakuwa wanalima kwa mkono kwa mkono.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwenda vijijini. Benki zisiangalie faida tu. Jaribuni kuinua miji mingine inayoendelea. Kwa mfano pale Chalinze panapendeza pale pana Benki. Lakini kuna mji kama Katoro, mji wa Katoro ni mkubwa kuliko wa Bukombe, ni mkubwa kuliko wa Bihalamuro, ni mkubwa kuliko Chato, ni mkubwa sana kuliko Chalinze. Nadhani hata Sengerema unaizidi. Hawana Benki, sasa watu kama wale fanyeni *study* hapo pana biashara kubwa sana pale kwa sababu watu wa Chato wanakuja kununua pale, Waganda wanakuja pale, Waburundi wanakuja pale, wa Bukombe wanakuja pale. Sasa ku-*stimulate* biashara ya pale, pelekeni Benki pale hata *NMB* au *CRDB*. Mimi naomba, suala langu ni la maombi tujaribu kuangalia hii ari mpya, kasi mpya, ninyi mnaielekeza wapi? Tuwasadie ndugu zetu hawa viongozi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, tumeshachangia sana suala hili. Naomba niwaombe sana hawa ndugu zetu. La mwisho, elimu ya masuala ya Benki iende kwa wananchi. Wengine ambao hata wana uwezo wa kukopa, hawaelewi. Nilikuwa naomba wapewe elimu ya kutosha ili waweze kuvutia kukopa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, namwita Mheshimiwa Martha Mosses Mlata, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Meryce Emmanuel, ambaye simwoni humu ndani ya ukumbi, lakini baada ya Mheshimiwa Meryce Emmanuel, kama atakuwepo atafuatia Mheshimiwa William Ngeleja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Muswada huu. Napenda kwanza kabisa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wote wa Benki Kuu kwa jinsi ambavyo tumeweza kufikia hapa tulipo kwenye huu Muswada. Naamini huko tunakoelekea mambo yatakuwa mazuri zaidi. Wengi wameshachangia, mambo mengi sana yamezungumzwa kwa ajili tu ya kuweza kuinua uchumi wa nchi yetu. Mambo yote yamezungumzwa kuielekeza Benki Kuu maana yenyewe ndiyo kiranja hasa wa kuweza kusaidia hata Benki zingine kwa ajili ya kuinua uchumi wa nchi yetu pamoja na kupunguza umaskini wa wananchi wote hasa walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, wengi wamezungumza kuhusu sekta ya kilimo kwamba ni namna gani benki ziweze kusaidia kwenye upande wa sekta ya kilimo. Mimi pia naunga mkono, lakini sekta hii ya kilimo naomba iende sambamba na viwanda vyetu kwa sababu utakapokuwa umemwezesha mkulima akapata vitendea kazi, akapanua mashamba yake, akalima vizuri sana na Mungu akamsaidia mvua ikanyesha vizuri au mabwawa kwa ajili ya kilimo cha kumwagilia, lakini bado tujue kabisa kwamba mkulima huyu siyo kwamba anahitaji tu chakula cha kujikimu yeye mwenyewe, sisi tunachotaka aweze kutoka pale alipo ni lazima aweze kuuza mazao yake, mazao haya ni lazima kuwe na soko la kutosha. Sasa soko la kutosha lazima kuwe na viwanda. Hivi viwanda aidha, viwe vikubwa au vidogo, lakini mimi nafikiri kwamba mabenki yetu yaweze kusaidia sana katika viwanda. Nasisitiza hili ili wakulima wetu wanapolima mazao yale ya biashara kama alizeti, pamba na karanga waweze kupata mahali pa kuuza.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mimi natoka mkoa wa Singida, zao la alizeti linalimwa sana. Lakini zao hili watu wanakuwa hawavutiwi nalo kwa sababu soko lake ni dogo sana, unaweza ukalima sana, lakini ukakosa mahali pa kuuza kwa sababu hakuna viwanda.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Benki ziweze kusaidia viwanda vya wale watu wadogo wadogo tuna viwanda kwa mfano kule Shelui vina uwezo wa kufanya kazi kubwa sana, lakini yule mwenye kiwanda hana uwezo wa kuweza kununua yale mazao kutoka kwa wakulima kutokana na mtaji wake mdogo. Basi watu hawa wawezeshwe ili waweze kununua yale mazao kutoka kwa wakulima ili wananchi wetu waweze

kuondokana na ule umaskini walionao, maana kuwawezesha tu katika kilimo bila kuwapatia masoko tunakuwa bado hatujawasaidia. Kwa hiyo, naomba benki iangalie Mheshimiwa Waziri utilie mkazo sana katika suala hili, kilimo iendane pamoja na viwanda ambavyo vitawasaidia wakulima kuuza mazao yao hasa yale ya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia mimi napenda kuzungumzia hasa kuhusu ajira ya vijana, naamini kabisa benki zinaweza zikatusaidia sana katika sekta hii hasa katika kuanzishwa Benki ya Vijana. Naomba sana Benki Kuu, chonde chonde, Benki ya Vijana itakapokuja kuomba, tunaomba sana muiangalie Benki hii. Hakika inaweza ikatusaidia sana katika kumuendeleza huyu kijana. Vijana ndiyo wimbi kubwa sana ambalo lipo, wanaomaliza elimu ya sekondari, msingi, vyuo na kadhalika, lakini bado unakuta ajira za Serikalini ni ndogo. Sasa vijana hawa wengi wao wanahitaji kujiajiri wenyewe, lakini bila kuwa na mitaji hawawezi kufanya kitu chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kila kijana ana kipaji chake, vijana wengine wanapenda kufanyabiashara, vijana wengine watataka kulima, vijana wengine ni wanamichezo na vijana wengine ni wasanii. Sasa utakuta kijana huyu labda nimzungumzie msanii, kwa sababu na mimi ni msanii. Sijawahi kuona kama kuna msanii yeyote ameenda benki kwenda kuomba ili akopeshwe kwa ajili ya kuendeleza sanaa yake akapatiwa mtaji. Lakini muziki huu na sanaa hii tunaihitaji na wengi wao tunaitumia. Hata ukiingia benki unakuta muziki unaendelea, hujui kijana huyu alihangaika vipi, kwani shida wanazozipata ni kubwa sana. Lakini wanahitaji kuwezeshwa sana ili na wao waingine katika mtandao wa wanamuziki ambao wana maisha mazuri, tutaondokana na tatizo hili la ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, ukienda vijijini kuna vijana ambao tunawarudisha, kuja mjini tunawarudisha. Wanataka kuja kucheza kwenye viwanja vizuri, ni wachezaji, anaona labda na mimi nitaonekana kule niingie kwenye timu, labda timu fulani. Lakini sasa kule kule vijijini wengine wanatamani michezo, kumbe angewezeshwa akalima bado angeendelea kucheza michezo ile ile kule anayotaka kama ni mpira.

Sasa unakuta ukienda wanakwambia Mheshimiwa Mbunge tunaomba utuletee hata mpira mmoja tu, mwingine wa mazoezi tutatengeneza wa vitambaa. Kwa hiyo, suala hili linawavutia wengi sana kutaka kuja mjini kwa kuona kwamba wao wamesahaulika kule vijijini. Basi naomba benki hii ili itakapokuja kuletwa mbele yenu, muiangalie kwa macho mawili. Mtusaidie ili tuweze kuwasaidia wale vijana walioko vijijini na walioko mijini wenye vipaji mbalimbali waweze kuondokana na tatizo la ajira, wakae watulie na nchi yetu itakuwa na amani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ninalotaka kuzungumzia ni kuhusu Benki ya Wanawake. Sina hakika sana kama benki hii ni kweli inatiliwa mkazo kwa sababu hizi asasi zingine mwanamke anapokwenda ni kweli anapewa mkopo, lakini riba inakuwa ni kubwa sana na masharti yake yanakuwa ni ya ajabu ajabu. Wengi wao unakuta anakata tamaa na anaogopa, anashindwa hata kuchukua mkopo. Lakini kama kutaanzishwa Benki ya Wanawake ambayo Benki Kuu mtatusaidia kuisimamia benki hii, unajua ni wazi

kabisa utakapomwendeleza mwanamke hakika umeendeleza Taifa zima. Tunaomba sana. Benki hii itatusaidia sisi hata katika kufanya shughuli zetu kwa sababu wanawake walio wengi wana vipaji mbalimbali. Wengine ni wafinyanzi, wengine ni wasusi na wengine ni wafanyabiashara, lakini wanahitaji mitaji kuweza kuondokana na tatizo la ukiritimba wa kukosa mitaji na kubakia tu kuwa tegemezi kwa wanaume.

Kwa hiyo, naomba sana Benki Kuu mtusaidie katika benki hizi mbili ili vijana pamoja na wanawake waweze kuondokana na tatizo la umaskini uliokithiri ndani ya maisha yao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuzungumzia, sielewi Benki Kuu au benki za kawaida wanashiriki vipi katika masuala ya elimu. Elimu ndiyo msingi wa maisha, elimu itatusaidia na kutufikisha mbali sana, sasa hivi tunasema kwamba kila Mtanzania apate elimu. Angalau hata nusu yao au robo tatu wamesoma elimu ya Chuo Kikuu. Kuna wale ambao wanaingia mkataba na Serikali moja kwa moja, lakini kuna wengi wao wanakuwa wamefaulu, bado wao wanataka kuendelea kwa kujilipia wao wenyewe. Tunamshukuru Mungu kwa sababu bodi ya mikopo iliyoanzishwa, lakini bodi hii ni dhahiri kabisa haina pesa za kutosha za kuweza kukidhi mahitaji ya Watanzania walio wengi wanaohitaji kupata elimu ya Chuo Kikuu.

Mheshimiwa Spika, sasa sielewi Benki Kuu kama wana utaratibu wowote kuhusu haya mabenki kuweza kutia mkono wake na kusaidia bodi hizi au asasi ambazo zinataka kukopesha kwa ajili ya masuala ya elimu.

Mimi ushauri wangu nilikuwa naomba kwa sababu pamoja na kwamba kuna taratibu ambazo zinakuwa zimewekwa, lakini pia taratibu hizi ziliwekwa na sisi tunaweza tukaweka kwamba benki ziingie, ziweze kusaidia bodi hizi ambazo zinatoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi wanaotaka kwenda vyuo vikuu ili bodi hii iweze kukidhi mahitaji na matakwa ya wale watu wanaotaka kwenda kusoma ili lengo, maana sera ya Chama cha Mapinduzi ni kumuelimisha mwananchi katika elimu ya juu.

Kwa hiyo, naomba sana Benki Kuu mtusaidie kuingiza mkono wenu katika bodi hii ya mikopo kwa wanafunzi angalau tutakuwa tumepiga hatua.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsanteni. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Simuoni Mheshimiwa Meryce Emmanuel, hapa. Kwa hiyo, itabidi nimwite Mheshimiwa Vita Kawawa ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, ajiandae Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, ambaye naye hayupo humu ndani, lakini tutaona.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika Muswada huu wa *Banking and Financial Institutions.*

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kabisa kuungana na wenzangu kwa kumpongeza kwanza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa

Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri na Manaibu Waziri kwa kutimiza siku 100 za uongozi wa awamu ya nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu katika mbio za kupokezana vijitu ukianza vizuri ndiyo ushindi unapatikana. Hivyo, Serikali ya Awamu ya Nne imetuonyesha kasi waliyoanza nayo na wanaendelea na ari na nguvu ile ile na matumaini yetu tutashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nataka tu kuwatahadharisha wale wanaodhania kwamba nguvu hizi za Serikali yetu ya Awamu ya Nne ni nguvu za soda, wamenoa. Viongozi wetu hawa ari yao, nguvu yao na kasi yao ni kama moto ule unaowaka katika visima vya kusafisha mafuta, hauzimiki. Ukitaka kuuzima kwa maji ndiyo kwanza unazidi kulipuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha hususan Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakia Hamdan Meghji, Manaibu wake wote wawili, Katibu Mkuu na timu yake yote ya maafisa waandamizi kwa kuandaa Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumpongeza Gavana Daudi Balali na timu yake kwa kuandaa na kwa kusikiliza ushauri mbalimbali wa Wabunge katika Muswada uliopita na kurekebisha yale ambayo waliona yanafaa. Mimi naomba kuunga mkono hoja ya Muswada huu, pia naunga mkono hoja nzuri zilizotangulia za Wajumbe wenzangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia usalama wa fedha za wateja wa benki. Kwa kuwa teknolojia imekua na uhalifu nao umeongezeka , mimi sina tatizo na kazi ya *daily monitoring of banking business* inayofanywa na Benki Kuu, ni nzuri na ndiyo maana imetusaidia uchumi wetu kukua kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita. Tatizo langu lipo kwenye uimarishaji wa usalama wa fedha zilizopo kwenye mabenki. Wananchi wengi, wawekezaji pia wafanyabiashara kisheria na kiutamaduni wa fedha wanaamini benki ni mahali salama pa kuweka fedha zao. Lakini sasa hivi ujambazi wa kupora benki ulitugubika kwenye benki zetu na mpaka Serikali yetu ikachukua maamuzi ya makusudi kabisa ya kuweka ulinzi wa polisi. Lakini benki hizi zinazo nafasi ya kulisaidia Jeshi letu la Polisi kuweka ulinzi wa mitambo, siyo ulinzi wa virungu.

Katika Ibara ya 5 *chapter* ya pili kipengele hiki kimewekwa kiujumla jumla, hakija-*specify* usalama au ulinzi wa fedha hizi za wananchi wanaoweka fedha zao benki utakuwaje.Hivyo nashauri, kipengele hiki kama kingeongezwa, kipengele kinacho-*specify* sheria ya ulinzi wa fedha ambayo italazimisha benki hizo za biashara kuweka *security components* katika benki zao na *branches* zao zote kama vile *detectors* za kutambua silaha za moto au mtu yeyote asiweze kuingia na silaha yoyote hatari ndani ya benki. Kuwekwa *CCTV* ili kusaidia kuzuia au kurahisha vyombo vyetu vyenye dhamana ya ulinzi na usalama kufanya uchunguzi wake wakati tukio likiwa limetokea.

Mheshimiwa Spika, ulinzi ni mpana sana na benki hazina budi kulisaidia Jeshi letu la Polisi kwani benki ni *part and parcel* ya ulinzi wa fedha za wananchi na wawekezaji wetu na Polisi haiwezi kuweka mitambo hiyo ndani ya benki hizo, lakini ili

kuimarisha ulinzi huo, lazima benki zishirikiane kwa njia hiyo. Kwa hiyo, hivyo naomba Muswada huu ukiweke kipengele hicho kitakacholazimisha benki hizi kuweka *security components* ambazo zitasaidia kuzuia na kuchunguza kirahisi matukio ya uhalifu yakiwa yametokea.

Mheshimiwa Spika, mimi sina zaidi ya kuongeza. Mchango wangu ulikuwa ni huo wa usalama. Naomba kama utazingatiwa nitashukuru na ninaomba kuunga hoja mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Bahati njema Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, yupo. Kwa hiyo, nitamwita sasa. Samahani Mheshimiwa William Ngeleja, basi utafuatia.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa mara yangu ya kwanza kusimamia kwenye Bunge hili na mimi nisingependa kuacha kuwapongeza viongozi wetu, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi na wananchi wa Tanzania. Vile vile nampongeza na Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wetu pia nichukue nafasi kukupongeza wewe Spika, kwa kuchaguliwa na Bunge lako Tukufu kuwa Spika wa Bunge. Bila kusahau kabisa nimpongeze mama yetu, Mheshimiwa Anne Makinda, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge letu, kwa kweli hii imetupandisha sana wanawake tunajisikia vizuri sana tunapomwona mama yetu akiwa huko mbele.

Vile vile napenda kuwapongeza Wabunge wote waliojaliwa na Mwenyezi Mungu kuingia katika Bunge hili kwa awamu hii ya nne bila kuwasahau Mawaziri waliochaguliwa na Rais kuwa Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini vile vile ninayo sababu kubwa ya kuwapongeza wa Wilaya ya Maswa, wanachama wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kwa kuniwezesha mimi leo hii kuwa katika Bunge hili Tukufu, maana yake bila wao yamkini hata nisingekuwa hapa kwa hiyo, nawapongezeni sana wana Maswa pale mlipo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia napenda kusema kwamba wenzangu wameshachangia kwa urefu sana hoja hii, lakini nafikiri kwamba si vibaya kama nitasema neno moja ambalo naweza kuliwekea msisitizo ambalo nimeliona ni la muhimu sana pia katika hoja hii. Ningependa kusema kuhusu suala la riba, nasema hili suala kwa sababu pale nilipo kwa uzoefu niliouchukua pale Wilayani na bahati nzuri kipindi kilichopita nilikuwa diwani pale kwa ile miaka mitano iliyopita.

Kwa hiyo, nimeliona jambo hili *especially* kwa wafanyakazi, wafanyakazi wamechukua mikopo ya benki lakini kutokana na ile riba inakuwa ni kubwa sasa wanajikuta kwamba yaani hakuna chochote wanachokipata katika mikopo hiyo wanayokuwa wanakopa.

Sasa mimi ningependa kusema kwamba kwa kweli wanakopesha ni vizuri na wanawasaidia sana wafanyakazi pamoja na wananchi wetu, lakini ningependa kusema kwamba wajaribu kuangalia tena kwa upya suala la riba hii. Hii riba mimi naiona ni kubwa sana hailengi kumsaidi huyu mfanyakazi au mwananchi wa kawaida. Sasa mimi kwa kweli mara nyingi nikiona kitu kimechangiwa sana sipendi kupoteza wakati kwa kweli hilo ndio ningependa kusisitiza kwamba wajaribu kutizama kabisa hii riba, hii riba inawaumiza sana, mtu anarejesha mwisho wa mwezi kuja kufikia ile miezi sita, mwaka hakuna chochote alichokifanya kama yeye. Kwa hiyo anajikuta amerudisha pesa ileile.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii maana na mimi kidogo angalau nimejaribu kusikika hata Maswa wamejua kwamba nipo ahsante sana. Baada ya kusema hayo naiunga hoja hii mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu katika Muswada huu. Nami naomba niungane na wenzangu kwanza awali ya yote kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Makamu wake wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Manaibu Mawaziri, pamoja na safu nzima ya Serikali kwa kweli kwa kutimiza siku mia moja katika nafasi zao lakini kwa mafanikio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imeshakuwa mazoe katika dunia yetu ya sasa kwamba siku mia moja zimekuwa ni kigezo cha kupima mwanzo mzuri ama mbaya wa Serikali inayokuwa kwenye madaraka, sasa sisi kwa Watanzania tuna nafasi ya kujivunia kwa sababu wananchi wameshuhudia vyombo vya habari vimeshatoa taarifa mbalimbali zikiwa zinaonyesha kuridhishwa na utendaji kazi wa Serikali yetu ya awamu ya nne kwa hivyo naipongeza sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri wa Fedha, mama yetu Mheshimiwa Zakia Meghji kwa kuleta Muswada huu pamoja na maafisa wengine wa Serikali pamoja na Benki na Taasisi zingine ambazo zimeshiriki kutayarisha Muswada huu. Pia niipongeze sana Kamati husika, Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa jinsi ambavyo imeshiriki kuupitia Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongezi hizo naomba sasa nami nijikite katika Muswada huu ulioko mbele yetu, nitakuwa na maeneo manne ya kuchangia. Kwanza ni lile ambalo wengi ambalo wameshalisema sana lakini mimi naomba tu niongeze msisitizo na hili linahusu ushiriki wa *BOT* kama Benki Kuu wakati wa utekelekezaji wake wa majukumu yake katika kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja katika nchi yetu. Tunajadili Muswada unaohusu Taasisi za kifedha zikiwa pamoja na benki. Lakini kwa hapa ilivyo Benki Kuu wana mkono wao mrefu ndio wanaohusika na masuala ya usimamizi katika Taasisi hizi.

Mheshimiwa Spika, mimi mchango wangu hapa nilikuwa naomba kusisitiza kama ambavyo wenzangu wamekwisha kusema wajipange upya wajiridhishe ni jinsi gani wana-*fit* katika mikakati ambayo Serikali ya awamu ya nne imejiwekea kupitia Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ambayo hiyo inakwenda mpaka mwaka 2010

kuna mikakati mitatu lakini katika hii taongolea mikakati miwili. Mkakati wa kwanza ni huu wa MKUKUTA yaani Mpango wa Kupunguza Umaskini na Kukuza Uchumi, lakini pia kuna huu Mkakati wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara Tanzania yaani MKURABITA.

Mheshimiwa Spika, hii ni baadhi ya mikakati ambayo Serikali katika utekelezaji wa ule mpango wa muda mrefu wa kumhakikishia kila Mtanzania maisha bora imeweza kuona kwamba mambo yote tunayoyafanya yanalenga kuhakikisha kwamba kila Mtanzania anapata fursa ya kuishi maisha bora kuliko ilivyokuwa awali na kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ni changamoto kwa Benki Kuu, kulingana na majukumu yao waliyonayo ya kisheria wajipange waone jinsi gani wana-*fit* katika hili. Kwa kufanya vile ninahakika kwamba watakuwa wamesaidia sana nchi hii kupiga hatua kubwa za maendeleo kututoa hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, ninalisema hili kwa sababu hata katika *level* ya Kitaifa sasa tuna *philosophy,* tuna fursa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuja na *philosophy* yake katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali ametukumbusha tusifanye kazi kwa mazoea na matokeo yake tunayaona.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hapa ndani ya Bunge tunafahamu kinachoendelea, tunakwenda kwa utaratibu wa *double "S"* yaani *Standard and Speed* ni huduma kwa viwango na kasi. Sasa naamini kwa majukumu ambayo Benki Kuu imepewa kusimamia hizi Taasisi za kifedha na mabenki. Katika kuimarisha uchumi wa Mtanzania na hasa ule uchumi wa mtu mmoja mmoja kuna kila sababu Benki Kuu nadhani kuja na falsafa yao ambayo itakuwa imezingatia falsafa tatu ambazo zinaongoza Watanzania kwa sasa ambazo zitatoa mwelekeo sahihi wa kuonyesha mchango wao, ambao mwananchi mmoja, mmoja, atauona katika uchumi wake binafsi. Wakija na falsafa hiyo itakuwa ni hatua kubwa sana kutusaidia sisi kama Watanzania lakini pia wao watakuwa wametimiza wajibu wao kwa kiwango ambacho Watanzania wataridhika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ambacho nasisitiza hapa ni wao kujipanga upya ili kuendelea na hizi kazi. Nasema hayo kwa sababu kwa hakika Benki Kuu na Taasisi nyingine za Kifedha haziwezi kuwa nje ya hii falsafa ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya, lakini pia inapofanya kazi kwa mazoea na pia hawawezi kuwa nje ya utashi ambao tunautaka tufanye kazi kwa viwango lakini kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia utendaji wetu kuna mambo ambayo Benki Kuu na Taasisi za Kifedha zina fursa ya kuboresha zaidi kuliko ilivyo sasa. Mojawapo kwa mfano, leo tunaongelea kuwasaidia wananchi wa Tanzania, lakini hasa walengwa wakubwa ni nani katika hili? Tunapoongelea umaskini wa Tanzania kama ambavyo Waheshimiwa wengine wamekwishasema hapa, kwa kiwango kikubwa tunaongelea tatizo linalowakumba wananchi wetu ambao ni asilimia 80 wanaoishi vijijini. Hawa ndiyo walengwa wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, amekuwa akitukumbusha kwamba kipindi hiki cha Awamu ya Nne ni kipindi cha kuweka mikakati ambayo mtu mmoja, mmoja atakuwa anapata uelewa na kuona kabisa kwamba uchumi wake binafsi umekua. Mazingira ya uchumi mkubwa yameshajengwa, lakini kazi tuliyonayo Watanzania ikiwamo Benki Kuu na taasisi nyingine sasa ni kuhakikisha kwamba uchumi wa mtu mmoja mmoja unakua. Tunapoongelea kwamba uchumi unakua na sasa hivi tuko kwenye asilimia 6.7, je, mwananchi wa kawaida, mwananchi wa kule Bitoto, mwananchi wa kule Sengerema ninapotoka mimi, mwananchi wa Urambo, mwananchi wa Njombe anaelewa kweli haya tunapoyasema ama inakuwa ni nadharia tu kwamba uchumi wetu unakua?

Kwa hiyo, huu ni mkakati mmojawapo ambao nadhani ni jambo la msingi sana kwa Benki Kuu kuzingatia kuona ni jinsi gani wana-*fit* katika hii mikakati ya MKUKUTA na MKURABITA. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tumekuwa tukihamasisha watu na sasa hivi tunaendelea kuhamasisha watu wajiunge katika vikundi vya uzalishaji na hasa *SACCOS* ambazo zitasaidia sana wao kuweza kukusanya nguvu zao na kufaidika na matunda ya fursa ambazo zinapatikana ndani ya Serikali yetu ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hili, naomba niwakumbushe kuhusu kutofanya kazi kwa mazoea. Napenda nitumie nafasi hii kuipongeza sana Benki ya *CRDB*. Benki ya *CRDB* kwa kweli katika Taifa letu imekuwa ikifanya kazi kubwa sana na imeonyesha kwa kweli kwa vitendo ina-*fit* katika mikakati hii ya Serikali ya MKUKUTA na MKURABITA. Wameshaanza kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali katika nchi hii, lakini tunafahamu kuna jambo na ndiyo maana hoja hii ninayoisema nasisitiza kwa ndugu zangu wa Benki Kuu ya kuwezesha kujenga mazingira, kurahisisha ile *facilitation* ya *players* ambao wanataka kufanya kazi kusaidia kutimiza hii mikakati yetu. Najua wameomba leseni pale ya kufanya *wholesale* ya *micro financing*. Nadhani hili ombi la leseni lina zaidi ya mwaka sasa, ndiyo maana nikaanza na maneno ya utangulizi kwamba tunahitaji kujipanga tuone tuna-*fit* jinsi gani katika falsafa hizi tatu ambazo viongozi wetu wakuu wa ngazi ya Taifa letu wamezitoa.

Mheshimiwa Spika, ombi limekaa pale kwa zaidi ya mwaka mmoja, lakini ambacho tunakisikia ni kwamba hawajakamilisha sera yao ya jinsi gani mpango huo wa kutoa vibali kwa mabenki na taasisi zingine ufanyike. Haya ndiyo mambo ambayo nadhani kwamba ni changamoto kwao, tuache kufanya kazi kwa mazoea, tujipange katika mikakati hii, vibali vitoke na hapa Mheshimiwa mmoja alitukumbusha kile kifungu cha kumi kwa hii sheria mpya kinasema: "Leseni zitatoka ndani ya siku kumi." Ninaamini ni pamoja na ombi la Benki ya *CRDB* ambalo sasa hivi liko *pending* Benki Kuu.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya msingi sana, tunasisitiza kwa sababu ni mambo ambayo yanamgusa mwananchi wa kawaida moja kwa moja, kwa hiyo ndugu

zangu wa Benki Kuu mlione hilo, mjipange upya, mfanye kazi ya *facilitation* kwa kasi na kwa viwango ambavyo vinakubalika, tuachane na kufanya kazi kwa mazoea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuongelea katika hili ni suala la utungaji wa taratibu ama kanuni za jinsi ambavyo Benki Kuu itakuwa inasimamia utekelezaji wa mambo mengine zikiwemo Asasi za Kifedha na mabenki. Tunaona kuna vifungu ambavyo vinaeleza, kwa mfano ukisoma kifungu cha 17 kinaelezea kiwango cha mitaji kuhusu Taasisi za Fedha zinazotoa huduma za fedha maeneo ya vijijini. Sheria inawapa mamlaka ya kutoa kanuni ama kutoa viwango vya kiasi gani au wakati leseni zinatolewa ni ada kiasi gani zilipwe na hao waombaji wanaotaka kufanya shughuli hizi za kifedha huko maeneo ya vijijini na sehemu za mijini. Tunasema hii sheria inataka kuweka utaratibu mahsusi ambao utakuwa unatoa ufafanuzi kwanza. Utaratibu huu unaeleweka na ni mahsusi na utawezesha urahisishaji wa utekelezaji wa majukumu ya kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali yakiwemo mabenki. Lakini kanuni hizi nadhani nyingi haziko wazi sana kwa walengwa ama wadau katika shughuli hizi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Benki Kuu kwamba hizi kanuni basi wazitunge mapema na ndiyo haya niliyoyasema kwamba tusifanye kazi kwa mazoea. Tunakumbushana, tunajadili mambo haya ili tu-*fit* katika hizi falsafa ili tuweze kuwa wazi zaidi. Lakini kwa kufanya hivyo tutakuwa tumeisaidia sana Tanzania kuweza kunufaika na hizi taratibu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwa mfano, kuna suala la kiwango gani mabenki yanaweza kuwekeza katika taasisi ambazo hujishughulisha na mamlaka ya fedha. Hili linahusu uwekezaji. *CRDB* wameomba leseni ambayo kama wataruhusiwa itawawezesha wao kuunda chombo kingine ambacho kitakuwa kinaratibu utoaji wa mikopo kule kwenye taasisi nyingine na hasa *SACCOS* kule nje ya wilaya, zinakwenda mpaka kwenye kata na tarafa. Sasa hapa hawako wazi. Sheria haiko wazi, lakini nadhani kwenye kanuni wataeleza. Kwamba, hiki kiwango cha wao, kwa mfano Benki ya *CRDB* kuwekeza katika hicho chombo ambacho wanataka kukianzisha wawekeze kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ambayo nadhani kwenye kanuni zao yatakuwa wazi kwa sababu wao ndiyo wanaratibu. Ni jambo la kuzingatia kwa sababu naamini litawakwaza wengine ambao wanataka kujua. Unaweza kusema kwamba wakitaka kuja waje wafanye *consultation,* lakini wadau katika shughuli hii ya maendeleo si wale tu wanaotaka kuanzisha, kuna watu wengine wanataka kujua kwa sababu wanakuwa na *interest*. Kwa hiyo, ni vema basi kanuni zikatoka mapema ili zinapotoka zitangazwe kwenye vyombo vya habari ili watu wajue kwamba zinakuwaje na wanapotaka kufanya, wafanye kwa kiwango gani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niliongelee ikiwa ni sehemu ya mkakati huu wa *BOT* ku-*fit* katika ile mikakati miwili ya MKUKUTA na MKURABITA ni suala la uwajibikaji. Ukisoma ule Muswada wa Benki Kuu ambao tumeupitisha juzi, nadhani kwenye kifungu cha 21 kuna sehemu ambayo wao watakuwa wanatoa taarifa

kwa Waziri wa Fedha ndani hasa ya kipindi kisichopungua miezi sita. Kwa hiyo, ni kama mara mbili kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naomba kushauri hapa ni kwamba kwa sababu nchi yetu imegubikwa na umaskini kwa kiwango kikubwa na wananchi wetu zaidi ya asilimia 80 wako vijijini na Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko hapa, napendekeza kwenye taarifa ile ambayo wanapaswa kuileta kwa Waziri wetu Mama Zakia Meghji, kwa sasa basi iwe na *component* pekee inayohusu ushiriki wao katika kufanikisha utoaji mikopo vijijini.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu kama litachukuliwa kwa uzito wa aina yake na kwa kweli hii ni *crisis* sasa hivi kwa sababu umaskini unaotugubika ni tatizo kubwa sana. Nadhani kama tutaweka huo utaratibu kwenye ripoti yao ielezee ni jinsi gani wame-*facilitate* kutoa mikopo kwenye sehemu za vijijini itakuwa imetusaidia sana kujua kwanza wao wenyewe ushiriki wao katika mchakato huu mzima, lakini pia kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewatendea haki Watanzania walio wengi sana na hasa kwa sababu wengi wetu tunakaa vijijini. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo la kuzingatia kuona kwamba ni jinsi gani *BOT* inashiriki katika mchakato mzima wa kumhakikishia kila Mtanzania maisha bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Benki Kuu imesheheni wataalam wa mambo mbalimbali, Serikali imesheheni na kuwashauri wadau wengine wa nchi hii tuangalie kama kuna uwezekano wa kuwa na mfuko maalum wa kusaidia hasa vikundi vya uzalishaji na utoaji huduma huko vijijini kama vile *SACCOS.*

Mheshimiwa Spika, tukiwa na mfuko rasmi, siwezi kusema hasa undani wa mfuko uweje, lakini naamini kwa sababu hili ni wazo tunalitoa, wataalam wako hapa wanaweza kuona kama inawezekana wakatumia hiyo nafasi kwa mamlaka ambayo wao wanayo kuweza kuanzisha mfuko kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mama Zakia Meghji pale kuona ni jinsi gani tunaweza kuanzisha mfuko wa fedha kwa ajili ya kusaidia ku-*complement* juhudi ambazo zinafanywa na taasisi nyingine kama mabenki kutoa mikopo kwa maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwa mara nyingine tena kwamba naunga mkono hoja hii na ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Gavana pamoja na watayarishaji wote wa Muswada huu ambao tunauzungumzia unaohusu *Banking* na *Financial Institutions*, ahsanteni sana.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwa kweli napenda kuwapongeza kwa sababu binafsi naona nilikuwa na maswali mengi kichwani kuhusiana na jinsi gani sasa Watanzania watawezeshwa, lakini naona Muswada huu umezingatia sana hali ya kuwaendeleza wananchi ili waweze kupata maisha bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida, pamoja na Muswada mzuri uliopo lakini kuna michango mbalimbali, ni lazima inajitokeza hasa kufuatia mazingira na hali halisi ya wananchi wetu ilivyo. Kuna siku nilikuwa nimekaa na vijana kwenye vijiwe vyao wakawa wanzungumza: "Sasa tumeshaahidiwa na hii ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya, lakini nguvu tunazo?" Tunamuona Mheshimiwa Rais kwa kweli jinsi anavyotuelekeza ana nia hasa ya kutusaidia, lakini sasa tutasaidiwa vipi? Yaani walikuwa kwenye *discussion* zao.

Mheshimiwa Spika, naona kwa kweli maelekezo ambayo yametolewa na Mheshimiwa Rais yatafanikiwa tu endapo sisi wote kwa pamoja tutashirikiana kuweza kutoa mawazo ya aina mbalimbali, uwezeshaji wa aina mbalimbali ili kuhakikisha kwamba maneno yake yanakuwa timilifu na hasa katika kipindi hiki cha mwanzo ambacho wananchi tayari wamejenga imani kubwa sana na Mheshimiwa Rais wa nchi hii pamoja na Serikali yake kwa ujumla na Waheshimiwa Wabunge wao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu naomba nifike hasa kwenye suala la wajasiriamali. Wajasiriamali wengi waliopo Tanzania ni wale ambao wamejikuta wakiingia katika shughuli mbalimbali kufuatana na hali halisi ya ukwasi unaojitokeza, kwa mfano kufuatia kupunguzwa makazini au kustaaafu. Wengi wamejikuta wanakuwa hawana shughuli maalum ya kufanya ya kuwaingizia kipato, hawana ajira ya kudumu, kwa hiyo inabidi awe katika ajira binafsi. Unakuta mpaka sasa hivi katika nchi yetu Tanzania kuna *gap* kubwa sana kati ya wafanyabiashara wajasiriamali wakubwa wakubwa na wajasiriamali wadogo wadogo. Kitu kingine ni kwamba wajasiriamali wadogo wadogo wamekuwa hawakui miaka hadi miaka. Toka ulivyomkuta anauza genge lake la maembe au ndizi miaka hiyo labda miaka ya 2000, basi hata leo utakuta yuko pale pale yaani hakuna ile hali ya kukua. Tuna *layer* kubwa iko hapo chini na tuna wachache sana wako kule juu. Nadhani hapa ndipo tunapotakiwa kupafanyia kazi zaidi. Vile vile, katika *data* inaonyesha kwamba *percent* kubwa ya wananchi wanaoishi Tanzania wanaishi kutokana na biashara au shughuli zisizo rasmi na ndiyo maana MKURABITA ukajitokeza.

Mheshimiwa Spika, vile vile nilikuwa naangalia kwa upande wa pili. Unakuta labda kwa mfano wanafunzi wengi wanaokuwa wamehitimu, kwa mfano kwenye masomo ya biashara au ufundi wanakuwa wameelimishwa vizuri kiasi cha kuweza kujiajiri, lakini wengi wao baada ya kumaliza hawako tayari kujianzishia shughuli zao, nao wanakuwa katika mkumbo ule ule wa kutafuta ajira ya Serikalini au kwenye mashirika ya umma ambayo tayari yameshapunguzwa kwa kiasi kikubwa sana. Sasa unajiuliza ni kwa nini hawako tayari na wakati kila siku wanafundishwa masomo hayo hayo ambayo yanahusu kujiajiri?

Mimi binafsi baada ya kufuatilia nimegundua kwamba, ile hali ya kutokuwa na uhakika wa kile ambacho wanategemea kukianzisha, *security* haipo matokeo yake sasa wanakuwa wanakosa ile hali ya kuwa na mwelekeo. Lakini vile vile endapo wangekuwa wamewezeshwa, wangeweza ku-*accommodate* wale wote wanaokuwa na woga wa kujiajiri na hivyo wakaweza kuanzisha shughuli ambazo zingeweza kutoa jibu hili la ajira binafsi.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia mfano mwingine nikiwa kama mjasiriamali jinsi ambavyo Serikali yetu imeweza kuingia ubia na *institutions* mbalimbali kwa mfano *NBC,* pale tunakuta kuna hisa za Serikali, *TBL* kuna hisa za Serikali na za wananchi vile vile. Nikajiuliza, je, Wizara yetu ya Fedha au benki kwa ujumla ambayo inasimamia shughuli hizi za kibiashara, za fedha, hatuwezi kuwa na utaratibu wa *PPP* yaani *Public Sector Private Sector Partnership* katika suala la kuwawezesha kimtaji? Kwa mfano, tuchukulie sasa hivi tulikuwa tunaongelea jinsi gani tutawapata Ma-*deputy Governors* na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye kuanzisha makampuni kuna watu tayari wana ujuzi ambao baada ya kumaliza amebobea vizuri labda kwenye *Business Management*, anaweza aka-*manage* vizuri ile biashara, lakini tu kwa sababu ya kukosa *security* anaogopa kuanzisha biashara yake binafsi. Sasa nikafikiria kwamba, endapo kutakuwa na *shares* za Serikali ambazo zitakuwa tayari kuchangia katika shughuli zile za wale ambao tayari wana uwezo wa kuendesha shughuli kwa mfano uanzishwaji wa viwanda kwenye maeneo ambayo sasa hivi hakuna viwanda, mfano viwanda vya matunda, basi Serikali ingeweza kutoa sehemu ya mtaji kwa kuungana na hawa ambao wana uwezo wa kuendesha ili waweze kuwaajiri wenzao ambao hawana ajira na hivyo kuweza kukamilisha dhamira ya Serikali ya kutoa ajira kwa watu wengi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwepo utaratibu ambao kwa mfano, kama kutakuwa na kikundi cha wahitimu wa Chuo Kikuu labda sita ambao vyeti vyao vinaweza vikachukuliwa kama dhamana wapewe *shares* na Serikali ambao pia watapewa mtaalam wa kuwa-*support* katika ile shughuli wanayoianzisha. Halafu waendelee kuwa nao wakiwa wanafahamu fika watawaajiri watu wa aina gani, kutakuwa *of course* na *business plan* itakayokuwa inaongoza. Baada ya kufanya hivyo labda kwa miaka mitano wanaweza waka-*graduate* na hivyo wakawaacha waweze kujiendesha wenyewe na Serikali labda ikajitoa sasa ili kuweza ku-*support* wengine wanaoanza.

Mheshimiwa Spika, nimesema hivyo pia kufuatia *policies* nyingi ambazo zipo, nyingi zimeishia kule kwenye makabati yetu, hazijulikani vizuri. Mfano ni *SME policy* ambayo inazungumzia wazi kuwepo kwa vitotozi *(incubators*) kwa ajili ya wajasiriamali. Hatuna hizo *incubators* mpaka sasa hivi na hii *policy* sasa hivi imeishakuwa na umri mkubwa tu, inafika sasa karibu miaka minne. Nafikiria kwamba dhamira ya kuzitengeneza hizo *policy* inakuwa ni nzuri, lakini utekelezaji wake unakuwa ni mdogo kwa sababu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine nadhani itakuwa ni wawezeshaji tulionao *(Business Development Services Providers).* Wengi wao hawajawa katika makundi maalum. Unakuta leo *BDS* huyu anashughulikia suala la UKIMWI, kesho anashughulikia la biashara, kesho kutwa anashughulikia la mazingira, huyo huyo mmoja. Sasa hata ule uendelezaji wa kile ambacho kinakuwa kimeanzishwa unakuwa hauna mtiririko.

Kwa hiyo, naomba pia hata kwa upande wa hawa *BDS* wetu tuweze kuwafanyia *screening* kama ilivyo kwenye *contractors*. Sasa hivi tunafahamu kuna *Electrical Contractor Class A, Class I* mpaka *VII*, tuna *Civil Contractor Class I* mpaka *VII* na *condition* zake ziko wazi.

Kwa hiyo, tunafahamu fika kwamba huyu atakuwa amebobea kwenye *line* hii na hivyo ataweza kuendeleza katika misingi hii na hiyo na hivyo tunaweza hata ku-*monitor*. Lakini kwa huu mchanganyiko uliopo sasa hivi na hizi *NGOs* zetu zinazoibuka nyingi zinajiita *non profit making* kama zilivyo. Isiwe kigezo, tulenge *profit* ile ambayo hata haionekani, lakini kimsingi ni *profit* kwa sababu inakuwa imewezesha. Kwa hiyo, kwa kweli naomba sana tuangalie katika hili.

Mheshimiwa Spika, upande mwingine nilikuwa nazungumzia kuhusu uwekezaji hasa kwa wawekezaji wa ndani kwenye suala la *tax holidays.* Kwa wawekezaji wa nje nadhani ni wazi kabisa, miaka angalau kumi mtu akishawekeza inabidi aangalie biashara inaenda vipi na kwa sababu tuna-*encourage* kuweza kupata ajira zaidi kwa watu wetu kwa hiyo tunajaribu kumpunguzia maumivu. Lakini vile vile, kwa wawekezaji wa ndani na wenyewe wakifanyiwa hivyo hata angalau miaka mitano nadhani itachochea sana uwezekano wa hawa wajasiriamali wetu kukua. Pamoja na jitihada nzuri ambazo tayari zimeishafanyika katika utoaji wa leseni na vile vile katika uboreshaji wa huduma za *TRA,* lakini kweli naomba pia kusisitiza kwamba uwepo uwezekano wa kupewa likizo hiyo ya kodi kwa hawa wawekezaji wa ndani kwa sababu wote tunalenga katika kutoa ajira na kuwawezesha zaidi wananchi wetu kuweza kujipatia mahitaji yao ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba napenda kushukuru kwa mtaji ambao mmeuzungumzia na ninazidi kusisitiza kwamba kwa wale ambao watakuwa wanaanzisha benki katika maeneo ya vijijini, basi mtaji wao uweze kupunguzwa ili kutoa *incentive* kwa watu wengi kuanza benki katika maeneo ya nje ya miji na pia kuwepo na *pressure* ya kuziwezesha hizo benki ambazo zimejazana mjini zirudi kwenye maeneo ambayo yana ardhi za kuweza kufanyia shughuli.

Mheshimiwa Spika, benki nyingi sasa hivi unakuta ziko Dar es Salaam na wawezeshaji wengi wanakuwa Dar es Salaam na vijana wetu wanachama huko vijijini wanakimbilia Dar es Salaam kwa sababu kila kitu kizuri kinakuwa kiko pale. Ninachukulia Dar es Salaam kama mfano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo yanakuwa wazi ambayo ndiyo yangetosheleza kwa uzalishaji. Maeneo ya mjini sasa yanakabiliwa na matatizo mengi, unakuta tayari kunakuwa na *environmental impact,* mtu wa mazingira sasa anahangaika. Ukirudi kwa upande wa makazi ni tatizo, ukirudi kwa upande wa barabara ni tatizo. Kwa hiyo, tusambaze hizi huduma zetu ili kuwawezesha wananchi waridhike kukaa kwenye maeneo wanayotoka kuliko wote ku-*concentrate* katika maeneo ya mjini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia hayo naomba nishukuru kwa kuwa mambo mengi wameyafanyia kazi na pia napenda kuwashukuru zaidi watayarishaji. Mheshimiwa Waziri, kwa kweli nimeona mmekuwa *flexible* sana kuweza kurekebisha

hasa kuweza kutu-*accommodate* sisi katika yale ambayo tunayaona yanawagusa wananchi. Tunashukuru sana kwa hali hiyo ya kuwa na mwelekeo wa kujali wananchi wenu. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Namwita sasa Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa na kwa hali halisi ninayoiona, tutamalizia na Mheshimiwa Martha Umbula kwa asubuhi ya leo.

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lyamba yupo.

**SPIKA:** Sawa sawa. Basi wote, muda unatosha**.**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa ni mara yangu ya mwanzo na mimi sina budi kutoa shukrani zangu kwa ushindi mzuri kwa Chama cha Mapinduzi, nikianzia na Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Makamu wake wa Rais kwa ushindi walioupata. Pia, natoa pongezi kwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa kuwa na ushindi wa hali ya juu ambao kwa kweli wananchi wamekuwa na imani nao baada ya kuona utekelezaji wa awamu iliyopita unavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia natoa pongezi kwa wananchi wa Jimbo langu la Bububu kwa imani yao na ujasiri mkubwa kabisa kwa kuzingatia kwanza mimi jina ni Cosmas na eneo ninalotoka ni tofauti kidogo kwa sababu wao ni Waislam wengi. Lakini kwa imani yao wameweza kunichagua bila kuzingatia kwamba ni kabila gani au jinsia gani. Nawapongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, nawapongeza Mawaziri kwa kuteuliwa na bila kumsahau Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na baadaye na sisi tukampitisha kwa kura nyingi. Ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwanagenzi kwa mambo hayo, lakini nisingependa kurudia rudia, ningependa ku-*hit points* ambazo nahisi kwamba zinaweza zikasaidia kidogo. Kwa sababu benki imeshapewa uhuru huu wa kusimamia, ni jambo zuri kwa sababu ninaamini wawekezaji wengi watakuja nchini na watakuwa ni wa nje zaidi, kwa hiyo mabenki mengi ni lazima Serikali ijihadhari nayo kwa sababu wanakuja hapa kwa sababu wanajua watapata *interest* kubwa na baadaye wataondoka watuachie mashaka na umaskini.

Mheshimiwa Spika, suala la leseni ni lazima liambatane na kumwangalia anayetaka kupewa hiyo ruhusa kwa sababu kuna mitandao mingi mikubwa sana. Wengine watakuja na mabenki ya kiroho, watawa-*convince* watu, lakini matokeo yake wanatuletea matatizo. Yatajengwa makanisa mengi, itajengwa misikiti, hii itakuwa haitusaidii sana sisi. Lengo ni kuimarisha uchumi wetu kwa kusaidia wakulima wetu. Kilio kikubwa hapa ni wakulima. Tanzania hatujawa na wakulima wa hivyo, bado tuna *peasants* ambao ni wakulima wadogo Wadogo. Sasa ni vyema Serikali ikalitupia jicho

hili ikiwezekana *BOT* yenyewe ikawa na ki-*branch* au taasisi maalum ambayo itahusu mambo ya kilimo na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano Kagera kule kuna matatizo, sasa hivi wanasema bei ya ndizi imepanda kwa sababu kuna maradhi ya migomba. Sasa maradhi ya migomba yamesababisha ndizi hazipatikani kwa wingi na wananchi wa sehemu hiyo hawapati msaada wowote wa kuweza kuinua au kuboresha mashamba yao kwa mfano dawa. Kwa hiyo, ni vyema Serikali au *BOT* ikawapa *priority* ambao watakuja na nia ya kuanzisha mabenki au taasisi ambayo itaanzisha benki hapa nchini basi sheria mojawapo ni kwamba ni lazima wakulima kama hawa wasaidiwe mambo ya pembejeo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni udhibiti wa hizi *Bureau de Changes.* Hapa nchini unaweza ukaenda mji wa Dar es Salaam ukatembelea *Bureau de Change* kama tatu, nne kila mmoja ana *exchange rate* yake. Sababu hizi kwa kweli zinasababisha thamani ya pesa inakuwa inashuka, haithaminiki. Unaweza ukaenda *Bureau de Change* moja anakwambia dola moja kwa shilingi 1,200, mwingine shilingi 1,300 ili mradi hakuna udhibiti maalum. *BOT* ingekuwa ni vyema wakawa wanatoa *instructions* kwamba katika wiki hii au katika kipindi ambacho kinaonekana kuna haja hiyo basi wapitishe maelekezo kwa kila *Bureau de Change, information* kwamba katika wiki hii au katika siku hizi *exchange rate* ni hii, isiwe na tofauti.

Mheshimiwa Spika, utaona kwamba sasa hivi ukikaa siku mbili unakuta *exchange rate* ya *Tanzania shilling* inazidi kwenda chini. Lakini ukienda *NBC* au mabenki ambayo *BOT* nafikiri inakuwa karibu sana na wenyewe wanajaribu kuwa wako *uniform,* lakini *Bureau de Changes* nafikiri ziko *loose* sana, wanafanya wanavyotaka. Imefika *time* sasa hivi wadhibitiwe na sidhani kama hizi pesa wanazobadilisha kama zinakuwa hapa nchini, zingine zinakwenda nje na sidhani kama Serikali inalifahamu hilo na kama inalitambua basi wafanye juu chini kuhakikisha kwamba hizo pesa wanazidhibiti.

Mheshimiwa Spika, wachangiaji wengi wamesema kwamba wanakuwa wanapo-*change* pale hupewi hata ile risiti. Sasa sijui watajizatiti vipi kuhakikisha risiti zinatolewa na ubabaishaji haupo.

Mheshimiwa Spika, ningezungumzia pia kuhusu suala la faini. Wasemaji waliopita wamesema kwamba kwa lugha ya kisheria faini inayotolewa ambayo ni *not exceeding so and so years* au faini fulani, basi ile *minimum*. Kungekuwa na *minimum* faini inayotakiwa kama ni milioni 10, lakini isizidi milioni 20. Lakini viboko navyo ni sehemu ya faini. Ni kwa nini pasiwe na bakora pia? Bakora na zenyewe ziingizwe. Mtu anakwenda kinyume, basi bakora angalau tatu au nne ili kuonyesha kwamba tuko *serious* na sisi kwa sababu Mwanasheria amepewa *loop* ya kuchagua lakini bakora nafikiri ni moja ambayo itakuwa ameshapigwa bakora aliyekosea kwamba anajua kumbe angalau kama nitalipa fedha kidogo lakini na bakora nimepigwa. Hilo liangaliwe bakora ni moja ya faini au adhabu itakayotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ningechangia kuhusu riba. Mabenki mengi kwa kweli riba inakuwa ni kubwa, unapokopa riba kubwa, lakini unapoweka wewe riba ni

ndogo. Lakini sasa Benki lazima iangalie uwiano pasiwe na *gap* kubwa sana ya kuweka halafu na kukopa. Kuwe na *ratio* yaani uwiano usizidi kwa asilimia japo 10. Kama ni riba ya kukopa ni asilimia 16 basi na ya kuweka basi labda iwe asilimia 12. Pasiwe na *gap* kama hiyo, kwa kweli hapa ndiyo inaonyesha kwamba mkulima hana uwezo na hataweza kukopa fedha kutoka Benki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *security* Mheshimiwa Vita Kawawa amezungumzia baadhi ya *components* zinazotakiwa lakini pia pawekwe na sheria ya makusudi kwamba ni mwenye Benki yoyote au Taasisi yoyote ya Benki, basi ni lazima awe na ulinzi wa polisi ambao wao tayari wana silaha na wawalipe kwa kiwango ambacho Benki itaona ni muhimu kwa kushirikiana na kikosi chenyewe. Kwa sababu fedha zinazoibiwa si kwamba ni za Benki ni fedha za wakulima na pia ni fedha ya Tanzania. Kwa hiyo, kuna haja ya kuliangalia hili. Ninashukuru Rais, alitoa amri kwamba kila Benki lazima iwe na ulinzi wa polisi. Sasa hivi ndiyo afadhali mambo yamedhibitiwa. Kwa hiyo, *BOT* iangalie iliweke kwenye sheria kwamba Taasisi au Benki yoyote ni lazima iwe na ulinzi wa polisi na hapa ultimate security basi wawalinde kwenye majumba yao badala ya kwenye Benki.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naunga mkono Muswada huu kwa 100% na nampongeza Waziri kwa kuuwasilisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu wa utaratibu wa kudhibiti Taasisi za fedha nchini. Nami pia naungana na wenzangu kuzipongeza jitihada za viongozi wetu wa ngazi ya juu katika kuleta ufanisi wa shughuli zote za maendeleo kwa kufuata kasma ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, kama nimeuelewa Muswada huu vizuri ni Muswada wa utaratibu wa kudhibiti (ku-*regulate*) Benki na Taasisi zingine za fedha kwa kuratibu shughuli za akiba na mikopo kwa nia ya kuimarisha usalama wa fedha na ufanisi wa Taasisi hizi ili kupunguza *risks* ya upotevu wa fedha za wateja ambao ni wananchi wanaoweka amana zao Benki.

Mheshimiwa Spika, Mabenki na Taasisi za kuweka fedha kama *CRDB, NBC* na zingine za sekta isiyo rasmi kama *SACCOS* na kadhalika zinahamasisha *savings* ama zina-*mobilize* akiba kutoka kwa wananchi kwa nia ya kuja kuzikopesha. Sasa katika ukopeshaji huo usalama unakuwa mdogo. Kwa hiyo, kwa sababu naamini kwamba huu Muswada unaweza ukawa wa msaada sana naamini kwamba itaimarisha sana sekta ya fedha nchini kwa maana ya usalama, ama kutopotea kwa fedha za wananchi.

Mheshimiwa Spika, kama basi tutakuwa na chombo cha kusimamia na kama nimeuelewa vizuri ndiyo nia ya Muswada huu, basi hatuna budi kuunga mkono na kushukuru Serikali na Wizara kuutayarisha Muswada huu. Tukiacha Benki kwa mfano *CRDB, NMB* na kadhalika hizi za *formal landing* na tukazingatia *Financial Institution* ama *Financial Companies* kama *PRIDE, FINCA* na kadhalika ambavyo imejulikana katika Muswada huu ambazo zinatoa mikopo yenye riba kwa bahati mimi nimefanya kazi katika Taasisi kama hizo za *Financial Institution* kwa zaidi ya miaka kumi, kwa hiyo, ningependa pia ku-*share* uzoefu.

Mheshimiwa Spika, unapoanzisha Taasisi kwa mfano ya kutoa mikopo ama *Financial Institution* ama *SACCOS* nia ni kudumisha ama kuendeleza Taasisi hiyo, ili pamoja na Taasisi kudumu na suala zima la kukopesha iwe endelevu. Sasa katika kujitosheleza huko kwa sababu katika kuanzisha Taasisi kama hiyo unakuwa na mawazo mawili, kwanza kuhakikisha kwamba ukopeshaji huo unaendelea na hali kadhalika Taasisi hiyo inadumu. Sasa inabidi riba inayoweka kwenye mkopo inatosheleza na inakuwa ni mkakati mmojawapo wa kufanikisha suala zima la uendelevu wa Taasisi za kukopesha.

Kwa mfano, kama nia ni kuwakopesha hususan wanawake ambao ndiyo sehemu kubwa ya jamii ambayo hizo Taasisi za fedha zinaokopesha sasa hivi kwa nia ya kuhakikisha kwamba shughuli hii inakuwa endelevu kiasi cha kuonyesha *impact* yake katika sehemu husika inabidi, kunaiwekea riba ambayo itaweza kui-*sustain* au kudumisha Taasisi yenyewe ama *Financial Institution* yenyewe na hali kadhalika pia isimuumize yule mteja wako ambaye unamkopesha. Sasa hii inakuwa changamoto. Kwa sababu utakuta tunaowalenga sisi ni watu ambao hawana uwezo na watu ambao hawana uwezo unapompa mkopo na unategemea kwamba atarejesha kwa kutumia riba ya asilimia kubwa hususan ishirini hadi thelathini inakuwa bado haujatimiza lile lengo la kumkwamua kiuchumi ama kuinua hali yake na kupunguza umaskini. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inakuwa ni changamoto kwa sababu utakapoweka riba ya chini ina maana unapotoa mkopo mteja anarudisha mkopo wake ambao ni ile *principal* na *interest* ambayo ile *interest* sasa unaitumia kuendeshea Taasisi ama ku-*cover* zile *operations.* Sasa usipoweka riba ya kutosha ina maana kwamba Taasisi ile haitaweza kuwa endelevu na ndiyo maana Taasisi nyingi zetu za mikopo zinapoanzishwa vijijini haziendi kwa muda mrefu kwa sababu urejeshaji unapokuwa chini ya asilimia 50 kwa mfano ina maana kwamba zile fedha zinazorejeshwa hakutakuwa na riba ambayo inaweza sasa ku-*cover* zile *operations* za kui-*sustain* ama kuifanya Taasisi iwe endelevu. Kwa hiyo, hiyo inabaki kuwa changamoto katika suala zima la kuweka riba kubwa kwenye mikopo inayotolewa na *Financial Companies.* Riba ni lazima, lakini kwa kiasi gani ndiyo tatizo.

Kwa hiyo, kama ambavyo nimesikiliza sana na kwa uzoefu kidogo suala la kuanzisha *SACCOS,* si suala rahisi sana kama tunavyoifikiria kwa sababu *SACCOS* ni wanachama ambao wamejikusanya pamoja wakajiandikisha kama wanachama wakachanga fedha zao wakaziweka kwenye mfuko maalum, ili waweze kukopa kutoka kwenye mfuko huo. Sasa kwa Taasisi zetu ama kwa hali yetu ya kijijini utakuta *SACCOS* zile za watu wa vijijini hazidumu sana kwa sababu kwanza wameliki wanakuwa wao wenyewe na kwa ajili hiyo, zinapotokea *(priorities)* kipaumbele mteja anakwenda anachukua fedha zake zote kwa hiyo, ule uimara wa *SACCOS* una-*shake* mara nyingi *SACCOS* zinazodumu ni zile za wafanyakazi au watumishi ambao wanarejesha mikopo kwa kutumia mishahara.

Sasa hiyo inakuwa tena ni changamoto nyingine ndiyo maana kulenga maskini wa maskini inakuwa ngumu na utakuwa Taasisi nyingi za fedha zinabadili mwelekeo, badala ya kuwalenga wale walengwa hasa wanaangalia wale wateja ambao ukiwapa mikopo wanaweza wakarejesha kwa uhakika yaani wafanyabiashara wenye uwezo. Sasa inaleta

pia changamoto kwetu kuifikiria kwamba pamoja na nia njema ya kuanzisha Taasisi hizi ndogo ndogo za fedha ni lazima pia tuangalie uimarishwaji wake na uendelevu wake na kufikia suala zima la kupunguza umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, sasa katika *Financial Institutions* hali kadhalika tunapotoa mikopo hususan wanawake ambao ndiyo hasa walengwa ambao tunawalenga tunatoa mikopo kwa kuweka riba kwa vyovyote vile. Lakini vile vile fedha ambazo unazitoa kwa nia ya kuzirejesha ndiyo maana ya mkopo, kunakuwa na *forces* mbili zinazovutana. Wale wanaoendesha Taasisi wanategemea ile riba ku-*cover operations* kwa sababu ni lazima uifuatilie ile mikopo kwa gharama na utakapokosea kuzifuatilia urejeshaji unakuwa hafifu. Kama urejeshaji ukiwa hafifu ndiyo tena Taasisi haiwezi kuwa endelevu. Lakini vile vile kuna haja ya kuangalia unayemkopesha. Sasa unayemkopesha ukimuwekea riba kubwa inakuwa tatizo lingine.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa wale ambao hawana uwezo mikopo inakuwa ni matatizo katika kurejesha. Kama nilivyochangia pia kwenye Muswada wa Benki Kuu, uliopita nilipendekeza kwamba ni wakati muafaka kujaribu kudhibiti *interest rate* inayowekwa kwenye mikopo kwa ajili ya kuwakopesha wananchi wa vijijini kwa sababu kama itakuja sheria yenyewe yaani kuthibiti riba inayowekwa kwenye mikopo hii inaweza ikasaidia kuthibiti riba iwe sehemu ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, nikiainisha Muswada huu na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uwezeshaji jamii kiuchumi, pamoja na uhamasishaji jamii kukopa kwa nia ya kuinua uchumi, mimi nilikuwa na mawazo kwamba vijiji vyetu vingi vina matatizo makubwa ya uhaba wa maji, barabara na umeme/nishati vigezo ambavyo kwa kweli bila kuvizingatia ukopeshwaji kwa sehemu za vijijini unakuwa tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza kwamba Serikali, yetu izingatie kuboresha huduma hizi kule vijijini. Kama kuna uhaba mkubwa wa maji suala hili la ukopeshaji linakuwa halina mafanikio. Hali kadhalika na suala la umeme kwa sababu nishati ya umeme ni muhimu na suala zima la barabara kwa sababu suala hili ni la kibiashara. Kama hakuna soko la uhakika vile vile inakosa ufanisi. Mimi nilikuwa na mchango huu mdogo wa kuchangia katika Muswada huu wa taratibu za kudhibiti Taasisi hizi za ukopeshaji kwa nia ya kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Muswada huu kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kutoa shukrani za dhati kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu katika Muswada ulio mbele yetu, Muswada wa Mabenki na Taasisi za Fedha wa mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitamke tangu awali nisije nikasahau mbele ya safari kwamba naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote nikizingatia sababu nyingi na za msingi ambazo wamekwishaeleza Waheshimiwa Wabunge waliokwishachangia katika kuujadili Muswada huu.

Pia kabla sijatoa mchango wangu na ushauri kwa Serikali na Benki Kuu, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika siku 100 za kwanza ambazo kwa hakika wote tunajua zilikuwa ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa shupavu kwa hakika wamezikuna nyoyo za Watanzania wote kwa ujumla kwa jinsi ambavyo walishughulikia masuala mbalimbali yaliyoikumba nchi yetu katika siku hizo. Kwa kweli wameonyesha mfano wa kuigwa na sisi viongozi wote katika ngazi mbalimbali za Serikali, Mashirika ya Umma, Taasisi na hata Makampuni binafsi. Somo kubwa tumejifunza hapa ni ile dhana kwamba sisi viongozi wote tunawajibika kwa wananchi na kuwa kipaumbele ni kuwajali na kuwatatulia matatizo yao kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya na kwa moyo wa upendo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisahau kutoa pongezi za dhati pia kwa Mheshimiwa Zakia Meghji, Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake na Gavana wa Benki Kuu na wataalam wake kwa jinsi walivyoandaa na kuwasilisha Muswada huu ambao umefika wakati muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kueleza hayo napenda niseme machache yafuatayo, kwanza ni suala la uwajibikaji. Wote tunatambua na naamini Benki Kuu inatambua kwamba Muswada huu unawapa uhuru mkubwa zaidi na madaraka makubwa zaidi Benki Kuu, katika kutekeleza majukumu yao. Nafikiri ni budi waelewe kwamba uhuru huu mkubwa waliopewa unawaongezea pia kiwango cha uwabijikaji katika kutimiza majukumu yao. Kwa maana hiyo, hata pale watakapokuwa wameteleza licha ya kupewa madaraka watawajibishwa kwa kiwango kikubwa zaidi kwa yale ambayo yatakwenda upogoupogo. Chamsingi ninachotaka kusema hapa ni kwamba tunawategemea watautumia uhuru huu vizuri ili kuleta ufanisi mkubwa zaidi katika kutimiza majukumu yao. La pili, ambalo liko wazi ni kuwa mara nyingi Mabenki makubwa yenye hadhi kubwa ni wagumu kubadilika. Ni suala la *change of attitude* katika mabadiliko makubwa yanapojitokeza kama haya ambayo yatajitokeza sasa hivi baada ya Miswada miwili kupitishwa na kuwa sheria. Benki Kuu mara nyingi zinajulikana ingawa siyo zote, kuwa wagumu ku-*change altitude* kwa sababu ya *inherent* urasimu ambao ukiwa *subjected* na *change* pengine huwa ni vigumu ku-*accommodate change* haraka.

Kwa hiyo, tunawategemea Benki Kuu wa-*change attitude* kufuatana na mabadiliko ya *services* ambazo sasa hivi zitapanuka kutokana na majukumu ambayo wanategemea kuyatekeleza. Ili ili waweze kuyatimiza majukumu yao ambayo tena yanaongezeka kuwa mengi zaidi budi watimize majukumu hayo kwa ufanisi na dhana ile ile ya ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. Wakatekeleza majukumu yao kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi ya zamani watakuwa wameboronga. Hatutakwenda kama inavyotegemewa. Kwa hiyo, tunaamini watakwenda sambamba na mategemeo ya sisi wote wananchi na Serikali kwa ujumla. Sina hakika kwa kiasi gani Benki kuu inaifahamu vizuri Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nafahamu kwamba wao ni wataalam na si

wanasiasa lakini, nashauri tu wawe wapesi au wapewe vile vitabu vya Ilani ya Chama cha Mapinduzi na wabobee katika lile eneo linalohusu masuala ya Benki ili iwe ni dira kwao wakati wote kurejea na kuhakikisha wanatimiza yale tunayoyategemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni suala linalohusu jinsi wanavyotakiwa kujishusha kwa kutoa huduma ambazo zitaenea kwa upana mkubwa vijijini. Benki Kuu sasa itabidi ijihusishe katika ngazi za chini kabisa kwa Mabenki na Taasisi za fedha zitakazoenezwa kule kama ni *Community Banks, SACCOS* na kadhalika hasa ukitegemea kwamba miradi ya MKUKUTA na MKURABITA itaenezwa katika maeneo ya vijiji. Kwa sababu hiyo itabidi watafute namna ya kuweka aina ya mtandao utakaopenyeza huduma zao za ushauri utakaokwenda mpaka chini ili Taasisi hizo mpya na changa ziweze kupata muongozo unaostahili kuwezesha kutoa huduma nzuri kwa sisi ambao tupo vijijini. *(Makofi)*

Wanavijiji ni watu wasioelewa masuala ya urasimu. Kama alivyozungumza Mheshimiwa mmoja Bungeni, wengi hata kwenda Benki wanaogopa. Wakifika kule wakikuta mtu amevaa suti na tai wanajua huyu ni mtu mwenye fedha hata kuongea naye wanakuwa na wasiwasi kidogo. Kwa hiyo, kwa wanavijiji itabidi elimu kubwa itolewe na *publicity* kusambaza *pamphlet,* programu za redio na majarida mbalimbali ya kuwawezesha kuwaondoa hofu na kuwa-*encourage* kwamba ni jambo zuri kabisa kuweka fedha kwenye *community banks* na ni jambo zuri pia kukopa wala siyo suala la aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine labda ni suala la tafsiri sahihi na mpango wenye kueleweka juu ya suala la MKUKUTA na MKURABITA wananchi wengi vijijini wanazungumza na kutumia maneno haya lakini hawajapata mwanga kabisa programu na ratiba au *procedure* au utaratibu wa utekelezaji wa miradi ya MKUKUTA na MKURABITA itatekelezwa kwa hatua zipi? Labda wakati umefika Taasisi husika na bila shaka zikisaidiana na Benki Kuu au Benki nyingine na Serikali, zitoe maelezo yaliyo fasaha kabisa kuhusu utekelezaji na maandalizi kutekeleza miradi itakayoendeshwa na MKUKUTA au MKURABITA.

Suala lingine linahusu elimu kwa viongozi wa Benki Kuu. Elimu haina mwisho, katika michango iliyotolewa na baadhi ya Wabunge, walitamka kwamba kuna nchi kadhaa duniani kama India, Bangladesh na sehemu nyingine zimefanikiwa kuanzisha na kusimamia na kuendesha *Community Banks successfully* vijijini. Basi ingekuwa ni jambo zuri wataalam wa Benki Kuu na Wizara ya Fedha, wafanye hima kwa kuwa tungependa huduma za Benki Vijijini, ziende haraka na muda hautusubiri, wateue tume ikatembelee nchi hizo na kujifunza jinsi wenzetu walivyofanikiwa katika kuanzisha Benki hizo, ili watakaporudi, kwa, kuzingatia mazingira yetu, waweze kuona kwa urahisi zaidi namna gani na sisi tunaweza tuka-*adopt relevant practices* zinazoweza kusaidia kuharakisha ufumbuzi wa uanzishaji, Usimamizi na uendeshaji wa Benki hizi.

Lingine dogo lakini nafikiri ni muhimu ni suala usimamizi wa fedha za *pension* za wastaafu. Kwa sababu Benki Kuu ina-*deal* na *monetary policy* pengine ilikuwa ni jambo la busara Serikali ikaangalia uwezekano wa kuwafanya Benki Kuu, wawe waratibu na washauri kwa mifuko ya pension katika masuala ya vitega uchumi na *investments.* Hii ni

kwa sababu zipo dalili zinazoonyesha kwamba mifuko ya pensheni sasa hivi ina fedha za kutosha, lakini naamini *investment propasals* ambazo zinafanyika sasa hivi nyingine zisingekuwa na *priority* inayostahili. Kwa maoni yangu ni vizuri ukifanyika upembuzi yakinifu, ili kuona kama isingekuwa wakati muafaka muafaka sasa kutumia baadhi fedha nyingi ambazo mifuko ya *pension* imehifadhi, kuongeza angalau kiasi kidogo fedha zinazolipwa kwa wastaafu. Fedha ambazo kwa sasa wanalipwa wastaafu ni kidogo mno, sehemu ya fedha inayobaki ndiyo iende kuwekezwa katika investments mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo naona ni la muhimu pia, ni kwa Benki Kuu kujifunza jinsi ambavyo Mheshimiwa Rais wetu alivyofanya. Najua majukumu yayooambatana na Miswada hii miwili ni makubwa sana na wengi tuna shauku yale yaliyomo yaanze kutekelezwa haraka. Basi ingekuwa ni jambo zuri Benki Kuu nao wakapata fursa ya kutafuta ka-Ngurdoto mahali fulani wakajitenga, wakajificha huko wataalam na waliobobea katika masuala mbalimbali wakawa kama *think tank* kwa muda wa siku kadhaa wakichanganua yote na mikakati iliyotolewa na Wabunge mbalimbali ili isaidie haraka kutekeleza majukumu yao vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yangu la mwisho ni suala la programu ya malengo ya shughuli muhimu za Benki Kuu. Waheshimiwa Wabunge, wengi wamezungumzia suala la riba na mfumko wa bei. Nafikiri ingekuwa ni jambo zuri kama katika mipangilio ya *plans* za Benki Kuu wangeandaa programu hata kama ni ya miaka mitatu mpaka mitano kipindi ambapo Ilani ya Uchaguzi kwa awamu hii itakuwa imekamilika, jinsi wanavyotegemea kutekeleza masuala haya yawe bayana, masuala kudhibiti mfumko wa bei, masuala ya plan ya kupunguza riba za Mabenki na kadhalika kwa ajili hii ili tuweze kuweka vigezo vya kupima mafanikio. Kwa kutumia *assumptions* fulani wanaweza kupanga programu hiyo na hatimaye baada ya kipindi fulani tunaweza tuka-*gauge* na kuona wame-*achieve* kitu gani kufuatana na *assumptions* ambazo walikuwa wameziandaa.

Mheshimiwa Spika, yangu kwa kweli yalikuwa ni hayo machache. Baada ya kusema hayo nasema naunga mkono hoja hii kwa nguvu zangu zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi nilikuwa katika Kamati. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii tena nichangie Muswada huu. Kabla ya yote nataka na mimi niongeze sauti yangu katika kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi yake nzuri aliyoifanya na kutupa moyo mkubwa kwa hizi siku 100 za Urais wake. *(Makofi)*

Kidole kimoja hakivunji chawa. Kwa hiyo, lazima tumsifu na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Edward N. Lowassa na Timu nzima ya Mawaziri na Watendaji Wakuu Serikalini kwa kazi waliyoifanya, kufika mahali ambapo kila mtu anasema kweli tumepata Rais. *(Makofi)*

Pili, naomba kama ilivyo ada, kumsifu, kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mama Zakia Meghji, Manaibu wake, Gavana na Timu yake kwa kutuletea Muswada huu. *(Makofi)*

Hakika huu Muswada ni ukombozi. Ukombozi kwa sababu tuko sisi tuliokuwa tunalia kila siku, lakini ukisoma ndani unakuta *Microfinance Company* na *Housing Finance Company.* Mambo haya angalau ya *housing,* ilikuwepo huko nyuma yakapotea. Sasa yanarudishwa tena. Huu ni ukombozi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ombi linaweza kutimizwa, nilikuwa naomba kwa heshima ya kilimo, kilimo nacho kingekuwa kinapewa jina haswa, Benki ya Kilimo. Inawezekana kabisa! Kama haiwezekani kwa sasa hivi na *CRDB* asili yake ilikuwa Benki ya Ushirika na mazao yenyewe yalikuwa ya kilimo, inaweza kufanywa mazungumzo, wanao uzoefu wa kukopesha wakulima wakapewa na Benki mtoto ili Benki hii iitwe *CRDB* Benki ya Kilimo au vinginevyo, lakini wakulima waweze kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *point* ya pili, huko zilikoanza Benki hizi liko suala la kukopesheka. Nao wamepata taabu sana, lakini wamefikia mahali huwezi kuweka Sheria ya Vyombo vya Fedha kwamba usikope mpaka uwe na *collateral,* uwe na rasilimali. Rasilimali ya mtu inaweza kuwa mali inayokamatika au bongo lake, yaani akili alizojaliwa na Mwenyezi Mungu inaweza kumpa nafasi ya kufanya kazi ya madaraka.

Basi hii nayo ingethaminiwa kama *collateral.* Wafanyakazi wengi wenye kazi ya kutosha inayofahamika, hawa Benki wangechukua dhamana ya kazi zao kama *collateral* na wangeweza kukopa na wakarudisha. Kama hawawezi kurudisha, inawezekana kabisa kufanya mahesabu kwamba hizo pensheni zao watakazolipwa, basi ule mkopo usidi zile pensheni kama una wasi wasi. Lakini wapate uwezo wa kukopa bila *collaterals*. Nadhani hili linaonekana geni lakini ni mtazamo ambao kwetu sisi hapa ni mpya. Lakini nani kakaa Uingereza? Nani kakaa Amerika, akaenda Benki kukopa akaambiwa lete hati ya nyumba, haiwezekani! Wazungu hawa siyo wengi wana nyumba, lakini wanakopa kila siku. Ni kwa sababu tu wana kazi na anuani, inatosha. Kwa sababu wanawajua wale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba jambo hili sio la mzaha. Ni hapa kwetu tu! Kwa nini tunataka kila mtu awe na nyumba? Inawezekana, lakini wazee wa Benki nyie, inawezekana hiyo?!! *(Makofi/Kicheko)*

Haiwezekani jamani kuwa nyumba. Sasa naomba mimi hili lifikiriwe kwa dhati yote kwamba watu wetu hawawezi kila mtu kujenga nyumba, kuleta *collateral* Benki. *(Makofi)*

Mimi nataka niisifu *CRDB* ilivyokubali kuwakopesha Wabunge kwa heshima ya kazi yao. Kwa hiyo, *CRDB* hongera. Maana yake wanajua kwamba baada ya miaka mitano, sisi tutalipa tu. Wafanyakazi wetu wengine katika Serikali au katika vyombo

vyote vinavyofanya kazi wanajulikana mishahara yao na pensheni mwishoni itakuwa ngapi? Hawa wakopeshwe. Hiyo ndiyo hoja yangu. *(Makofi)*

Tatu, naona hata haya, maana kila Mbunge hapa amesimama na kusema tafadhali punguzeni riba ya Benki ili watu wengi wakope. Nami naongeza sauti yangu hivyo hivyo, tafadhali tupunguze riba. Suala lingine inazungumzwa, tafadhali pelekeni huduma za Benki Vijijini kwa sababu huko ndiyo kwenye asilimia 80 ya watu. Hii ni haki na mimi naongeza sauti yangu hapo hapo. Tunazungumza juu ya *SACCOS* kusaidiwa kwa nguvu zote, halafu yanakuja tena maombi ya mikopo ya muda mrefu. Yaani haya maneno nilikuwa nateteta na mtu mmoja maarufu, nimesikiliza *speech* zote na zote zinazungumzia habari ya riba kwamba kupunguza riba.

Imezungumzwa habari ya kupeleka Mabenki Vijijini. Yaani habari ni zile zile. Mimi nadhani kwa kweli Mheshimiwa Gavana angeweza kuandika, yaani hata mistari mitatu tu inatosha, mambo Wabunge wanayoyataka ili Benki itufanyie. Kwa hiyo, hicho ni kilio maalum na kinarudiwa kwa maana ya kutia uzito kwamba jambo hili sasa lifike linakotaka kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijui ndiyo penyewe pa kusemea! Basi kama ni hapa ni hivi, kama tunataka ku-*create middle class,* yaani Waswahili ambao nao wananyanyuka katika biashara kungetakiwa kuwe na Sheria ya *Monopoly* kwa mfano wewe unakwenda Usukumani kule wanalima dengu. Haja yako uchukue mkopo Benki ununue dengu labda za Shilingi milioni 200 uzilete kwa *exporters* waipeleke ng'ambo kwa biashara. Au unakwenda Mtwara unanunua korosho, unaleta kwa *exporters* wanapeleka nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, kinyume chake unamkuta huyo *exporter* naye ana watu wake kule kule mnashindana. Sasa huyu bwana yeye kawa *registered exporter of commodities.* Leo anakwenda kule anaziba riziki ya *middle class* people ambao wanataka na wao waende wanunue waje kumuuzia na jambo hili linaturudisha nyuma sana hasa wafanyabiashara ambao hawajasimama sawasawa. Kwa kweli wenzetu hawa wana mipango mibaya sana. Ukionekana unakwenda kwenda kule unaweza kupata matatizo. Maana yake anataka yeye mwenyewe aende kule anunue halafu a-*create* bei zake huku akauze yeye tu. Hatuachii sisi twende kwanza Shinyanga kununua dengu tuje nayo Dar es Salaam tumuuzie, yeye ndiyo awe na kazi moja ya ku-*export*.

Nadhani hili kwa baadaye Serikali itabidi ilitazame kwa sababu Sheria ya *Monopoly* haitaanza hapa. Walijulikana hawa watu wa biashara wana tabia mbaya. Wakikuona unafanya biashara, basi yeye anataka kila kitu kiende kwake. Kwa hiyo, nadhani ukitaka kujenga *middle class* nzuri itakuwa jambo zuri sana kutilia mkazo kwamba waliojiandikisha katika *export business* wafanye *export business.* Mambo yetu sisi haya ya kukusanya ndizi, kahawa, watuachie sisi na sisi tupate chochote katika biashara ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kurudia tena kauli ile kule Rufiji, Mji wetu wa Utete uko kilomita 84 kufikia Benki. Watumishi wa Bomani wote wako pale, wafanya biashara wote wako pale, wanabeba fedha na Mbunge wao naye yuko pale. Tunafuata kilomita 84

kwenda kuweka hela na kutoa. Jambo hili Benki huwa haiwezi kujenga pale. Lakini kama nilivyosema katika Muswada uliopita nataka atakayeomba nafasi ya kufungua Benki, basi aambiwe apeleke Tawi moja kule Rufiji.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kurudia maneno ambayo kila mtu yanamghasi, kwa sababu maandishi mbali na matendo mbali. Sasa ninalotaka kuomba mimi haya maandishi tunayoyaruhusu katika Bunge hili na matendo yake yafanane. Nitaomba Mheshimiwa Gavana atuletee hapa Taarifa za utekelezaji, yaani kwa nini tumepoteza pumzi nyingi kuzungumza jambo hili. Basi faida yake tuione kwa maana ya utekelezaji wa haraka. *(Makofi)*

Sijui kama kuna *sanction* kwamba usipotekeleza tukufanye nini? Lakini nchi hii inatusikia. Tunamwomba Gavana, tunampa nguvu zote ili aweze kufanya kazi kwa haraka na itekelezwe kama ilivyo katika Muswada huu. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya, Mheshimiwa Spika, naomba kutamka kwamba naunga mkono hoja asilimia 100. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa orodha niliyokuwanayo na baada ya wengine kujitoa, naona wachangiaji wetu sasa tumemaliza. Kwa hiyo, mjadala umefungwa. Saa 11.00 nitamwita tu mtoa hoja tuendelee na zile taratibu nyingine. Kwa kuwa hakukuwa na utata mkubwa sana katika Muswada huu, naamini mtoa hoja naye atatumia muda mfupi tu kuweza kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge ambao takriban wote wamesema wanaunga mkono Muswada asilimia 100 na wengine zaidi hapo.

Sasa kuna matangazo machache. Kutakuwa na tukio la kuwatambua mashujaa wetu wanariadha, vijana wetu waliofanya vizuri kule *Melbourne* Australia mara baada ya Muswada huu kupitishwa. Naomba Waheshimiwa Wabunge wasiwe wamepumzika sana jioni. Tukae tuwe wengi kidogo maana yake tukio hili nalo ni la kuwahamasisha vijana wetu Watanzania Mikoa yote. *(Makofi)*

Sasa ikionekana baadhi ya viti ni vitupu, hakuna Wabunge inakuwa matatizo. Nitashukuru sana ikiwa Waheshimiwa Wabunge tutakaa kama tunavyokaa wakati wa Maswali ili tuwaenzi vijana wetu hawa. Niseme tu kwamba, itakuwa ni utamaduni wa Bunge hili kuwaenzi vijana katika fani mbalimbali. Isionekane kama vile tunawapendelea tu hawa wanariadha. Nadhani nchi yetu inahitaji kutambua mambo makubwa sana ambayo baadhi ya vijana wameyafanya ndani na nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Ilikuwa tuwe na fursa pia ya kuwatambua waliofanya vizuri katika mtihani wa *Form Four* lakini maandalizi hayakukaa vizuri na hilo halikuwezekana. Lakini siku za usoni tutafanya hivyo. *(Makofi)*

Ningependa tu kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba binti Wende aliyeongoza katika mtihani wa *Form Four* anatoka Wilaya ya Urambo. La tatu,

kutakuwa na hafla iliyoandaliwa na Gavana wa Benki Kuu mara baada ya kumaliza shughuli zetu hapa leo jioni. Ooh! Nashukuru sana, kwamba imeahirishwa. Karatasi ya mwisho nilipata kwamba bado ipo. Ahsante sana. Kwa hiyo, hiyo imeahirishwa. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11 jioni.

*(Saa 06.41 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia)*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006
### *(The Banking and Financial Institution Bill, 2006)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Sasa nitamwita mtoa hoja kwa sababu mjadala umekwishafungwa. Samahani Naibu Waziri kwanza anatangulia.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MUSTAPHA H. MKULO):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi ya Kilosa walionifikisha hapa, napenda kutoa mchango katika maeneo machache yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba riba za mikopo inayotolewa na Benki zetu kwa Dola za Marekani ni za chini ikilinganishwa na riba za mikopo inayotolewa kwa Shilingi za kitanzania. Kutokana na sababu zifuatazo:-

Sababu ya kwanza ni kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania mara kwa mara ikilinganishwa na Dola ya Marekani, ambapo kiwango cha ubadilishanaji wa Shilingi kwa Dola za Marekani, yaani *exchange rate risk* kinaongezeka na kufanya thamani ya Dola ya Marekani kuwa juu zaidi ukilinganisha na Shilingi ya Tanzania. Hali hii ya thamani hafifu ya Shilingi, yaani *exchange rate risk* ikilinganishwa na Dola za Marekani inasababisha riba ya mikopo inayotolewa kwa Dola za Marekani kuwa chini zaidi kuliko ile inayotolewa na Mabenki yetu kwa Shilingi ya Tanzania.

*Risk* na *interest rate risk* ya mikopo inayotolewa kwa Dola za Marekani na kurejeshwa kwa Dola za Kimarekani iko chini ikilinganishwa na ile mikopo inayotolewa kwa Shilingi za Kitanzania. Hata hivyo, tunapenda kuwashauri Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba ni vizuri kuchukua mkopo kwa Shilingi ya Tanzania kwa sababu haibadiliki. Ukichukua mkopo leo wa Dola millioni moja kwa Shilingi bilioni kumi baada ya mwaka mmoja unaanza kujikuta unalipa Shilingi bilioni 15 ambayo ni juu zaidi kuliko kama ungechukua kwa Shilingi.

Muswada unajielekeza vipi katika masuala ya mikopo ya nyumba. Serikali inakubaliana na hoja kwamba utaratibu wa wananchi kutumia fedha zao wenyewe kwa

ajili ya ujenzi wa nyumba unapingana na *best practices* katika masuala ya kiuchumi. Kwa kutambua hili, Serikali imewasilisha marekebisho ya Muswada huu katika kifungu cha 24 (n) na (o) ili kuruhusu Mabenki na Taasisi za Fedha kuanzisha Kampuni Tanzu zitakazojishughulisha na kutoa huduma mbalimbali za kibenki zikiwa ni pamoja na kutoa mikopo ya nyumba, yaani *mortgage finance.* Sambamba na hatua hii, mkakati wa awamu ya pili ya mageuzi katika Sekta ya Fedha, yaani *the second generation of financial sector reforms* unaosimamiwa na Benki Kuu, umeandaa utaratibu wa kutoa mikopo ya muda mrefu ikiwemo mikopo ya nyumba.

Tatu, *NMB* imewekeza asilimia 84 za amana za wateja katika dhamana na Serikali badala ya fedha hizo kuzikopesha kwa wananchi. Ni kweli kwamba *NMB* imekopesha asilimia 16 tu za amana za wateja na kuwekeza kiasi kikubwa katika dhamani za Serikali kwa sababu tangu kuanzishwa kwa *NMB* Benki hii imekuwa ikifanya kazi zake chini ya Mkataba wa makubaliano, yaani *memorandum of understanding* baina ya Serikali, Benki Kuu na *NMB*. Aidha, chini ya makubaliano haya, *NMB* ilipewa masharti na Benki Kuu kutojiingiza katika shughuli za kutoa mikopo, badala yake ijiandae kiutaalam kufanya shughuli za kuendeleza mikopo midogo midogo na wakati huo huo kujiandaa kubinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba *NMB* ilibinafsishwa mwaka 2005. Wakati inabinafsishwa *NMB* ilikuwa na mtaji wa Shilingi bilioni 61.8 ambao ulitokana na faida iliyozalishwa katika miaka ya 1999 hadi 2005. Kwa mtaji huo, *NMB* ndio Benki yenye mtaji mkubwa zaidi kuliko Benki zote za biashara hapa nchini. *NMB* kwa sasa ina matawi 108 ambayo yameboreshwa ili hadhi ilingane na Mabenki mengine hapa nchini. *NMB* inakusudia kufungua Matawi mapya 50 katika kipindi cha miaka mitano ijayo ili kusogeza huduma zake karibu na wananchi wengi na hasa wakulima Vijijini.

Mheshimiwa Spika, hisa za *NMB* zinamilikiwa kama ifuatavyo:- Serikali ya Tanzania ina hisa asilimia 51, *Arabo Bank* ya Uholanzi ina asilimia 34.9, NICO ina asilimia 6.6, *EXIM Bank* asilimia 5.8 na *TCCIA Investment Company* ina asilimia 1.7.

Mheshimiwa Spika, ifikapo Oktoba, 2006 yaani mwaka huu, Serikali inatarajia kuuza asilimia 21 ya hisa zake kwa Watanzania tu ikiwa ni pamoja na asilimia tano ambazo zimetengwa kuuzwa kwa wafanyakazi wa *NMB*.

Mheshimiwa Spika, wakati *NMB* hairuhusiwi kutoa mikopo, Serikali imewezesha *NMB* kuwa na thamani kubwa zaidi ya kuboresha fedha ambazo ziliwekezwa katika amana za Ofisi zake na pia kujiandaa kitaaluma. *NMB* kwa sasa inaruhusiwa kutoa huduma zote za kibenki ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo.

Nne, uanzishwaji wa Mabenki kwa ajili ya vikundi maalum, kwa mfano vijana wanawake na vikundi vingine, kama nilivyoeleza hapo awali kwamba awamu ya pili ya mkakati wa Benki Kuu wa mageuzi katika Sekta ya Fedha utaweka mazingira yatakayowawezesha wadau mbalimbali kuanzisha vyombo mbalimbali vya kifedha zikiwemo Benki za Maendeleo kwa ajili ya mikopo ya muda mrefu katika Sekta za

Kilimo, Viwanda, Ujenzi wa Nyumba na Uvuvi na Vikundi Maalum kwa mfano vijana na wanawake na Benki za kutoa mikopo midogo midogo.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyoahidi wakati wa kujadili Muswada wa Benki Kuu wa mwaka 2006, Serikali itaanda Mkutano wa wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Benki Kuu na Benki ya Biashara na wadau wengine ili kuangalia uwezekano wa Mabenki na vyombo vingine vya fedha, kupunguza riba za mikopo, kuboresha riba za amana na kupeleka huduma, na kupeleka huduma za kibenki karibu na wananchi Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa popote penye shughuli za uzalishaji huduma za kibenki zinasogezwa karibu na sehemu hizo ili wananchi wafaidike na mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini, yaani MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwako kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge. Pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walichangia katika hoja hii na mawazo ambayo waliyatoa. Kwa sababu utakubaliana nami kwamba hoja hii imeungwa mkono na Waheshimiwa Wabunge wote. Kwa hiyo, tunatoa shukrani.

Lakini zaidi, wamezungumzia juu ya mikakati kwamba ni mikakati gani na utekelezaji gani utumikie katika masuala yanaoonekana ni ya umuhimu kuhusiana na kupunguza kwa mfano riba, masuala ya kupeleka Sekta ya Fedha Vijijini, masuala ya kuhakikisha kwamba Sekta hii na Benki hizi zinafanya kazi katika kupunguza umaskini ili katika kutekeleza suala zima la MKUKUTA na MKURABITA. *(Makofi)*

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba Gavana wa *BoT* yuko hapa pamoja na Watendaji pamoja na sisi, tutahakikisha kwamba yale yote ambayo Waheshimiwa Wabunge wameyaeleza kwa nia njema kabisa tutayatekeleza hatua kwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwanza kwa majina na wale ambao walichangia kwa maandishi. Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge wa Handeni, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Pili, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed - Mbunge wa Wawi na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Willbrod Slaa, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Emmanuel Luhahula, Mheshimiwa Castor Ligallama, Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Charles Kajege, Mheshimiwa Adam Kigoma Malima, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba,

Mheshimiwa Phares Kabuye, Mheshimiwa Said Omar Arfi na Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Ibengwe Mongella. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Aziza Sleyum, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, Mheshimiwa Meryce Mussa Emmanuel, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Mheshimiwa Masolwa Masolwa, Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mheshimiwa Clemence Lyamba, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia na Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Naibu Waziri wa Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Mheshimiwa Khalifa Suleiman, Mheshimiwa Lucy F. Owenya na Mheshimiwa Fatma Mikidadi wa Viti Maalum. *(Makofi)*

Kama nilivyosema wakati ule, kama nimemsahau yeyote, naomba radhi lakini mnaweza kuniletea vikatarasi nikaweza kuwataja. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa kuunga mkono Muswada huu. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani kwa kuunga mkono Muswada huu.

Tunaahidi, kama nilivyosema kwamba Serikali itayafanyia kazi maelekezo na mawazo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi pamoja na Kambi ya Upinzani na Waheshimiwa Wabunge wote. Sasa nianze kujibu hoja mbalimbali kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza kabisa, kulikuwa na hoja ya *credit guarantee scheme* kwamba kutoa dhamana kwa *SACCOS* ili kuziwezesha kupata mikopo kutoka kwenye Mabenki kwa kuzingatia ukweli kwamba riba za mikopo zinazotolewa na Mabenki ni kubwa. Serikali inapenda kwa kuanzia kuwahimiza wanachama wa *SACCOS* zao na baadaye fedha hizo zitumike kuwakopesha wanachama. Kwa hiyo, kipindi hiki ni kwamba *SACCOS* lazima kuziimarisha. Fedha zaidi ziingie halafu ndipo mikopo ifanyike.

Mikopo ya aina hii mara nyingi inakuwa na riba ndogo ukilinganisha na riba itolewayo na Mabenki. Lakini pamoja na hili, Benki Kuu kama tulivyoeleza itaangalia suala zima la *credit guarantee* kwa ajili ya *SACCOS* na *SACCAS. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa mtaji wa Benki wa Shilingi bilioni tano na viwango vya mitaji ya Mabenki mengine. Kiwango cha mtaji kwamba kwa Mabenki cha Shilingi bilioni tano ni kwa ajili ya Mabenki makubwa ambayo kwa kweli shughuli zake zinahitaji kiwango kikubwa cha mtaji kama ambavyo ilipendekezwa kwenye Muswada. Wingi wa shughuli zinaweza kufanywa na Benki na Taasisi ya Tedha inakuwa sawa sawa na kiwango cha mtaji wake. Huo ndio msingi wa upangaji wa viwango vya mtaji kwa Benki na Taasisi za Fedha. Kwa kuwa Benki za Mikoani au Wilayani na Ushirika na Taasisi ndogo ndogo Mijini na Vijijini shughuli zake ni chache, viwango vya mtaji kwa maana hiyo ni vidogo kuliko vile vya Benki kubwa.

Viwango vya mtaji kwa Benki na Taasisi ni kama ifuatavyo:- Benki kubwa kitaifa ni Shilingi bilioni moja, Taasisi za fedha kubwa kitaifa ni Shilingi milioni mia tano, Benki au Taasisi za Fedha ndogo ndogo ambazo ziko kwenye Makao ya Mkoa na Wilaya ni kati ya Shilingi milioni hamsini na Shilingi milioni 200. Kwa hiyo, ukiangalia Muswada huu unaona kwamba Muswada huu unaipa Benki Kuu mamlaka ya kuweka viwango vya mitaji kwa Benki ndogo ndogo za Kimkoa, Kiwilaya na za Ushirika ambavyo vitazingatia hali halisi za Benki na Taasisi hizo na viwango vya mtaji vitakavyotoa uwezo wa kutosha kwa Benki na Taasisi hizo kutimiza majukumu yake. Kwa hiyo, kwenye Muswada, inaelezea juu ya *categorization* kwamba zile ambazo ni ndogo na shughuli zake ni ndogo, kwa hiyo mtaji wake utakuwa ni mdogo.

Serikali inapendekeza kuendelea na utaratibu huu ili kutoa nafasi kwa Benki Kuu kama msimamizi wa Mabenki kupanga viwango vya mtaji kwa Benki na Taasisi ndogo ndogo ili viende na wakati na kukidhi mahitaji ya wananchi. Suala lingine lilikuwa tatizo la Mabenki kutokukubali malipo kwa njia ya hundi. Tatizo la Mabenki kutokukubali malipo kwa njia ya hundi linachangiwa zaidi kwa kiasi kikubwa na sababu zifuatazo:-

Kwanza kabisa, wananchi kutokuwa na vitambulisho vya kitaifa ambavyo vinamtambulisha mlipaji kwa Mabenki haya. Pili, matumizi ya fedha tasilimu kama njia ya malipo. Tatu, tatizo la baadhi ya walipaji kutokuwa waaminifu na kwa maana hiyo kutoa hundi hewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo haya, Benki nchini zimebuni njia mbalimbali mbadala za malipo ikiwa ni pamoja na matumizi ya mashine maalum ya kuchukulia fedha *ATM, Credit Card* na *Dept Cards.* Lakini nafikiri suala lile ambalo tunazungumza, suala la vitambulisho, litasaidia sana kuondoa tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba Muswada unalenga zaidi kwenye udhibiti kuliko uwekezaji. Ni kweli kwamba Muswada unalenga zaidi katika udhibiti wa Mabenki na Taasisi za Fedha kwa kuwa lengo ni kuweka mfumo madhubuti wa udhibiti wa shughuli za Mabenki na Taasisi za Fedha. Katika mfumo huu, jukumu la Benki Kuu ni kusimamia na pia kudhibiti shughuli za Mabenki na Taasisi za Tedha ili kuweza kulinda fedha za wananchi. Benki kuu itatoa leseni kusimamia shughuli na kusimamia uendeshaji wa ufilisi wa Mabenki na Taasisi za fedha. Hata hivyo, ukiuangalia huu Muswada unalenga pia katika uwezeshaji na pamoja na hayo maelezo mbalimbali na michango mbalimbali ambayo Waheshimiwa Wabunge wameweza kuyatoa.

Labda nitoe mifano michache ya jinsi tunavyoona Muswada unavyotambua uwezeshaji. Muswada unatoa fursa ya kuanzishwa kwa Mabenki yatakayotoa huduma za mikopo midogo midogo, yaani *Microfinance,* mikopo ya ujenzi wa nyumba yaani *mortgage finance* na ukodishaji wa mitambo na vitendea kazi, yaani *lease finance*. Huduma hizi zote zinalenga kukidhi matakwa ya sasa ya uchumi hususan uwezeshaji wa Mabenki na Taasisi za Fedha kutoa huduma hizo.

Muswada huu pia unatoa mamlaka kwa Benki Kuu kuweza kuweka viwango vya mitaji kwa Taasisi za Fedha kama vile nilivyoeleza na kwa maana hiyo, kuziwezesha

Taasisi ndogo za Fedha kuanzishwa Vijijini na Mijini kwa maana *Community Banks* na *Microfinance Institutions*. Aidha, Mkakati wa Urekebishaji wa Sekta ya Fedha kama tulivyoeleza, yaani *Second Generation Financial Sector Reforms* unalenga kuwawezesha wananchi kupata huduma zaidi kutoka Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, Suala lingine lilikuwa juu ya Mabenki kutoa huduma za kibenki kwa kutumia magari yaani *Mobile Banks.* Serikali inakubaliana kimsingi na wazo zuri kuhusu Mabenki kutoa huduma za kibenki kwa kutumia magari ili kuwezesha huduma hii muhimu kuwafikia wananchi.

Kwa kutambua umuhimu huu, Serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu itafanya mashauriano na Benki na wadau wengine vikiwemo vyombo vya usalama kwa lengo la kuhakikisha huduma hii muhimu inawafikia wananchi hasa wale wa Vijijini, wakati huo huo kuhakikisha usalama wa huduma hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni juu ya je, noti za Dola ya Kimarekani yenye sura ya Rais George Washington yenye kichwa kidogo, je, kichwa kidogo ni halali? Kuna taarifa kwamba baadhi ya Mabenki na *Bureau de Change* zinakataa kupokea noti za Dola za Kimarekani zenye sura ya George Washington kufuatia nia ya Serikali ya Marekani kuziondoa noti hizo katika mzunguko. Serikali inapenda kuwahakikishia wananchi kwamba noti hizo kwa hivi sasa bado ni halali kwa matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa inahusu Mabenki kuanzisha matawi nje ya nchi kwamba je, Benki Kuu itadhibiti masuala ya fedha haramu *(money laundry)?* Muswada unatoa mamlaka kwa Benki Kuu kutathmini na pale itakapoona inafaa kutoa idhini kwa Mabenki nchini kuwa na Matawi na Ofisi nje ya nchi baada ya kufanya tathimini kama vile ambavyo baadhi ya Benki zenye Makao yake Makuu nje ya Tanzania zilivyoanzisha Matawi yao na Ofisi hapa nchini. Kwa hiyo, kuna Benki za nje nazo pia zimeanzisha Matawi yake hapa nchini.

Aidha, Benki Kuu hushirikiana na wasimamizi wa Mabenki *(regulators)* waliopo nje ya nchi kwa lengo la kuhakikisha kwamba Benki hizi zinafuata Sheria na taratibu zilizopo katika nchi ambapo Benki husika hutoa huduma zake. Vile vile, taratibu za kibenki zinaruhusu Wasimamizi wa Mabenki kupeana taarifa za ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa fedha haramu, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Benki Kuu ilitoa waraka Na.8 wa udhibiti wa fedha haramu kwa Mabenki, yaani *money laundering contro*l *circular No. 8 of 2000.* Waraka huu unaelekeza Mabenki na Taasisi za Fedha kuhusu umuhimu wa kutambua wateja wao, yaani lazima uwajue. *Know your customers* na kutambua shughuli zinazoweza kuashiria kuwepo kwa fedha haramu ambapo Benki yoyote itakapotilia mashaka kuwepo kwa fedha haramu inapaswa kutoa taarifa mara moja kwenye vyombo vya usalama na pia Benki Kuu.

Vile vile, Waheshimiwa Wabunge, Serikali inaandaa utaratibu wa kuwasilisha Bungeni Muswada wa Udhibiti wa Fedha Haramu kwa Taasisi Mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine lilikuwa je, Muswada huu unajielekeza vipi katika kushughulikia *SACCOS* na *SACCAS?* Nafikiri hili nimelijibu nilipokuwa naeleza mwanzoni.

Suala lingine ni kwamba kifungu cha 6(2) cha muswada kitamke bayana kiwango cha chini cha faini atakayotozwa mtu atakayepatikana na hatia ya kuendesha shughuli za kibenki bila ya leseni. Kwa kuwa kifungu hiki cha Muswada kimetumia maneno adhabu ya faini isiyozidi milioni ishirini, Serikali inapendekeza kifungu hiki cha Sheria kibakie kama kilivyo ili kutoa uhuru kwa Mahakama kutoa adhabu kulingana na uzito wa kosa husika. Aidha, maneno kama haya yanatumika pia katika Sheria mbalimbali.

Hoja nyingine ilikuwa ni juu ya kutafsiri Sheria ya Mabenki katika lugha ya Kiswahili. Serikali inakubaliana na hoja ya Waheshimiwa Wabunge kwamba kutokana na umuhimu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha kwa wananchi, ni vyema Sheria hii ikatafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ili iweze kueleweka vizuri kwa wananchi wa kawaida. Utaratibu wa kutafsiri Sheria kwa lugha ya Kiswahili sio dhana ngeni, wakati tukiandaa tafsiri hii Benki Kuu itaandaa vijarida na vipeperushi kwa lugha ya Kiswahili vitakavyoelezea maeneo muhimu ya Muswada kwa manufaa ya wananchi. *(Makofi)*

Hoja nyingine ni juu ya ufafanuzi wa maneno *"Banking Business"* na *Core-capital.* Serikali inapendekeza maneno *"Banking Business"* yabakie kama yalivyo katika Muswada. Kwa sababu tafsiri hii inatosheleza matakwa ya huduma za kibenki za kisasa ambazo hazihusishi uchukuaji wa amana tu kutoka kwa umma. Huduma kama mikopo ya muda mrefu, yaani *development financing*, mikopo ya ujenzi wa nyumba yaani *mortgage financing,* ukodishaji wa mitambo na vitendea kazi, yaani *lease financing* na *investment Banking* zinaweza kutolewa bila kuhusisha uchukuaji wa amana kutoka kwa umma. Ufafanuzi wa maneno haya kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada kwa kweli ni mpana na unazingatia dhana inayojumuisha huduma za kibenki zaidi ya uchukuaji amana kutoka kwa umma kama vile ilivyoainishwa chini ya awamu ya pili ya mageuzi ya Sekta ya Fedha, yaani *second generation of financial sector reform. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tafsiri ya maneno "Core-capital", Serikali inakubaliana na hoja kwamba maneno *"common stock*" yana maana sawasawa na *ordinary shares* ambayo kwa pamoja yametumika katika Muswada. Hivyo marekebisho yamefanyika kwenye Muswada kwa kuondoa maneno *"common stock."*

Hoja nyingine ilikuwa maombi ya *Bukombe Community Bank Limited.* Benki Kuu ilipokea maombi ya *Bukombe Community Bank* tarehe 24 Novemba, 2004 na maombi hayo yalijibiwa tarehe 4 Januari, 2005 ambapo Benki Kuu ya Tanzania ilitoa masharti yanayopaswa kutimizwa na Benki hii kisheria. Masharti hayo ni pamoja na kuonyesha mtaji wa Benki, Wakurugenzi wa Bodi, Maafisa Waandamizi wa Benki na masuala mengine yanayohusu usajili wa Benki.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo *Bukombe Community Bank* hadi sasa haijawasilisha maelezo waliyopewa na Benki Kuu licha ya barua ya Benki Kuu ya tarehe

01 Aprili, 2005 ya kukumbushia suala hili. Ningemwomba Mheshimiwa Mbunge labda baadaye anaweza kuonana na watu wa Benki Kuu ili kuweza kumaliza suala hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba, ni wananchi wangapi wamefaidika na mikopo ya Benki? Hadi kufika Januari, 2006 idadi ya wananchi, Kampuni na vikundi vilivyofaidika na huduma za Benki na Taasisi za Fedha, ni takribani milioni mbili. Hata hivyo, idadi hii haijumuishi wananchi, Makampuni na vikundi vinavyopata huduma nyinginezo za kibenki zisizo za uwekaji wa amana za kukopa kwa mfano *money transfer safe custody services* na kadhalika. Hii *figure* niliyoitoa ni wale ambao wanaweka *deposit* yao Benki.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa Benki Kuu kuwa na Wakaguzi wa Benki wenye ujuzi na utaalamu wa kutosha. Serikali inakubaliana na ushauri wa Wabunge kuwa na Wakaguzi wa Mabenki wenye ujuzi na utaalamu ili kwenda sambamba na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia. Serikali inapenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Benki Kuu ya Tanzania inao wataalamu wenye sifa na ujuzi wa kutosha katika ukaguzi wa Mabenki. Aidha, Benki Kuu imekuwa ikitoa mafunzo ya mara kwa mara ya ndani na pia ya nje ya nchi kwa wataalamu na pia kuweza kubadilishana utaalamu wa Mabenki na nchi mbalimbali kwa mfano nchi jirani ya Kenya.

Hoja nyingine ni kufanyia marekebisho kifungu cha 41 kuhusu uteuzi wa Mfilisi wa Benki. Malengo ya msingi ya usimamizi wa shughuli za Mabenki na Taasisi za Fedha ni kuhakikisha kwamba Sekta ya Fedha ni salama ili kupunguza uwezekano wa wenye amana kupoteza fedha zao. Kifungu cha 41 kwa Muswada kuhusu uteuzi wa Mfilisi kama ilivyopendekezwa kwenye Muswada, kinakwenda sambamba na malengo haya ya kimsingi. Madhumuni ya kifungu hiki ni kuweka utaratibu ulio tofauti na ule ulioainishwa kwenye Sheria ya Makampuni kwa sababu utaratibu huu huchukua muda mrefu na hivyo kuweza kuhatarisha usalama wa fedha za wenye amana katika Benki itakayothibitishwa na Benki Kuu kuwa imefilisika.

Hoja nyingine ni kufanyia marekebisho kifungo cha 61(3), kwa kuwa Sheria hii inatumika pande zote mbili za Muungano. Muswada umefanyiwa marekebisho katika kifungu cha 61(3) kujumuisha Sheria ya Makampuni ya Zanzibar yaani *Companies Decree.*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kwamba Serikali iwezeshe maskini kukopesheka. Kama tulivyosema kwamba Serikali inakubaliana na dhana hii na kwamba tutafanya Kikao pamoja na Mabenki mbalimbali ili kuhakikisha kwamba suala hili linatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nasema tena kwamba napenda kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, mawazo yao tunayachukua kwa uzito ili kuweza kutekeleza katika kufanikisha Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha wa Mwaka 2006**
***(The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii kwa kuzingatia utaratibu wetu tunapokuwa na Muswada ambao unakuwa na vifungu vingi sana, basi natumia mamlaka mliyonipa chini ya Kanuni ya 72(3) kwamba tuupitie Muswada huu kwa sehemu badala ya kifungu kimoja kimoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Kifedha wa Mwaka 2006**
***(The Banking and Financial Institutions Bill, 2006)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Kifungu Kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 7

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17
Ibara ya 18

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 24

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31
Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45
Ibara ya 46
Ibara ya 47

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 48

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 49
Ibara ya 50

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 51

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 52
Ibara ya 53

Ibara ya 54
Ibara ya 55
Ibara ya 56

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 57
Ibara ya 58
Ibara ya 59

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 60

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63
Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68
Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara ya 71
Ibara ya 72

*(Ibara zilivyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha wa Mwaka 2006**
***(The Bank and Financial Institution Bill, 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha, yaani *The Banking and Financial Institutions Act 2006,* sehemu kwa sehemu na kukubali pamoja na marekebisho yake. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolwa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**BUNGE KUWATAMBUA NA KUWAENZI WATANZANIA WALIOFANYA VIZURI KWENYE MAADHIMISHO YA KIMATAIFA YA *COMMONWEALTH OLYMPIC GAMES***

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowatangazia katika Kikao chetu asubuhi, tuliamua kwamba ni utamaduni mzuri kuwaenzi vijana wetu Watanzania pale wanapofanya vyema katika jambo lolote ambalo lina maslahi kwa nchi yetu. Leo tunawatambua wanaohusika na kutupa ushindi kule kwenye michezo ya riadha kule Melbon Australia, michezo ya Jumuiya ya Madola. Lakini narejea nilichokisema asubuhi kwa sababu wengine hamkuwapo.

Itakuwa ni utamaduni wa Bunge letu kuzitambua juhudi mbalimbali za Watanzania katika fani mbalimbali, na huu ni mwanzo tu, kwa hiyo, sio vizuri tukawa tunaacha vijana wetu ama watu wengine, watu wazima wamefanya mambo makubwa yawe katika sanaa, elimu, uvumbuzi na hata sitashangaa kama tutakuja kuenzi Halmashauri ya Wilaya ambayo imefanya vizuri sana katika malengo ambayo yamechangiwa. *(Makofi)*

Sasa, kwa kuwa katika kuwatambua inabidi wageni hawa waingie Bungeni, basi sasa nitamwomba Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu atoe hoja ya kutengua kanuni husika ili wageni waweze kuingia humu Ukumbini. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Karibu.

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI YA 114(1)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu na kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (1) naomba kutoa hoja kwamba wananchi wafuatao, Koplo Samson Ramadhan Nyoni na Ndugu Phabian Joseph Naasi waruhusiwe kuingia na kukaa ndani ya Bunge. Kwa historia ya Bunge hili ni viongozi wa Kitaifa tu, Marais Wastaafu, Mawaziri Wakuu wastaafu na Majaji peke yake wamewahi kuombewa na kuruhusiwa kuingia na kuketi Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi hawa wameliletea heshima kubwa Taifa letu katika medani ya michezo, hivyo naomba kutoa hoja kwamba wananchi hawa wawili waruhusiwe kuingia na kukaa Bungeni jioni hii hadi utakapoahirisha Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuilwa na kuafikiwa)*

*(Hapa Wageni Waalikwa Waliingia Ukumbini)*

**SPIKA:** Sasa nitamwomba *Sergeant At Arms* awaonyeshe sehemu ya kuketi.

*(Hapa Wageni Waalikwa waliketi katika Jukwaa la Spika)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, aliyekaribu yangu kabisa sio mwingine, ndiye Koplo Samson Ramadhan Nyoni, mshindi wa Medali ya Dhahabu katika michezo ya *Olympic.* Anayemfuata ndiye Ndugu Nasi ambaye ni mshindi wa Medali ya Shaba kule Melbon. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu tutakuwa na hoja ya kuwatambua rasmi, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Habari aweze kuwasilisha hoja ya Bunge. Kabla Mheshimiwa Waziri hujafanya hivyo, nilipenda Waheshimiwa Wabunge tutambue kuwepo kwa mkewe Koplo Nyoni, yupo kwenye *Speakers Gallery* amesima na mtoto wao. *(Makofi)*

*(Hapa Mke wa Koplo Nyonyi alisimama na kuonekana)*

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mtoto wao anaitwa Museven. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika; Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waheshimiwa Wabunge: Naomba kutoa hoja kwamba kwa idhini yako, Bunge lako sasa liwatambue na kuwaenzi Watanzania wenzetu waliofanya vizuri kwenye mashindano ya Kimataifa ya Jumuiya ya

Madola yaliyofanyika huko Austria hivi karibuni. Uamuzi wenu Waheshimiwa Wabunge wa kuwatambua na kuwaenzi wapendwa wetu Koplo Samson Ramadhan wa Jeshi la Wananchi Tanzania na Ndugu Phabian Joseph ni kitendo kilichowapa heshima na hadhi siyo wanamichezo hawa tu, bali ni kielelezo cha kuwaheshimu na kuwatukuza Watanzania wote hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamusi ya Kiswahili Sanifu ukurasa wa 73 imetafsiri neno "enzi" kama ifuatavyo:-

"Onyesha heshima au mapenzi au pendo, weka mtu kwenye nafasi ya heshima au utukufu." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Naam kweli Bunge letu Tukufu kwa niaba ya Watanzania wote leo limeonyesha heshima, mapenzi na huba kwa Wanariadha wetu hawa na kualikwa kwao hapa Bungeni rasmi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwepo kwao humu Bungeni kwa ruhusa yako, wanariadha hawa wamewekwa katika nafasi ya kuvishwa heshima, huba na utukufu na Taifa letu hili. Kwa niaba ya wananchi na wapenzi wa michezo nchini, nashukuru sana Bunge lako Tukufu kwa kutupa heshima hii Wanamichezo wa hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na Bunge lako Tukufu kufuatilia matokeo ya mashindano haya, napenda kuelezea kuwa Tanzania imeweza kupata Medali ya Dhahabu na ya Shaba. Mchezaji wa mbio ndefu za Marathon Koplo Samson Ramadhan ameipa Tanzania Medali ya Dhahabu baada ya kushinda mbio hizo kwa kushika nafasi ya kwanza baada ya kutumia saa 1:11.29 kwa kukimbia kilomita 42.2. *(Makofi)*

Mchezaji mwingine ni Joseph Phabian wa *Club* ya *Team* ya Max ya Arusha. Alishiriki katika mbio za mita 10,000 na kushika nafsi ya tatu baada ya kutumia muda wa dakika 27.51 na kuipatia nchi yake Medali ya Shaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi wa vijana hawa haukupatikana kwa miujiza, ni jitihada zao binafsi, nidhamu, kujituma, ustadi wa Walimu wao na pia mchango wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza Chama cha Riadha Nchini kwa juhudi zake za kueneza michezo na Wanariadha hawa kuweza kuipatia nchi yetu heshima kwa ushindi huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuelezea historia fupi ya mashujaa hawa wawili. Kwanza, nianze kwa Joseph Phabian aliyeiletea nchi yetu Medali ya Shaba. Ndugu Joseph Phabian alizaliwa tarehe 24 Desemba, 1975 Babati Arusha, anasoma Shule ya Michezo Arusha *Academy.* Baadhi ya mashindano aliyoshiriki ni kama ifuatavyo:-

Mwaka 2003 alishiriki mashindano ya dunia ya nusu Marathon yaliyofanyika Ureno ambapo alipata Medali ya Fedha. *(Makofi)*

Mwaka 2004 alishiriki mashindano ya dunia ya nusu Marathon yaliyofanyika India na alipata Medali ya Fedha. *(Makofi)*

Mwaka 2004 alishiriki katika mashindano ya dunia ya Marathon, huyu kijana alipata tena medali ya Fedha. *(Makofi)*

Mwaka 2005 alishiriki mashindano ya dunia ya nusu Marathon yaliyofanyika Edenton Kanada na kupata Medali ya Dhahabu. *(Makofi)*

Mwaka 2005 alishiriki mashindano ya dunia ya nusu Marathon yaliyofanyika Ufaransa, alishiriki pia mashindano ya NYIKA yaliyofanyika Spain, mashindano mengine yaliyofanyika *Classic* Marekani na mwaka huu ameshiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola yaliyofanyika Melbourne Austraria na amerudi na Medali ya Shaba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huo ni wasifu mdogo wa Ndugu Phabian. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikirejea kwa mwanamichezo Samson Ramadhan Nyoni, yeye ana wasifu ufuatao:-

Alizaliwa tarehe 24/12/82 Kijiji cha Kisaki Singida Mjini. Alihitimu Elimu ya Msingi ya Darasa la Saba mwaka 1995 katika Shule ya Msingi ya Mankonko Singida Mjini.

Ameajiriwa na Jeshi la Wananchi Tanzania mwaka 1998. Baadhi ya mashindano aliyoshiriki ni kama yafuatayo:-

Mwaka 2003 alishiriki mashindano ya *DEPEN Oppten Marathon* Japan akatokea wa kwanza. Mwaka 2003 London alishiriki mashindano ya *Land Marathon* alitokea wa tano, lakini pia alishika nafasi ile ile ya *record* ya Nkangaa. Kwa hiyo, alishika nafasi ya *record* ya Nkangaa. *(Kicheko/Makofi)*

Mwaka huo *Ufaransa World Champion Marathon* alitokea wa 15; Mwaka 2004 Korea Dunka Marathon, Marathon alishika nafasi ya saba na katika mwaka huo huo pia alishiriki Janga Marathon akawa mtu wa 13. *(Makofi)*

Mwaka 2004 pia alishiriki katika mashindano ya Greece Olympic akawa mtu wa 38. *(Makofi)*

Mwaka 2005 alishiriki mashindano ya Marathon yaliyofanyika Moshi Kilimanjaro kilomita tano, akawa mtu wa Saba; Alishiriki tena kule Helsinki katika mbio za Marathon tena akachukua nafasi ya tano na Moshi Kilimanjaro, nusu Marathon mtu wa tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka huu huko Austria Jumuiya ya Madola Ndugu Samson Ramadhani Nyoni alikuwa mtu wa kwanza na kuchukua dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania imekuwa ikishiriki katika mashindano ya Madola toka zamani, sana lakini kati ya mwaka 1974 na 2006 tumekuwa tukipata Medali za Dhahabu kadha wa kadha. Mfano, mwaka 1974 Philbert Bayi alikimbia mita 1500 na kushinda dhahabu; Mwaka 1982 Bwana Shahanga mita 10,000 akapata dhahabu; Mwaka 1998 kule Kuala Lumpa Bwana Michael Yombayomba mtu wa kwanza, naye alipata dhahabu. *(Makofi)*

Mwaka 1998 pia mita 10,000 Ndugu Naali alipata dhahabu na mwaka huu Marathon Samson Nyonyi kapata dhahabu. Hii inaonyesha kwamba ni kiasi gani tunajitahidi kushindana katika mashindano mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, zipo sababu nyingi zilizowafanya Wanariadha wetu tuwape leo heshima hii inayostahili. Wao ndio washiriki huko Austria na kulitangaza jina la nchi yetu kwa niaba yetu sote, hivyo walipeperusha Bendera yetu ya Tanzania huko Austria.

Idadi ya nchi zilizoshiriki zilikuwa 71 na sisi katika mashindano hayo makali sana tumechukua nafasi ya 20, sio haba. Ziko nchi nyingine zilipeleka washiriki hata 600 ambazo nafasi zao za kupata medali nyingi ilikuwa kubwa ukilinganisha na sisi kupeleka watu 21 tu.

Tukubali pia kwamba taaluma ya Sayansi ya Michezo, kwetu iko nyuma na uchumi wetu siyo mkubwa hasa pale inapoonyesha maendeleo ya kisayansi na uchumi wa nchi kama Australia, Canada, Uingereza na India ambao ndiyo walichukua medali nyingi zaidi. *(Makofi)*

Hivyo basi, ushindi wetu wa Medali hizi, ni nafasi ya watu 20 kati ya 71. Ni ushindi wa kujivunia! Tumeshinda kwa ari ya uzalendo! Naomba tujipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushindi wetu na kujivunia tusione aibu katika muktadha huu kwani wapo wanamichezo wengine wameshiriki huko Austria mwaka huu bila kupata medali, lakini walituwakilisha vyema huko Australia na ninaomba pia nao tuwapongeze. *(Makofi)*

Hata hivyo, wanariadha wafuatao ingawa hawakupata medali lakini waliweza kuzivunja medali zao wenyewe huko Austria. Wa kwanza ni Damian Chop; wa pili ni Jackson Marowa na wa tatu ni Binti Josephine Dumi. Wote hawa ninawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika baada ya kutoa wasifu wa mashujaa wetu ni vyema ieleweke kuwa Serikali itaendeleza michezo nchini kwa nguvu zote. Serikali ya Awamu ya Nne imedhamiria kwa dhati kuinua michezo na viwango vya michezo katika medani ya Kimataifa. Aidha, wakati Mheshimiwa Rais Kikwete akihutubia Bunge Dodoma hapa

mwaka jana 2005 alisisitiza dhamira yake ya kusaidia Sekta ya  Michezo kwa kusema yafuatayo, nami namkariri:-

"Tutafanya jitihada ya kuwezesha Vyama vya Michezo ili Tanzania iweze kushiriki vizuri na isiwe msindikizaji katika mashindano makubwa ya michezo ya Ulimwengu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wale waliowapongeza na kuwapa zawadi mbalimbali mashujaa wetu hawa.  Hata hivyo, napenda kutoa shukrani maalum kwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Waitara kwa kumtunuku Cheo cha Ukoplo Mwanariadha Samson Ramadhan kutokana na heshima hiyo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Pia namshukuru sana Mkuu wa Majeshi kwa kuwapa usafiri leo asubuhi wa ndege ya Jeshi kuwaleta hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba sasa hivi Tanzania inakabiliwa na michezo mitatu mikubwa.  Michezo hiyo ni Michezo ya *Africa Games,* michezo ya *Olympic* na michezo ya Jumuiya ya Madola.  Tunadhamiria katika miaka mitatu hii au minne, tujitahidi tupate medali zaidi katika michezo hiyo inayofuata.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba nimshukuru Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Akukweti, yeye ndiye aliyewapa Bendera wale vijana waliokwenda kule Austria.  Mimi najua kwamba Mheshimiwa Akukweti ni Sharif, kwa hiyo aliwapa baraka na wakashinda. Lakini aliwaambia ninyi Watanzania mna mikono ya kupigana ngumi kama Wazungu, basi wachapeni.  Ninyi Watanzania mna miguu ya kukimbia kama Wazungu, hivyo basi wapiteni na kweli wametekeleza, bahati mbaya ngumi hazikuwapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Watanzania wengine kutosita kuwapongeza na kuwatunuku zawadi kwa heshima na fadhila walizotufanyia vijana wetu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba aliposema yule mtoto anaitwa Museven, sio utani.  Jina lake kweli ni Museven. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri sasa ...

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:**  Mheshimiwa Spika, samahani, mwongozo wa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Utaratibu kifungu gani?

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Kifungu cha 43

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Kanuni ndogo ya 1 kuhusu hoja zinazotolewa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwa idhini yako tujadili *issue* hii iwe kama hoja kutokana na kifungu hiki ambacho kinasema kwamba, nitasoma kama kilivyoandikwa:"Isipokuwa kama Kanuni hizi zimeagiza vinginevyo, hakuna mjadala wowote utakaoendeshwa Bungeni ila tu kuhusu shughuli iliyoingizwa katika kitabu cha shughuli za Bunge na kuwekwa kwenye orodha ya shughuli."

Kwa hiyo, kwa sababu shughuli hii tuliwekewa toka asubuhi katika zile orodha za shughuli ambazo zitafanyika leo ikiwa ni pamoja na maswali, Muswada, pamoja na shughuli hii ya kuwatambua wanariadha hawa ambao wamefanya vizuri katika michezo ya *Olympic,* basi ningeomba kwa idhini yako, Bunge hili lijadili hoja hii na tuizungumzie vizuri kwa ajili ya kuwapa moyo hawa na vijana wengine wote wa Tanzania katika kufanikisha michezo yetu isonge mbele.

Mheshimiwa Spika, naomba Kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, umefanya papara tu. Huko ndiko tunakokwenda sasa. Wewe umetangulia, lakini sio mbaya maana yake ni kama Waswahili wanasema umeongezea asali kwenye mseto. *(Kicheko)*

Kwa hiyo, natambua wapo Waheshimiwa Wabunge walikwishaniletea taarifa kwamba wangependa kusema machache kuwapa moyo hawa vijana na hoja ya namna hii haiwezi kwisha kavukavu tu baada ya kutolewa na Serikali. Kwa hiyo, nitaanza na wewe Mheshimiwa Amina. *(Kicheko)*

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa Msemaji wa kwanza katika hoja hii ya kuwapongeza wanamichezo hawa wanariadha ambao wamefanya vizuri.

**SPIKA:** Dakika zisizidi tano.

**MHE. AMINA CHIFUPA MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Mimi binafsi nikiwa kama Mbunge wa Viti Maalum (Vijana Taifa) nimefurahishwa sana na kitendo kikubwa, naweza nikasema ni tukio kubwa kabisa la vijana hawa kurudi nchini kwetu wakiwa na medali mbili za dhahabu pamoja na shaba ukizingatia michezo hii ilikuwa imejumuisha wanamichezo kutoka katika nchi mbalimbali duniani.

Hii ni heshima kubwa sana ambayo nchi ya Tanzania imepata nadhani pia ni changamoto kwa vijana wengine wa Tanzania katika maeneo mbalimbali ya michezo ukiwemo mchezo wa mpira wa miguu hasa timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu, nayo nadhani iige mfano mzuri kutoka kwa vijana hawa, kwani siku zote tumekuwa tukisema Tanzania katika michezo ni kichwa cha mwendawazimu, lakini kama tutaendelea hivi kama ambavyo hawa wameonyesha mfano, basi tutafika mbali sana kimichezo.

Hii ni changamoto katika Sekta nzima ya Michezo ambayo imeonyeshwa na vijana hawa wawili. Kwa hiyo, mimi kwa niaba ya Wabunge wote wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ningependa kuwapongeza kwa dhati kabisa ya moyo wangu na ninawatakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jinsi ambavyo Mheshimiwa Waziri amekuwa akisoma yale maelezo ya utangulizi pale, imeonyesha kwamba hii sio kazi ya siku moja, waliifanya kwa muda mrefu sana. Kwani ametupa historia fupi ambayo imeonyesha michezo mbalimbali waliyoshiriki na pia wamefanya vizuri. Tunaomba iwe changamoto wao wawe kama ni mwongozo, watoe elimu ya kutosha pia kwa vijana wengine. Kama mtapata nafasi mkianzia huko Jeshini mliko na pia mwende mpaka sehemu nyingine za nje muweze kuwapa elimu ya kutosha vijana wetu ili waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niokoe muda ili nitoe nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge wengine pia waweze kuzungumza. Lakini nawaomba basi vijana wengine wote wa Tanzania waige mfano mzuri ambao umeonyeshwa na vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii ya vijana wetu, Ndugu Koplo Samson Ramadhan na Ndugu Fabian Joseph. Binafsi kwa niaba ya wananchi wa Kisiwa cha Mafia natoa pongezi kwenu kwa kutuweka katika chati ya dunia ya mashindano hayo mliyokwenda. Sasa Tanzania kama walivyosema wenzangu, siyo vichwa vya mwendawazimu, tunaweza kumbe tukashinda michezo mingi kabisa ya kila aina. Hii inatokana na juhudi zenu kwa ajili ya kuitangaza nchi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nilikuwa naomba nitoe ushauri kwa Serikali kwamba mfano huu usiishie hapa leo kwa vijana wetu, uende na kwa wengine watakaojaliwa kushinda ili waweze nao kuja kupewa motisha kama hizi na nyingine ili waweze kuzidi kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lingine, mimi nimefurahi sana juzi baada ya kurejeshwa hii mitaala katika Shule za Msingi. Nafurahia sana sasa michezo ikianzia kwenye Shule za Msingi na kuendelea, basi hali itakuwa nzuri zaidi kwa vijana wetu kuwatangaza hata kutoka Mafia, maana yake mara nyingi ndiyo huwa zinatoka Kanda ya Kati na Kaskazini. Kumbe hata sisi Wandengereko na Wazaramo tunaweza tukakimbia! Kwa hiyo, mimi nawatakieni kila la kheri na afya njema na ninawatakia wanamichezo wote waweze

kufanya vizuri zaidi na binafsi ninayo furaha. Hongereni sana. Naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami nizungumze kidogo kuhusu vijana wetu. Nimejawa na furaha kuwaona vijana wetu mbele yetu wametutoa aibu na wametufariji Watanzania. Nina imani vijana wengine ambao hawamo katika Bunge hili wanaona nyie kama mashujaa wetu. Hakika mmetuweka kwenye ramani hata Mzungu ambaye alikuwa amelala hafikirii Tanzania iko wapi sasa hivi anaweza akaangalia kwenye ramani, hawa wametoka wapi? Tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina imani tungekuwa na vijana wengine zaidi, kama tungekuwa na utaratibu wetu wa zamani ule wa michezo kwa vijana wa Sekondari na vijana wa Shule ya Msingi kama michezo ingeendelea. Kumekuwa na badiliko hapo nyuma. Nadhani sasa kwa sababu hili tunalivalia njuga na umri wangu hatuwezi kuingia kwenye kushindana; na kwa kuwa tunao wale vijana ambao wana nguvu walioko katika Shule za Msingi na walio katika Shule za Sekondari, ule utaratibu urudi ila uangaliwe utaratibu ambao hauwezi kuharibu masomo, ukashusha tena kiwango cha elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu Kenya kwenye michezo wanawapeleka vijana wetu kwa sababu wana utaratibu mzuri, hawaharibu kipindi hata kimoja. Kwa hiyo, kama tukifanya utaratibu huo utakuwa mzuri. Niliwahi kuwaandikia Wizara ya Elimu na Utamaduni miaka iliyopita kwamba wafuate utaratibu ule, kwani tutapata wachezaji wengi sana. Kwa kweli mimi nimefurahi na nadhani Vyuo vyetu sasa vya Michezo vitaimarika na vitafanya vizuri. Kwa kweli mmetufariji sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Pia napenda kutoa pongezi kwanza kwa Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa kuweza kuleta hoja hii hapa Bungeni.

Pili, napenda kuwapongeza vijana hawa kwa ushindi mkubwa waliotuletea hapa nchini Tanzania na kuweza kulitangaza jina la Tanzania dunia nzima ikatambulika kwa sehemu hii ya riadha. *(Makofi)*

Vilevile napenda kuomba kwanza kwa sababu hawa wametuletea sifa nzuri na tumeweza kuona faida ya michezo, mimi kama mwanamichezo ambaye nimetoka kwenye fani ya michezo kama Afisa Michezo, halafu vile vile nimesomea fani hiyo, naomba waitangaze Shule ya Arusha ya Michezo ili iweze kutambulika hapa Tanzania nzima, ikiwezekana Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania waweze kupeleka watoto wao huko ili kuongeza kipaji hiki cha michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuipa kipaumbele fani hii ya michezo hadi kufikia kupata medali kama hizi. Nafikiri kama yeye asingetoka katika nafasi hii nzuri kwa michezo kama alivyoitoa kwenye hotuba yake wakati anafungua Bunge jipya, haya maendeleo

tusingeyapata. Japokuwa tulikuwa tunayapata siku za nyuma mmoja mmoja, lakini sasa hivi naona tutapata wengi zaidi kwa sababu Mheshimiwa Rais amelivalia njuga suala la michezo. *(Makofi)*

Halafu vilevile, mimi kama mwanamichezo, namalizia kwa kusema kwamba nawaomba Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili wale ambao hawashughuliki kwenye michezo wajiunge asubuhi kwenye mazoezi kule Uwanja wa Jamhuri wafanye mazoezi kama wanavyofanya Waheshimiwa Wabunge wengine. Tunawakaribisha pale kwa ajili ya afya zenu na kwa ajili ya kuipa nafasi hii fani ya michezo ionekane kwamba ni fani bora.

Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuwapongeza vijana wetu ambao wamefanya vizuri katika michezo ya Jumuiya ya Madola.

Mheshimiwa Spika, lakini awali ya yote kwanza nikupongeze wewe mwenyewe kwa utamaduni ambao umeuanzisha ambao haujapata kutokea katika Bunge letu. Hawa ni vijana mbali na Viongozi Wakuu wa Nchi ambao wamepata kuingia katika Bunge hili Tukufu. Ni watanzania wa kwanza na wananchi wa kawaida waliopewa heshima kuweza kuingia katika Bunge hili. Ni kwa sababu ya kuwa na Mheshimiwa Spika ambaye anatazama viwango. Napenda nikupongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi binafsi, Chama changu pamoja na Watanzania wote tunapenda kuwapongeza sana vijana hawa kwa haya ambayo wameweza kuyafanya. Eneo la michezo ni eneo ambalo tulikuwa tunaliona linapuuzwa sana. Lakini napenda pia niseme kwamba Serikali ya Awamu ya Nne imeweza kuona dosari hizi na imeanza kutoa kipaumbele katika kusimamia michezo ipasavyo. Nami napenda niipongeze Serikali kwa juhudi za awali ambazo imeanza kuchukua na kuanza kuthamini michezo. Michezo kama zilivyo fani nyingine na tamaduni ni moja katika vielelezo vya kuonyesha Utaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijana hawa wameweza kuitangaza nchi yetu kwa sababu ya kutumia miguu yao. Tuna vitu vingi ambavyo tunaweza tukavitumia kama Serikali itaangalia na kusaidia kuwekeza katika michezo. Naamini kabisa Watanzania tunaweza tukafanya vizuri, sio kwenye riadha peke yake, naamini kabisa kwa jitihada ambazo Mheshimiwa Rais ameanza kuzichukua za kukihimiza, Chama cha Mpira wa Miguu kuweza kujirekebisha. Nina matumaini makubwa kwamba baadaye timu yetu ya Taifa ya Mpira wa Miguu nayo inaweza kufanya maajabu kama waliyofanya vijana hawa.

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kuwaomba hususan vijana, najua watu wa rika langu hawana nafasi tena ya kuweza kuiletea medali nchi hii. Lakini vijana wana nafasi kubwa na wanaweza kabisa kama wataongeza juhudi na maarifa na Serikali ikawasaidia katika kuwekeza katika mafunzo, vijana hawa watafanya vizuri na nchi hii itapata heshima kubwa katika fani ya michezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninarudia tena kusema kwamba Koplo Nyoni na mwenzake hapa mimi ninawapongezeni sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutakuwa na wachangiaji wawili tu. Nimepata maombi kutoka kwa wengine 12 ambao nitawataja tu majina kwa heshima kuonyesha kwamba walikuwa na nia ya kuwaunga mkono vijana wetu, lakini hawakupata nafasi. Lakini nitakaowapa nafasi kwa sababu ndivyo tulivyopanga toka mwanzo ni Mheshimiwa Martha Mlata na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora Mheshimiwa Philip Marmo.

Wafuatao ndiyo wametuma maombi, lakini namna tulivyopanga jambo hili na ukizingatia kwamba vijana hawa wanachelewa kwenye mazoezi, hawa kazi yao siyo maneno maneno. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mheshimiwa Idd Mohamed Azzan, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Fatma Mikidadi na Mheshimiwa Dr. Omari Nibuka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana, tunaelewa wote tumefurahi na nchi nzima imefurahi, lakini nadhani waliosema na hawa watakaomalizia wanatosha. Pia, nimepata maoni mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Cynthia Ngoye ambayo ni ya maandishi, nitayafikisha Serikalini. Sasa namwita Mheshimiwa Martha Mlata azungumze kwa kifupi na atamalizia Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala wa Bora. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na mimi kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuongea haya machache niliyonayo.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikupongeze wewe binafsi pamoja Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutoa heshima kubwa sana kwa hawa wachezaji kuwapa ridhaa ya kuweza kuingia ndani ya Bunge hili Tukufu ili tupate kuwapongeza. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niungane na Wasemaji waliotangulia kutoa pongezi za dhati kabisa kwa vijana ambao wameweza kushinda. Lakini mimi sitakuwa mwingi wa fadhila nikiacha kumpongeza mama Museven pamoja na mtoto wake, maana huo ni mgawanyo wa madaraka na kazi. Wakati baba akiwa mazoezini au kwenda kushiriki katika michezo, basi mama anakuwa mwangalizi wa familia, nyumba pamoja na afya ya baba pia. Kwa hiyo, nakupongeza sana mama Museven kwa kumtunza mume wako vizuri hatimaye ameweza kushinda medali ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana Mkuu wa Majeshi kwa kutambua umuhimu wa medali hiyo na kuweza kumpandisha cheo cha Ukoplo, nampongeza sana. Lakini pia sio vibaya sana kama nikiendelea kumwombea maana medali ya dhahabu imetuletea sifa kubwa sana ndani ya nchi yetu. Angemsogeza kidogo akawa hata *Sergeant* kwa ombi hili nadhani limefika mahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nashukuru sana kwa sababu mimi ni Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, basi nipende kumpongeza kwa sababu ametoka Singida, naamini Singida itatazamwa kwa mtazamo wa peke yake kwamba wachezaji wa mbio za namna hii wako wengi. Kwa hiyo, namwomba Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo aelekeze nguvu zake kule kwa watu wa namna hiyo. Wako wengi sana, tutapata medali za dhahabu nyingi sana! Wako Vijijini hawa wanamichezo. Ninaomba Wizara ielekeze macho yake kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, basi nitoe wito pia kwa wachezaji wengine wenye vipaji mbalimbali wasikate tamaa kwa sababu Serikali ya Awamu ya Nne hakika imezingatia na kuelekeza nguvu zake kwenye michezo na mfano tunauona kwa vitendo. Kwa hiyo, tunawakaribisha waendelee kuonyesha vipaji vyao.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adimu sana ili niwapongeze vijana wetu hawa kwa kuiletea nchi yetu sifa kubwa.

Mheshimiwa Spika, tukio hili la sasa kwa kweli ni tukio la pekee kabisa katika historia ya Bunge letu. Bunge hili kutengua Kanuni zake kuwaruhusu wageni hutokea mara chache sana. Wewe mwenyewe umesema ni pale ambapo unaruhusu Viongozi wa Juu sana wa Kitaifa na Viongozi wa Nchi na mara nyingi ni Viongozi wa Nchi ambazo wamechaguliwa kidemokrasia. Hivyo, vijana hawa pamoja na vijana wengine wa Tanzania waone tukio hili kama tukio siyo tu kuwaenzi, lakini tukio ambalo wenzetu walione kwamba fedha siyo lolote isipokuwa kuipatia nchi yako heshima ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi, kwa sababu wakati wa maandalizi ya michezo hii ya riadha kulikuwa na vijana wengi ambao laiti wangekuwa hapa nchini wakashindanishwa wakapimwa wangelikwenda wengi zaidi na pengine tungelipata medali nyingi zaidi. Hawakuwepo kwa sababu wengi wametapakaa katika sehemu mbalimbali duniani wakikimbia kwa kulipwa, wakifanya michezo ya ngumi kwa kulipwa, basi ukurasa mpya tuliofungua leo, basi uwe ni mwanzo na wale ambao walikuwa wakibeza michezo hii ya *Olympic* ya Jumuiya ya Madola kwamba ni muhimu sana na inaheshimika sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, mimi ni mmoja wa wale ambao wanaunga mkono hoja ya kurejesha michezo Shuleni ikiwa ni pamoja na kurejesha mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA ambapo vipaji hivi vinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa mara nyingine kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima sasa nitawaomba hawa vijana wasogee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wamwonyeshe hizo medali ili azione kwa niaba yetu na baada ya hapo anaweza akasema mambo mawili, matatu. *(Makofi)*

*(Hapa tukio la kuonyesha Medali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu lilifanyika)*

*(Hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu alizionyesha Medali hizo kwa Waheshimiwa Wabunge)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe kwa uamuzi huu ulioufanya wa kuwaleta vijana hawa mbele yetu. Umefanya uamuzi mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini inatuonyesha hatukukosea siku ile tulipokuchagua maana ulituambia utaweka viwango na viwango hivi tumeanza kuviona kwamba kila anayefanya kwa viwango vinavyopaswa anakuja Bungeni kupewa sifa. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kujiunga na Waheshimiwa Wabunge na wote wale ambao wamewapongeza vijana hawa kwa kutujengea heshima kubwa sana. Hongereni na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina hakika siku ile Koplo Nyoni aliposhinda halafu Bendera ya Tanzania ikawekwa pale na wimbo wa Taifa letu ukapigwa, alikuwa anamwakilisha kila Mtanzania popote alipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana uamuzi wako wa kuwaleta hapa Bungeni ili Watanzania wanaowakilishwa hapa Bungeni wawapongeze ni uamuzi wa kuenziwa sana. Tunakushukuru sana na tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawapongeza pia na kuwashukuru Mkuu wa Majeshi kwa uamuzi wake wa kumzawadia Koplo Nyoni. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuwasilisha hoja vizuri sana na historia nzuri aliyotoa juu yao. Lakini wote tukiri kwamba tukiendelea na utaratibu huu wa kuwaenzi Watanzania hivi heshima ya nchi yetu itakuwa juu na nina hakika tutashinda katika michezo mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nina hakika hata wale wanaokwenda nchi za nje hata wakishinda hawatapata heshima ya kwenda kwenye Mabunge ya nchi zile. Heshima ya

kuja kwenye Bunge utaipata katika nchi yao na ndiyo mmeipata vijana wetu. Hongereni na ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami ninajiunga na Mheshimiwa Martha Mlata kumpongeza Mama Museven na Museven mdogo. Maana mama Museven na Museven mdogo walikuwa na mchango kwa Koplo Nyoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema yafuatavyo:- Kwamba, tumeshauriana mimi na wewe na kukubaliana kuwaenzi vijana wetu kwa kitu kidogo kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Mheshimiwa Spika inampa Koplo Nyoni Shilingi milioni moja na inampa Fabian Joseph Shilingi laki tano. Ofisi ya Waziri Mkuu inampa Koplo Nyoni Shilingi milioni mbili na Fabian Joseph Shilingi milioni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Hapa Ukumbi mzima ulirindima kwa vifijo na nderemo)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama ambavyo imekuwa kawaida kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne, mambo yake yanakwenda kwa kasi, nadhani mmeona majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hakika bila yeye na yeye ndiye anayeunganisha shughuli zote za Serikali, kwa hiyo, nilipoomba kwamba vijana watambuliwe lingeweza likaishia katika maneno tu. Lakini nilimtarajia yeye, amewezesha kukusanya nguvu zote za Serikali, vijana hawa walikuwa hawajui lolote hadi jana asubuhi na wamearifiwa jana, ndege imepatikana, wameletwa hapa, tumewalipia posho ya siku tatu wanakaa mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yote haya yamewezekana kwa sababu Serikali hii inaliunga mkono Bunge lake na sisi tutajitahidi kutimiza wajibu wetu kama Wabunge. Kwa sababu wananchi wanaonyesha matumaini sana kwako Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa Mheshimiwa Rais, tunawaombeeni afya njema mwendelee hivyo, kwa sababu nyota njema huonekana asubuhi. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, namwomba sasa *Ser-geant at Arms* awatoe wageni ili tuendelee na shughuli zetu.

*(Hapa msafara wa Wageni Waalikwa ulitoka nje ya Ukumbi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu shughuli za leo zimekwisha kabla saa ya kawaida ya kuahirisha Bunge, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu aweze kutoa hoja ya kuahirisha Bunge kabla ya wakati wake.

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI WAKE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kazi hii muhimu na nzuri sana ya kutoa heshima kwa vijana wetu waliofanya kazi nzuri ya kulijengea heshima Taifa letu huko kwenye michezo, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako liahirishwe sasa kabla ya wakati wake mpaka kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 12.25 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi tarehe 6 Aprili, 2006 saa Tatu Asubuhi)*